# Nipashe

Jumanne Aprili 2, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579881

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




## JPM aitaka TRA kupanga viwango kodi inayolipika

UKURASA 2


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI
JE, WAJUA? PAKA SHUME NA MBWA KOKO WANALAUMIWA KWA KUHARIBU
Mrima, Bara walivyovuruga Kiswahili cha Unguja, Pwani
Utatuzi migogoro nje ya Mahakama, nuru kwa pande zinazotofautiana

UKURASA 13

# Wananchi wajeruhi askari polisi watatu

• **Walikuwa** wakimwokoa mtuhumiwa ujambazi, lakini akauawa...*Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**KANUNI MPYA ZAJA MADUKA YA FEDHA**
UKAGUZI wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni uliofanywa na...

UKURASA WA 3
**MENEJA BENKI AELEZA MAZITO KESI AVEVA**
MENEJA wa Benki ya Barclays tawi la Mikocheni jijini Dar es Salaam...

UKURASA WA 26
**MAALIM SEIF AJIWEKA KANDO MADENI CUF**
ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), ambaye...


## Hoja sita kutikisa Bunge

UKURASA 3



Rais John Magufuli akizungumza jambo na Mbunge wa Arusha Mjini (Chadema), Godbless Lema, baada ya kutoa heshima za mwisho kwenye msiba wa marehemu Tryphosa Simon Sanga ambaye ni dada wa Mbunge wa Iringa Mjini (Chadema), Mchungaji Peter Msigwa (kushoto), Kimara, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Mashirika 65 yamjia juu Msajili Vyama vya Siasa

UK.2


**MICHEZO** AUSSEMS AKILI JESHINI, AIPOTEZEA MAZEMBE UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wananchi wajeruhi askari polisi watatu

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

POLISI watatu wamejeruhiwa na wananchi mkoani Geita, walipokuwa wakimwokoa mtuhumiwa wa ujambazi asiuawe na wananchi.

Kutokana na shambulio hilo, askari hao wamelipata majeraha na kupelekwa zahanati, huku mmoja wao akihamishiwa katika Hospitali ya Rufani ya Bugando jijini Mwanza.

Hata hivyo, licha ya askari hao kutaka kumwokoa mtuhumiwa huyo, mkazi wa kijiji cha Lwamgasa wilayani Geita, Makoye Kengele (46), aliuawa na wananchi katika kijiji na kata ya Nyijundu wilayani Nyang'hwale mkoani Geita, kwa tuhuma za kuhusika na matukio ya ujambazi, huku wananchi 28 wakikamatwa kwa kuwashambulia na kuwajeruhi polisi.

Wananchi hao waliwashambulia askari hao wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Nyang'hwale, wakati wakiwazuia kumshambulia mtuhumiwa huyo.

Tukio hilo lilotokea kijijini hapo usiku wa kuamkia Machi 30, mwaka huu, baada ya kaya mbili kuvamiwa na kundi la watu wanaodaiwa ni majambazi wakiwa na silaha za jadi yakiwamo marungu na mapanga kisha kupora fedha na kujeruhi.

Baadhi ya mashuhuda waliliambia Nipashe kijijini hapo kwa nyakati tofauti kuwa mtumiwa huyo alikamatwa na wananchi katika kijiji jirani cha Iyogelo kisha kufikishwa kijiji cha Nyijundu ulikotokea uvamizi huo.

Waliongeza kuwa baada ya kumfikisha kijijini hapo walianza kumshambulia mtuhumiwa huyo na kuwa askari polisi waliwahi kufika eneo hilo kwa lengo la kumnusuru mtuhumiwa huyo, lakini ghafla wananchi walianza kuwashambulia askari hao kisha kuwajeruhi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Mponjoli Mwabulambo, alithibitisha tukio hilo na kusema kuwa mtuhumiwa huyo alikuwa akituhumiwa kuhusika na matukio ya ujambazi kijijini hapo na kuwa baada ya kuhojiwa alikiri.

Alifafanua kuwa wakati askari wakiwazuia wananchi wasimshambulie mtuhumiwa huyo, nao walianza kushambuliwa na wananchi hao.

Alisema askari watatu wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Nyang'hwale, Omary Nassoro na askari namba H 16 D/C Yusuph walipata majeraha na kutibiwa katika zahanati ya Nyang'hwale, huku mwenye namba H 4311D/C akijeruhiwa vibaya na kupelekwa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Geita na baadaye kuhamishiwa katika Hospitali ya Rufani Bugando jijini Mwanza .

Kamanda huyo alisema watuhumiwa 28 wanashikiliwa kwa tuhuma ya kuwashambulia askari polisi hao, huku akitangaza kiama kwa wananchi wanaojichukulia sheria mkononi, kwamba Jeshi la Polisi halitasita kuwachukulia hatua watakaokaidi.

Pia alilaani vikali kitendo cha askari kupigwa na wananchi wakati wakitekeleza majukumu yao.

Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi (wa pili kulia), akipanda mti kama ishara ya kumsherehekea Profesa Wangari Maathai, mwanaharakati wa mazingira kutoka Afrika Mashariki, katika tafrija fupi iliyoandaliwa na Ubalozi wa Kenya jijini Dar es Salaam jana na kuhudhuriwa na mabalozi mbalimbali wa nchi za Afrika, wawakilishi kutoka sekta binafsi na Umoja wa Mataifa. Katikati ni Balozi wa Kenya hapa nchini, Dan Kazungu, Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani (kulia) na wafanyakazi wa ubalozi huo. **NA MPIGAPICHA WETU**



## Mashirika 65 yamjia juu Msajili Vyama vya Siasa

**Na Beatrice Shayo**

ASASI 65 za kiraia zimemjia juu Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, zikimtaka kuacha kutengeneza migogoro ndani ya vyama vya siasa, badala yake awe mlevi wa vyama hivyo.

Hayo yamo kwenye tamko la vyama hivyo kuhusu hali ya demokrasia, haki ya kujumuika na kujiunga na vyama vya siasa nchini, lililotolewa jana jijini Dar es Salaam na Mratibu wa Mtandao wa Kutetea Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumo.

Olengurumo ambaye alizungumza kwa niaba ya asasi hizo, alimtaka Jaji Mutungi aache kuvitisha vyama vya siasa, badala yake aongozwe zaidi na hekima katika kusimamia misingi ya demokrasia na haki za wananchi kujiunga na vyama.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili wameshuhudia haki ya demokrasia, uhuru wa kujumuika na kujiunga na vyama ikizidi kuzorota kila uchao.

Alisema wanaitafsiri hali hiyo kuwa ni mwanzo wa

INAENDELEA UK. 8

# JPM ataka TRA itoze watu kodi inayolipika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli ameitaka Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA), kujenga mazingira rafiki kwa watu na kuweka viwango vya kodi vinavyolipika na vitakavyowavutia watu wengi zaidi kulipa kodi.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla ya kumuapisha Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango atakayeshughulikia Sera, Adolf Hyasinth Ndunguru na Naibu Kamishna Mkuu (TRA), Msafiri Lameck Mbibo.

Hafla ya kuapishwa kwa viongozi hao ilihudhuriwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Prof. Palamagamba Kabudi, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Ashatu Kijaji, Makatibu Wakuu, Viongozi Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama na wafanyakazi wa Wizara ya Fedha na Mipango.

Rais Magufuli aliitaka TRA na Wizara ya Fedha na Mipango kupanua wigo wa kodi kwa kuongeza idadi ya walipa kodi na kuibua vyanzo vipya vya mapato, pamoja na kujenga mazingira rafiki kwa watu wengi zaidi kulipa kodi ili kuongeza makusanyo.

Alielezea kutoridhishwa na utendaji wa TRA ambayo mpaka sasa inakusanya kodi kwa walipa kodi milioni 2.7 pekee kati ya Watanzania wote zaidi ya milioni 55 na alisema kwa mtindo huo TRA itakuwa inazidi kukamua walipa kodi wachache wakati ingeweza kupanua wigo wa kodi na kuweka viwango vya kodi vinavyolipika na vitakavyowavutia watu wengi zaidi.

"Ukienda mipakani wafanyabiashara wanafungua maduka upande wa nchi za wenzetu na sio upande wa Tanzania, na sababu ni kwamba wakifungua upande wa Tanzania wanasumbuliwa na TRA, wekeni viwango vya kodi vinavyolipika ili watu wengi waweze kulipa kodi badala ya kukwepa," alisisitiza Rais Magufuli.

Rais Magufuli alielezea kutofurahishwa na mrundikano wa kesi za kodi mahakamani na alitaka tatizo hilo lifanyiwe kazi kwa kuwa linasababisha kodi nyingi kutolipwa

INAENDELEA UK. 8


## TAUSI AUCTION MART & COURT BROKER CO. LTD

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa kisheria ya kukusanya madeni sugu na kufanya Minada,Tutauza dhamana za wadaiwa wa **PROUD MICROFINANCE LTD** kama ifuatavyo:-

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Juma S. Ngole | Nyumba | Matosa karibu na shule ya sekondari | 13/04/2019 | Saa nne na nusu Asubuhi |
| 02 | Othman Issa Ndui | Nyumba | Matosa kwa komba | 13/04/2019 | Saa sita na Nusu Mchana |
| 03 | Sarah Hoseah Chamla | Kinzudi/Majengo-Mkupita Road | 17/04/2019 | 17/04/2019 | Saa nne Asubuhi |
| 04 | Lilian Meshack Luoga | Nyumba | Msumi | 17/04/2019 | Saa saba Mchn |
| 05 | Miraji Juma Hanje | Kiwanja 26 * 25 | Mpiji Majohe | 20/04/2019 | Saa nne Asbh |
| 06 | Mwajuma S. selemani | Nyumba | Msakuzi karibu na S/Mtaa | 20/04/2019 | Saa sita Mchana |
| 07 | Joseph P. Kombe | Kiwanja 16*13 | Saranga Mtaa wa Ukombozi | 21/04/2019 | Saa sita Mchana |
| 08 | Germana I. Mchungu | Kiwanja | Kibaha/Kidimu karibu na Shule | 27/04/2019 | |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% papo hapo baada ya nyundo ya Dalali kupigwa na 75% italipwa ndani ya siku 14.
2. Ukaguzi wa mali unaruhusiwa kufanyika siku mbili kabla ya siku ya Mnada. Gharama za kubadilidha Umiliki na makabidhiano mengine zitakuwa ni juu ya Mteja.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**
TAUSI AUCTION MART & COURT BROKER CO. LTD AU PROUD MICROFINANCE LTD
P.O.BOX 71418- DAR ES SALAAM P.O.BOX 63316- DAR ES SALAAM
0764 -351 040 0786- 004 744
0713- 237 650 0715-804 450

215151102



## REQUIREMENT OF WAREHOUSE

We urgently require spacious warehouse for immediately long term lease with below specifications

**Capacity –** 3000 to 5000 square meters
**Location –** Along Nyerere/Pugu Road and/or Chang'ombe
**Accessibility –** Should be accessible by road throughout the year
**Entrance –** Entrance to containerized cargo is a must for both 20 & 40 feet containers 24/7

**Space –** Should have sufficient space to carry out both offloading from containers and loading customer's vehicles simultaneously

**Ownership –** The owner should possess sufficient and credible evidence regarding title, registration and other statutory requirements Middlemen not entertained

Interested parties to call
+255 784 /620 305 085; +255 713 254 912
Or send email to info@diy.co.tz

215146302

# Kanuni mpya zaja maduka ya fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UKAGUZI wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa mikoa ya Arusha na Dar es Saalam, umebaini dosari saba ikiwamo kuathiri usalama wa nchi.

Kufuatia dosari hizo hivi sasa serikali inaandaa kanuni mpya kwa ajili ya biashara hiyo ambazo zitaelekeza jinsi ya kuomba leseni za uendeshaji wa maduka hayo kwa mtu binafsi au taasisi yoyote na masharti ya kuzingatiwa wakati wa shughuli hizo.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alitoa taarifa hiyo wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kuhusu ukaguzi uliofanywa kwenye maduka hayo na serikali kupitia BoT.

Alisema maduka mengi yaliyofanyiwa ukaguzi huo yamebainika kuendesha shughuli zake kinyume cha sheria ya ubadilishaji wa fedha za kigeni ya mwaka 1992, kanuni zake za mwaka 2015 na marekebisho ya mwaka 2017 pamoja na taratibu za utoaji wa huduma za ubadilishaji fedha za kigeni.

Alisema kufuatia hali hiyo zoezi maalum la ukaguzi wa kina wa maduka hayo lilifanywa Arusha mwezi Novemba 2018, Dar es Saalam, Februari 29, 2019 na Machi 1 na 8, mwaka huu kwa kuhusisha vyombo vya dola na kubaini ukwepaji mkubwa wa kodi na uvunjaji wa sheria.

"Zoezi hili limebaini pia uondoshwaji wa fedha katika mfumo rasmi wa fedha na kuelekezwa kwenye mifumo ya utakatishaji wa fedha haramu, kupokea amana kutoka kwa wafanyabiashara kinyume cha matakwa ya leseni za biashara husika, kudhoofisha thamani ya shilingi, pamoja na mambo mengine ambayo yalianza kuathiri usalama wa nchi kwa ujumla," Dk. Mpango alisema na kuongeza:

"Kwa mfano baadhi ya maduka yaligundulika kutumia fedha nyingi za Tanzania kununua fedha za kigeni, lakini fedha kidogo za kigeni ziliuzwa na hakuna taarifa ya matumizi ya fedha za kigeni zilizobaki," alisema.

Alibainisha kuwa zoezi hilo la ukaguzi wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni lilitekelezwa kwa kuzingatia sheria za nchi, tofauti na malalamiko na tuhuma mbalimbali zilizotolewa za kudai uwapo wa ukiukwaji wa sheria na haki kwa wamiliki wa maduka hayo.

"Jambo la kushangaza ni kwamba hakuna mmliki yeyote wa duka aliyewasilisha malalamiko kuhusiana na zoezi hili kwenye mamlaka husika, hata hivyo Benki Kuu ya Tanzania na mamlaka nyingine za serikali zinafuatilia kwa umakini ili kubaini ukweli wa tuhuma hizo zinazotolewa," alisema.

Dk. Mpango alisema kuwa serikali ya awamu ya tano inatekeleza majukumu yake kwa umakini, hivyo anauthibitishia umma wa Watanzania kuwa katika zoezi la ukaguzi wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni hakuna fedha wala mali yoyote iliyotaifishwa.

"Taratibu za kisheria zilifuatwa wakati wa kuchukua vielelezo mbalimbali zikiwamo fedha, kompyuta, simu za viganjani, mashine maalum za kuhifadhi taarifa na taarifa mbalimbali ili kusaidia uchunguzi," alisema.

Pia alisema lengo la zoezi hilo siyo kufuta biashara ya maduka ya kubadilishia fedha za kigeni kwa watu binafsi, bali ni kudhibiti ukiukwaji wa sheria uliokithiri, ukwepaji wa kodi na utakatishaji wa fedha haramu.

Naye Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, alisema kuwa katika ukaguzi huo kwa Mkoa wa Dar es Saalam, jumla ya maduka 87 yalikaguliwa.

Prof. Luoga alisema kati ya maduka hayo, matano pekee ndiyo yaliyokuwa yanakidhi vigezo na mengine 82 yalikuwa hayastahili kuendelea kutoa huduma hiyo na kupewa notisi ya kuyafunga.

"Tayari tumeshatoa notisi katika maduka yote nchini ambayo hayakidhi vigezo vya kuendelea kuendesha huduma hii ya ubadilishaji wa fedha za kigeni na uchunguzi bado unaendelea hatua zaidi zitachukuliwa baadaye dhidi ya wahusika wote," Prof. Luoga alisema.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati), akiongoza kikao cha Kamati ya Kanuni za Bunge kilicholenga kupokea na kujadili waraka wa Spika kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya nyongeza ya nane katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kilichofanyika katika Ofisi za Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Meneja wa benki aeleza mazito kesi vigogo Simba

**Na Hellen Mwango**

MENEJA wa Benki ya Barclays tawi la Mikocheni jijini Dar es Salaam, Prisca Saudi (39), amedai kwamba akaunti binafsi ya aliyekuwa Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva, iliingiziwa Dola za Marekani 300,000 kama malipo ya mkopo kutoka akaunti ya klabu hiyo iliyopo benki ya CRDB.

Shahidi alitoa madai hayo jana dhidi ya kesi ya kutakatisha Dola za Marekani 300,000 inayomkabili Aveva na aliyekuwa Makamu wake, Godfrey Nyange maarufu kama 'Kaburu' na mfanyabiashara Zakaria Hans Poppe.

Ushahidi huo ulitolewa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Akiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai, meneja huyo alidai Machi 16, 2016 akaunti ya Aveva iliyopo katika benki ya Barclays ilipokea Dola za Marekani 300,000.

"Mheshimiwa hakimu dola hizo zilipoingia taarifa yake ilieleza kwamba Klabu ya Simba inamlipa deni la mkopo Aveva," alidai shahidi Daudi.

Alidai baada ya kuingia dola hizo, mteja wao alikuwa akizitoa kwa nyakati tofauti na nyingine zikiingia.

Alidai Aprili, 2016, Aveva alihamisha Dola za Marekani 62,183 kuilipa Kampuni ya Nina Guangzhou Trading Limited ya China kwa lengo la kuagiza nyasi bandia.

Alidai baada ya mteja kutoa na kupokea dola nyingine hadi kufikia Novemba 26, 2018 akaunti hiyo ilikuwa na balansi ya Dola za Marekani 2,751.38.

Katika kesi ya msingi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Shadrack Kimaro, alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Machi 10 na 16, 2016 Aveva na Kaburu walikula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya ofisi.

Shtaka la pili, ilidaiwa katika tarehe tofauti kati ya Machi 10 na 16, 2016 jijini Dar es Salaam, Aveva na Kaburu walifanya matumizi mabaya ya madaraka kwa kuandaa hati ya kuhamisha Dola za Marekani 300,000 kutoka akaunti ya Klabu ya Simba benki ya CRDB tawi la Azikiwe kwenda akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays tawi la Uhio.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa shtaka la tatu, Machi 15, mwaka 2016 Aveva na

INAENDELEA UK.8

## Hoja sita kutikisa Bunge

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

MKUTANO wa 15 wa Bunge la Bajeti, unaanza vikao vyake jijini Dodoma leo, huku hoja sita zikitarajiwa kutikisa mkutano huo.

Hoja hizo ni pamoja na vipaumbele vya serikali mwaka 2019/20, bajeti za kila wizara, hatima ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG), Prof. Juma Assad na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

INAENDELEA UK.8




# Walalamikaji 6 kesi DECI wakamatwa kortini

**Na Hellen Mwango**

JESHI la Polisi limewakamata walalamikaji sita kati ya 18 jana katika viunga vya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam dhidi ya Kampuni ya Development Entrepreneurship for Community Initiative (DECI), kwa madai kuwa katika hati ya kiapo walichokiwasilisha mahakamani hapo, walikiri kucheza upatu huo na kulipwa fedha.

Kesi hiyo imesikilizwa mbele ya Jaji Stephen Magoiga.

Walalamikiwa 18, wanaiomba Mahakama Kuu iamuru walipwe Sh. bilioni 2.4 katika mali ambazo Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) inaomba zitaifishwe na serikali.

Walalamikaji waliokamatwa jana ni Andrew Kagutwa, Frida Msuva, Imelda Tarimo, Jackson Nyella, Thadeo Mgoso na Philemon Mwaluko, moja kwa moja walipelekwa Kituo Kikuu cha Polisi kwa tuhuma za kukiri kwa kiapo cha kucheza upatu huo.

Walalamikaji wengine ambao hawajakamatwa ni, Joseph Kessy, Samwel Tarimo, Nobel John, Aden Kimambo, Jacline Chacha, Vincent Chacha, Christina Mkundi, John Kulwa, Joseph Mnangu, Oliver Ndanshau, Omary Kimossa na Energy Petroleum (T) LTD ambao wametakiwa kufika mahakamani hapo leo.

Hatua hiyo ilikuja baada ya mahakama kuahirisha kusikiliza maombi namba 65/2019 na namba 45/2019 ambayo watu hao kupitia mawakili Charles Mutakyawa na Majura Magafu, wanaomba mahakama kwamba katika mali zilizoombwa na serikali zitaifishwe, iwalipe kwanza Sh. bilioni 2.4.

Wadai hao walikiri kupanda kila mmoja Sh. 300,000 na kuvuna kwa gharama tofauti kwa kadiri ya upandaji wa mbegu zao.

Katika maombi namba 42/2019, DPP anaiomba mahakama kutaifisha mali zilizotumiwa na DECI zenye thamani ya Sh. bilioni 14.

Awali, DPP Biswalo Mganga, aliiomba mahakama hiyo kuamuru walalamikaji katika maombi namba 65/2019 wote 18, wafike mahakamani hapo ili wawatambue kama ni wale waliohusika katika kupanda mbegu au la.

Alidai kuwa wana haki ya kuwatambua waleta maombi hao kwa sababu masuala yaliyojitokeza katika maombi hayo ni ya kitaalamu na kutokana na maslahi ya umma, amelazimika yeye mwenyewe kusikiliza kesi hiyo.

Alidai miongoni mwa mambo yaliyojitokeza ni kughushiwa kwa saini za mawakili wawili wa serikali ambao ni Theopil Mutakyawa na Wankyo Simon ili kuonyesha kuwa DPP, ameondoa rufani aliyoikata Mahakama ya Rufani jambo ambalo si kweli.

"Tulipobaini kuwa walighushi sahihi hizo mbili tumeona kuwa walioghushi ni wale wenye uhusiano na fedha hizi na nimeagiza Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI) kufanya uchunguzi kubaini waliohusika na hili sitalinyamazia," Mganga alidai.

Katika suala lililowasilishwa na Wakili Charles, kwamba wanaomba kuwasilisha vielelezo vitakavyoambatana na hati ya kiapo, DPP alidai kuwa hilo liko kinyume na utaratibu kwa sababu sheria iko wazi kwamba wanatakiwa kuwasilisha vielelezo vyote pamoja na hati ya kiapo. Jaji Magoiga aliamuru walalamikiwa wafike mahakamani hapo leo na mtu asiyefika ataonekana kama mfu na kuagiza DPP kuwasilisha hati kinzani pamoja na majibu yake ili shauri lianze kusikilizwa.

Hata hivyo, Wakili Charles alidai kuwa mmoja wa wateja wake, aliposwasilisha hati hiyo ya kiapo alisafiri kurudi Bukoba, hivyo hana uhakika kwamba ataweza kufika kesho badala yake apewe muda ombi ambalo halikukubaliwa.

## Serikali Mitaa zatajwa vinara kwa rushwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani Dodoma imetaja Serikali za Mitaa kuongoza kwa tuhuma na makosa ya rushwa kwa asilimia 25.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mkuu wa Takukuru, Sosthenes Kibwengo kuhusu utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa robo ya kwanza ya mwaka 2019, alisema Takukuru ilipokea taarifa za rushwa na makosa 96, huku serikali za mitaa ikiongoza kwa tuhuma za rushwa kwa asilimia 25.

Alizitaja sekta zingine na asilimia

INAENDELEA UK.8








Mkazi wa jiji akipita jirani na rundo la takataka zilizotelekezwa na mamlaka husika katika eneo la Makumbusho jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Afungwa jela miaka 30 kumbaka mwanafunzi

**Na Ibrahim Yassin,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, imemhukumu adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela na kuchapwa viboko 12 mfanyabiashara Anthony Mandawa (58), baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mwanafunzi na kumsababishia ujauzito.

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa wa Mbeya, Rashid Chengula, alisema Mandawa alitenda kosa hilo Februari mwaka jana na mahakama imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Hakimu Chengula alisema mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo kwa kumbaka mwanafunzi wa kidato cha kwanza aliyekuwa akisoma shule ya Upili Samora na kumsababishia ujauzito huku akijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Alisema Jamhuri kupitia mashahidi wake, akiwamo muathirika wa tukio hilo bila kuacha shaka, mfanyabiashara amefanya makosa yote mawili hivyo kumtia hatiani na kumpatia hukumu hiyo.

Awali katika utetezi wake, mshtakiwa Mandawa alikana kutenda kosa hilo, huku akikosoa mwenendo wa shauri hilo kwa madai kuwa muathirika alichelewa kutoa taarifa akidaiwa kuripoti baada ya siku 30.

Aidha, alidai kuwa yeye (mshtakiwa) ni muathirika wa ugonjwa wa Ukimwi na kujitetea kuwa mwanafunzi anayedaiwa kubakwa hajaathirika hivyo mahakama inathibitishaje kama kweli alimbaka.

Hata hivyo, mahakama ilisema utetezi wa mshtakiwa hauna mashiko ya kutomtia hatiani.

Shauri hilo lilikuwa likiendeshwa na mawakili wawili wa serikali, Davice Msanga ambaye aliiomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa Mandawa, ambaye ni mfanyabiashara na mkazi wa Isanga, alishtakiwa na Jamhuri kwa makosa mawili ya kumbaka mwanafunzi wa kidato cha kwanza kinyume na kifungu namba 130 (2) e na 131 (1) ya kanuni ya adhabu.

Kosa la pili ni kumsababishia ujauzito mwanafunzi huyo, kinyume na kifungu namba 60 A (3) cha Sheria ya Elimu sura ya 353 na marekebisho yake kifungu namba 22 (3) cha sheria namba 2 ya mwaka 2016.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Chengula, alisema mshtakiwa anahukumiwa kifungo cha miaka 30 jela na kuchapwa viboko 12 kwa kosa la kwanza ikiwa ni pamoja na kulipa faini ya Sh.milioni mbili.

## HABARI KITAIFA

# Waziri aagiza kuanzishwa soko la madini

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

NAIBU Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, ameelekeza soko la madini katika mkoa wa kimadini wa Kahama pamoja na maeneo mengine ya Chunya, Musoma, Singida kuanzishwa mara moja ili kudhibiti utoroshwaji wa madini unaosababisha serikali kukosa mapato.

Naibu Waziri Nyongo aliyasema hayo katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika mjini Kahama. Alisema baada ya kufanya ziara yake ya siku moja katika Wilaya ya Kahama, alibaini kumekuwapo na udanganyifu mkubwa katika shughuli za uchenjuaji wa madini huku akitoa mfano wa kampuni ya Busami inayojihusisha na uchenjuaji wa madini ya dhahabu.

Alisema alibaini kumekuwapo na udanganyifu kwenye uzito na kiwango halisi cha dhahabu kwenye madini yaliyopatikana hali inayosababisha serikali kukosa mapato yake stahiki.

"Kwa mfano katika mtambo wa kuchenjua dhahabu unaomilikiwa na kampuni ya Busami tumebaini kuna udanganyifu kwenye uchenjuaji, jana baada ya kufika na kuona namna uchenjuaji wa madini unavyofanyika na kuelekeza wataalam wa madini kuchenjua upya mchanga uliokuwapo kwenye maji yaliyohifadhiwa, tulibaini kuna madini," Nyongo alisema.

Katika hatua nyingine, alisimamisha shughuli za uchenjuaji katika kampuni ya Busami na kutaka hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi ya mmiliki wake.

Wakati huo huo, Nyongo alielekeza wamiliki wote wa mitambo ya kuchenjulia madini ya dhahabu nchini kuhakikisha wanakuwa na mizani na mashine maalum za kupimia madini ya dhahabu zilizoidhinishwa na Wakala wa Vipimo Tanzania, na biashara ya madini kufanyika katika masoko ya madini yaliyoanzishwa na kusisitiza kuwa lazima madini yajulikane yanapopelekwa na ofisi za madini nchini kuhakikisha zinatunza kumbukumbu sahihi.

# Mkurugenzi Global Space aitwa Takukuru

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA



TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imemtaka Mkurugenzi wa Kampuni ya Global Space East Africa Limited ya jijini Dar es Salaam, Gaston Francis, kuripoti mara moja Takukuru baada ya kubainika kufanya udanganyifu katika mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mima wilayani Mpwapwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Mkuu wa Takukuru, Sosthenes Kibwengo (pichani), kuhusu utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa robo ya kwanza ya mwaka 2019, alisema udanganyifu huo umeisababishia hasara serikali bila kutaja kiwango cha fedha.

Aidha, alisema kuwa katika kipindi hicho Takukuru ilifuatilia miradi ya Sh. bilioni 39.8 ya maendeleo ili kujiridhisha iwapo fedha zinatumika vizuri kwa wakati na iwapo miradi inatekelezwa kwa ubora na thamani halisi ya fedha inapatikana.

"Miradi iliyofuatiliwa ni katika sekta za maji, ujenzi, elimu na afya, katika miradi iliyofuatiliwa, Sh. milioni 900 inachunguzwa baada ya viashiria vya jinai kuonekana," alisema.

Kadhalika, alisema Takukuru imefanikiwa kuokoa Sh. milioni 152.3 ambazo zingelipwa kwa makandarasi ambao hawakutimiza majukumu yao ipasavyo.

"Pia tumebaini udanganyifu katika mradi wa ujenzi wa kituo cha afya cha Mima wilayani Mpwapwa, hivyo tunamtaka Mkurugenzi wa Kampuni ya Global Space East Africa Limited ya DSM, Gaston Meltus Francis ambaye kampuni yake ilipewa kazi hiyo, kuripoti mara moja kwenye ofisi zetu za Wilaya ya Mpwapwa," alisema.

**Miradi iliyofuatiliwa ni katika sekta za maji, ujenzi, elimu na afya, katika miradi iliyofuatiliwa, Sh. milioni 900 inachunguzwa baada ya viashiria vya jinai kuonekana.**

ROYAL DANISH EMBASSY

TADIYE

DTBi
DAR TEKNOHAMA BUSINESS INCUBATOR

## SHINDANO LA ANDIKO BORA LA BIASHARA; KUWASILISHWA MAOMBI

**Utangulizi**
Mradi wa uwezeshaji wa vijana (TADIYE) ni mradi wa kibunifu na kijasiriamali unaotekelezwa na Atamizi ya "DTBi" pamoja na washirika wengine wenye maono sawa kwa ufadhili wa Ubalozi wa Denmark. Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili vijana hasahasa wanawake wadogo wanaoishi kwenge mazingira magumu kwa kuwapatia elimu na ujuzi wa kijasiriamali kupitia simu za mkononi. Kwa kupitia elimu hiyo ya ujasiriamali kwa njia ya simu vijana hao wanaweza kutumia fursa za uchumi wa kidigitali kutengeneza ajira, kujitengenezea kipato na kuongeza wingi wa biashara endelevu.

Ili kuweza kufikia malengo yake, DTBi na washirika wake walikuja na mfumo wa kibunifu ujulikanao kama "BESP App" ambao unatumika kutoa elimu ya ujasiriamali mtandaoni kwa kutumia simu ya mkononi. Mfumo huu una masomo au moduli 8 ambazo zimetengenezwa kisanifu kuweza kukidhi mahitaji ya walengwa wa mradi wa TADIYE.
Shindano la Andiko bora la Biashara

Baada ya kujisajili na kupata mafunzo ya ujasiriamali kupitia mfumo wa "BESP" Mradi wa TADIYE unawapa walengwa wa mradi nafasi ya kushiriki katika shindano la andiko bora na la kibunifu. Kupitia shindano hili, vijana wenye mawazo ya kibunifu pamoja na wanawake wadogo wanaoishi kwenye mazingira magumu wataandaa na kuwasilisha mawazo yao ambayo yatafanyiwa uchambuzi kutumia kamati maalumu ya wabobezi wa maswala ya biashara na ujasiriamali. Katika shindano hili mipango bora ya biashara isiyopungua 20 ina nafasi ya kujishindia ruzuku ya mtaji unaofikia hadi kiasi cha shilingi za kitanzania milioni 20.

Kwa kutipia tangazo hili tunakaribisha maombi kutoka kwa vijana mbalimbali wenye mawazo ya kibunifu kuweza kushiriki kwa kuwasilisha maombi yao. Muda wa kuwasilisha mbaombi hayo ni siku 21 kuanzia tarehe ya kutolewa kwa tangazo hili na hakuna maombi yoyote yatakayokubaliwa baada ya muda ulioainishwa hapa.

**Sifa za muombaji**
- Lazima awe mwanaume au mwanamke mwenye umri wa miaka 15-35
- Lazima awe anatokea Tanzania Bara au Visiwani (Zanzibar)
- Lazima awe anazungumza Kiingereza au Kiswahili
- Lazima awe amejisajili na kupata mafunzo kupitia mfumo wa BESP and kukamizisha angalau masomo matano ikiwa ni pamoja na somo la ***Uandaaji wa Mpango wa Biashara***
- Wazo la biashara litakalowasilishwa lazima liwe na uwezo wa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) kama chombo au kiwezeshi cha wazo hilo.
- Wazo pendekezwa lazima liendane na sharia na taraibu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Kama wazo litaibuka na ushindi, muombaji atatakiwa kutumia fedha hizo kutekeleza wazo hilo au kuendeleza mradi wake na si vinginevyo

**Jinsi ya Kuwasilisha Maombi**
Maombi yote yatumwe kupitia mfumo maalumu wa uwasilishaji maombi unaopatikana kwenye website ya mradi wa TADIYE (**https://tadiye.or.tz**) kwa kubonyeza kutufe kilichoandikwa **"omba hapa".** Wanawake waishio kwenye mazingira magumu wanahamasishwa sana kuwasilisha maombi yao.

Kwa maelezo zaidi tembelea kurasa zetu za mitandao ya kijamii ya Facebook, Instagram na twitter (**@besptz or @tadiyetz**)

**Dar Teknohama Business Incubator**
**COSTECH Building, Ali Hassan Mwnyi Road, Box 4302, Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: +255766368387; Fax: +255222775313/4; +255 684 863 390**
**Email: admin@teknohama.or.tz; Web: www.teknohama.or.tz**

21515080Z

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri wabunge kikao cha bajeti

**KIKAO** cha Bunge la Bajeti kinaanza leo mjini Dodoma, wakati huo huo huko Visiwani Zanzibar Baraza la Wawakilishi linatekeleza jukumu kama hilo la kuisimamia serikali, kuishauri na kupitisha bajeti ya mwaka 2019/2020.

Zama hizi kote duniani wanahitajika wabunge wenye kujadili na kusimamia mijadala inayolenga kuhamasisha na kuleta matumizi bora ya fedha za umma kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Ni wazi kuwa Tanzania inahitajika wabunge wanaosimamia utendaji kazi wa serikali, taasisi za umma, pia wanaotunga na kuboresha sheria ili kuweka mazingira bora ya kufikia maendeleo endelevu.

Hivyo wanatarajia kuona wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakichambua, kufuatilia kwa kina bajeti za kila wizara na kuona kuwa fedha zinazotolewa kwa kila sekta, zinatumika kutimiza kile kilichopitishwa ili kufikia maendeleo yaliyokusudiwa kwenye bajeti wanazozijadili.

Wabunge na wawakilishi wana jukumu la kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwa kina kama inavyofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Macho na masikio ya Watanzania yanaelekezwa bungeni na Baraza la Wawakilishi ili wawasikie wakiibua mijadala na hoja zinazolenga kuleta maendeleo.

Kama ilivyo ada, wapigakura wanataka kuona wabunge wakionyesha ushahidi wa kazi za kuigwa au 'mbovu' walizoibua kwenye kuisimamia serikali majimboni na kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.

Wapiga kura wanataka kuona wawakilishi wao wakijadili kwa ushahidi, kwa kina na kwa uchambuzi visa mkasa vya wanaohujumu uchumi, mafisadi na pia kazi bora za mifano ambazo wawakilishi wa wananchi wamekutana nazo wakati wa kuisimamia serikali.

Tunahitaji kuwaona wawakilishi wetu Bara na Visiwani pamoja na kuonyesha mifano ya 'madudu' na 'mafanikio' waliyogundua kwenye kuisimamia serikali, wakiwa mstari wa mbele kupendekeza ufumbuzi na mbinu mbadala za kuondoa matatizo na changamoto zilizoko.

Tunapenda kuona wakifanya utafiti na kutoa mijadala yenye kuleta ufumbuzi wa matatizo yanayoikabili nchi badala ya kulaumu na kulalamika kila wanapochangia au kutoa hoja binafsi.

Tunahitaji kuona wawakilishi wetu wakiunda timu za kuhamasisha maendeleo. Kama kulivyo na wabunge wa wanaohamasisha umma kuhusu kujikinga na VVU na Ukimwi.

Wabunge wawe mstari wa mbele kuchagiza maendeleo na mkakati wa kuhakikisha kuwa taifa linaendelea kutokana na fedha za bajeti na kuweka mkazo kwenye usimamizi bora wa pesa za miradi ya maendeleo mijini na vijijini.

Aidha, taifa linataka kuona wabunge wenye ari ya kuleta maendeleo, kuhamasisha watendaji kuwajibika kuanzia wizarani, wilayani hadi vijijini. Kusisitiza kufanyakazi kwa bidii, kuwajibika na kuwa wafuatiliaji wa kazi za maendeleo badala ya kusimamia itikadi za vyama, kudharauliana na kupuuzana kwenye mijadala.


Tunatarajia kuona wabunge wakijielimisha na kufahamu masuala muhimu ya maendeleo ya taifa. Haitoshi kuwa mbunge kama huelewi mambo muhimu ya kisiasa ambayo Tanzania inahusika nayo.

Kwa mfano masuala ya kisheria, mikataba mbalimbali, sera, matamko ambayo ndiyo unapaswa kuyasimamia ili kuleta mabadiliko kwa wapigakura wako.

Tunawashauri wabunge kufanyakazi pamoja bila kujali vyama vyao na itikadi zao kwa sababu Tanzania ni yetu sote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tanzania itastawi tukiacha kufanya kazi kwa mazoea

Na Raphael Kibiriti

**MOJA** ya kikwazo kinachokwamisha gurudumu la maendeleo ya taifa ni cha watu kufanya kazi kwa mazoea.

Na ndiyo maana kinaendelea kupigwa vita kwa nguvu na serikali ya awamu ya tano, ili kisiwe sehemu ya utamaduni wa Mtanzania.

Kwa miongo sasa, suala la watu kufanya kazi zao kwa mazoea, likijionyesha kwa uwazi upande wa watumishi wa umma, limekuwa ni kama utamaduni wa kawaida.

Wahenga wanasema mazoea hujenga utamaduni na wataalamu mbalimbali wanabainisha wazi kuwa mazoea ni adui mkuu wa ufanisi, iwe katika sekta ya umma au binafsi, iwe kwenye biashara mpya au za zamani.

Kwa nini, kwa sababu katika zama hizi za mabadiliko makubwa ya maendeleo, zama za sayansi na teknolojia, zama za utandawazi, kunahitajika nidhamu ya kipekee ya utendaji kazi.

Nidhamu inayoongozwa na sheria, kanuni na taratibu za kitaasisi ili kuweza kufikia maendeleo ya watu na taifa kwa ujumla.

Na kwa kulitambua hilo, baada ya awamu ya tano kuingia madarakani, Rais John Magufuli aliwaonya watumishi wa umma kuachana na utamaduni huo.

Akachukua hatua madhubuti za kuwatumbua wale wote ambao hawakuendana na maelekezo yake ili kuonyesha anamaanisha anachokisema.

Dk. Magufuli akawataka wasaidizi wake kwenye wizara, idara, mashirika na taasisi za umma waongozwe na sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma zinazowataka wawatumikie wananchi kwa mujibu wa miongozo ya ofisi zao.

Hata hivyo, Muungwana anaona kwamba suala la kuchukulia vitu kwa mazoea ni kama imekuwa utamaduni si tu kwa watumishi wa umma, bali hata kwa wananchi wa kawaida.

Na matokeo yake, ndiyo hasara tunazoendelea kuzishuhudia kama nchi karibu kila siku.

Hasara za kupotea kwa maisha ya watu, wengine wakiambulia vilema vya maisha, uharibifu wa mali na hatimaye kuathiri uchumi wa nchi.

Hata hivyo, kinachomshangaza Muungwana ni kwamba bado baadhi yetu tunaendelea na utamaduni huo wa kufanya kazi kwa mazoea na hatusikii la mwadhini wala mnadi swala na hivyo kuishia kusababisha majanga makubwa.

Na hiyo ni pamoja na maelekezo, maonyo na tahadhari zinazotolewa na viongozi wa serikali, dini, kimila na taasisi mbalimbali, yanayobainisha madhara ya kufanya kazi kwa mazoea.

Kwa mfano utafiti mbalimbali uliofanywa nchini, unaonyesha asilimia 75 ya ajali za barabarani zinatokana na makosa ya kibinadamu, huku asilimia 50 ya makosa hayo yanahusiana na mambo ya kibinadamu yanayofanywa na madereva.

Lakini mpaka sasa bado unakuta dereva wa Kitanzania anaendesha gari huku akiongea na simu, akichati au akizungumza na mtu wa pembeni.

Bado unakuta dereva wa Kitanzania akipita kwenye taa ambazo hazimruhusu, hasimami kwenye alama za pundamilia ama akipita gari la mbele bila ya kuchukua tahadhari na matokeo yake ni ajali.

Ukimuuliza ana majibu yasiyo na mashiko, kwamba hajaanza leo kuendesha gari akiongea na simu au akichati!

Tunaambiwa kwa mfano tuachane na mazoea ya kuchoma moto misitu au kukata miti ovyo, kwani yanagharama kwa maisha yetu, hatusikii.

Takwimu za uhifadhi wa mazingira zinaonyesha kuwa Tanzania hupoteza takribani hekta 400,000 za misitu kila mwaka kutokana na miti kukatwa kwa sababu ya mazoea.

Matokeo yake ni mabadiliko ya tabianchi ambayo ndiyo chanzo cha mafuriko na ukame tunaoushuhudia katika baadhi ya maeneo nchini.

Tunaambiwa na wataalamu wa afya tuweke mazingira yetu katika hali ya usafi ili kuepukana na magonjwa kama ya kuharisha na kipindupindu.

Hata hivyo, kutokana na mazoea ndio haohao tunaofungulia maji ya chooni na kuyaelekeza kwenye mitaro ya maji na hatimaye magonjwa ya kuambukiza.

Ni wakati sasa kwa Watanzania wa kuachana na utamaduni wa kufanya kazi kwa mazoea, ili kuliepusha taifa na majanga ambayo kimsingi yanaepukika.

## BARUA & MJADALA

# Tabia hii iachwe kwani inakera

***Mhariri***
***Habari za majukumu!***

*KIMSINGI nimejitokeza leo katika ukurasa huu wa barua kwa Mhariri unaotupatia fursa sisi wasomaji ya kuelezea changamoto na kero mbalimbali zinazotukabili, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu mbele.*

*Lakini ukurasa huu hautoi fursa tu ya kuwasilisha changamoto na kero zinazotukabili, bali pia kupongeza inapobidi kwa kazi nzuri inayokuwa imefanyika katika maeneo yetu na hasa kama inalenga tija kwa jamii.*

*Mhariri, leo nimeona nijitokeze kuelezea kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo sana niwapo katika mihangaiko yangu ya kutafuta riziki ya kila siku, kwenda na kurudi nyumbani. Nikiwa ni mkazi wa eneo la Mbagala katika jiji hili la Dar es Salaam, mara nyingi usafiri wangu wa kwenda na kurudi kutoka kwenye mihangaiko yangu huwa ni ule wa umma kwa maana ya daladala.*

*Kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo katika usafiri huu na wengine wenye mtazamo kama wangu, si ile ya kujazana kwenye mabasi hayo na hasa kwetu sisi wakazi wa Mbagala kama inavyojulikana na wengi katika jiji hili. Kimsingi ninazungumzia tabia ya baadhi ya wasafiri wenzetu kuweka hadharani mambo yao ya siri ya kifamilia, mitaani ama kimahusiano kupitia mazungumzo ya simu za mkononi tena kwa sauti kubwa kiasi cha kuwa kero kwa wasafiri wenzao.*

*Unakuta mtu anaongea na shoga yake kwa simu kwenye daladala tena kwa sauti kubwa akimueleza namna pengine alivyomchongea jirani yake kwa mumewe au namna alivyomshushua mbele ya mashoga zake.*

*Kibaya zaidi unaweza ukakuta mtu anajadiliana na anayewasiliana naye mambo ya mahusiano ya kimapenzi, namna gani wakutane, saa ngapi na wapi kwa sauti kubwa bila hata ya kujali kama mazungumzo yake na hata sauti yake inakera wengine.*

*Kupitia kwako Mhariri, ninaomba watu wenye tabia hii waelewe kuwa kuna baadhi ya mazungumzo yasiyostahili kuwekwa wazi hadharani katika vyombo vya usafiri wa umma, ambavyo viko pale kwa ajili ya kusafirisha watu na si vinginevyo.*

*Ni muhimu watu hao wakaelewa kwamba ndani ya usafiri wa umma, kila mtu anakuwa na mipango yake kichwani kama anaenda kazini, na anahitaji utulivu kama anarudi kutoka kazini kwa sababu ya uchovu wa siku nzima na changamoto nyingine alizokutana nazo katika mizunguko yake. Hahitaji kusikia kelele za namna mnavyotongozana au jinsi ulivyomchongea jirani yako kwa mumewe au jinsi ulivyomshushua shoga yako mbele ya watu.*

***Deo Lyimo- Mbagala***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Tokomeza zero inapotoa matokeo Kisarawe

**Na Sabato Kasika**

**KISARAWE** imepania kuinua kiwango cha elimu na sasa imekuwa ikiendesha kampeni iliyopewa jina la 'Tokomeza Zero' ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi na kufuta kabisa zero, ambazo miaka ya nyuma zilionekana kuwa nyingi.

Mkuu wa wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo alishazindua kampeni hiyo ikijumuisha wanafunzi kuwekwa katika kambi kwa ajili ya mafunzo maalum, uboreshwaji wa miundombinu shuleni na elimu na kozi kwa walimu.

Walimu wanapata kozi lengo likiwa ni moja tu kuinua kiwango cha elimu wilayani Kisarawe, kwa vile elimu ndio ufunguo wa maisha, ndio maana imeanzishwa kampeni hiyo maalum.

Kwa mujibu wa Mwegelo, wanafunzi wote wa kidato cha nne na cha sita wamekuwa wakipata mafunzo ya ziada ili kujiandaa na mitihani yao ya taifa, na pia kuwaepusha na kazi za kila mara.

Wanafunzi hawa huwekwa kambini kwa muda wa miezi miwili kabla ya mitihani yao ya taifa.

Walimu nao wamekuwa wakipewa mahitaji yote muhimu ili kufanikisha kazi ya ufundishaji na pia kuboresha miundombinu ya shule ili kuweza kukidhi mahitaji ya wanafunzi na walimu.

Anasema elimu itaendelea kuwa kipaumbele ndani na nje ya darasa na kwamba wataendelea kutenga bajeti kubwa kutoka vyanzo vya ndani ya halmashauri na kushirikisha wadau katika kuboresha elimu, kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanafunzi.

**Mtoto wa kike, ambaye atahitajika kufanya usafi nyumbani kisha aende shule kwa kutembea huchoka zaidi, miundombinu ya shule ni changamoto na hata idadi za shule wilayani ni chache...**

Hayo ni baadhi ya mambo muhimu, ambayo yamekuwa yakifanywa wilayani Kisarawe ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi na kutokomeza sifuri, kwani kumsaidia mtoto kupata elimu ni jambo la msingi.

Mkuu wa wilaya anasema utafiti unaonyesha wanafunzi wengi wa Kisarawe hutembea umbali mrefu kwenda shule, kama kilometa tano kwenda pekee, hali inayowafanya kufika shuleni wakiwa wamechoka.

"Mtoto wa kike, ambaye atahitajika kufanya usafi nyumbani kisha aende shule kwa kutembea huchoka zaidi, miundombinu ya shule ni changamoto na hata idadi za shule wilayani ni chache... kwa kulitambua hilo kuna ushirikishwaji wa wadau wa elimu ili kuwezesha ujenzi wa shule kwa ajili ya wana Kisarawe na mkazo unawekwa zaidi ili kufanikisha kampeni ya Tokomeza Zero," anasema.

Anafafanua kuwa mwaka 2016 ziro zilikuwa ni 457, lakini uliofuata zilipungua na kufikia 259 na kwamba zimeendelea kupungua zaidi ambapo mwaka jana zilikuwa ni 175 na inawezekana zikatokomea kabisa.

"Tumeendelea kutokomeza ziro kwani kidato cha nne ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 70 kwa mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 82.81 kwa mwaka 2018," anasema.

Kimsingi wakati huu ambao nchi inalekea kuwa ya viwanda, kuna haja ya kuzalisha wasomi wengi zaidi na njia nzuri ya kuwapata ni kuiga mfano wa kampeni zilizoanzishwa na wilaya Kisarawe.

Kampeni hizo zimekuwa zikienda sambamba na kuwadhibiti viongozi, watendaji na wazazi wanaowaficha wanafunzi wanaopewa ujauzito na kukatisha masomo ili kufanikisha kutokomeza sifuri.

Elimu inahusu watoto wa kike na wa kiume, hivyo wote wanatakiwa kuondolewa vikwazo ili waweze kuwa na mchango kwenye Tanzania ya viwanda.

Katika ulimwengu wa leo, elimu inazidi kutambulika na inatazamwa kama ndilo tumaini la kipekee kiuchumi na kimaendeleo kwa sasa na siku zijazo, hivyo ni muhimu itiliwe mkazo.

Ikumbukwe kuwa elimu ina manufaa kwa mtu mmoja mmoja anayeipata na hata kwenye jamii anayotoka, kwa hiyo kuna uwezekano mkubwa kwamba anapoelimika mtu mmoja hata taifa nalo linanufaika.

Wilaya ya Kisarawe imeamua kuwekeza kwenye elimu na ndio maana imewapa onyo viongozi, watendaji na wazazi watakawaoficha 'mafataki', itachukua hatua za kisheria. Watu hao wakidhibitiwa itakuwa ni rahisi zaidi kutokomeza sifuri, ambayo huenda wanahusika kwa kiasi kikubwa kukwamisha maendeleo ya watoto wa kike wilayani humo.

Mbinu hizo kama zikiigwa maeneo yote nchini, mimba na sifuri vitakuwa historia shuleni, badala yake watoto watasoma na hatimaye wataweza kutimiza ndoto zao za baadaye walizojiwekea.

Hii inatokana na ukweli kwamba siyo rahisi kutimiza ndoto ya kushika nafasi ya uongozi wa nchi au utaalam wowote bila kuwa na elimu, hivyo watoto wa kiume na kike waachwe wasome.

## KABWELA

**Na Fadhili Mohammed**



# Hoja sita kutikisa Bunge

INATOKA UK. 3

Nyingine ni taarifa ya ukaguzi ya CAG kwa mwaka wa fedha 2018/19, kuzuiliwa kwa mshahara wa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, hoja ya wabunge wa upinzani kuhusu mahabusu wanaokaa muda mrefu gerezani.

### VIPAUMBELE VYA 2019/20

Katika bajeti ya 2019/20 serikali inatarajiwa kukusanya na kutumia Sh. trilioni 33.10, huku Sh.trilioni 20.85 zikitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwamo gharama za uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019 na Uchaguzi Mkuu 2020.

Kwa mujibu wa mapendekezo ya serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na kiwango cha ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20, yaliyowasilishwa hivi karibuni na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, Sh.bilioni 33,105.4 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika, ambapo mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Sh. bilioni 23,045.3.

Mikopo ya ndani inakadiriwa kuwa Sh. bilioni 4,960.0, mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara Sh.bilioni 2,316.4 na misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo Sh. bilioni 2,783.7. Aidha, Waziri Mpango alisema mapendekezo hayo yanatekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2016/17-2020/21.

Alitaja vipaumbele hivyo ni viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda ambapo miradi itakayotekelezwa katika eneo hilo ni ile yenye lengo la kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana nchini hususan kilimo, madini na gesi asilia.

"Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kuchakata gesi asilia, uanzishwaji na uendelezaji wa kanda maalum za kiuchumi na viwanda, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, kuongeza thamani ya madini na usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu," alisema.

Kipaumbele kingine ni kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, ambapo miradi itakayotekelezwa katika eneo hilo ni ile yenye lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, elimu na ujuzi, upatikanaji wa chakula na lishe bora na huduma za majisafi na salama.

Aidha, alisema kipaumbele kingine ni uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji, ambapo miradi itakayotekelezwa katika eneo hilo ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu ambayo ni reli, bandari, nishati, viwanja vya ndege na barabara.

"Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kufua umeme wa maji Rufiji MW 2,115, kuboresha Shirika la Ndege Tanzania, ujenzi wa reli ya kati na kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara na Uwekezaji," alisema.

Aidha, alisema mpango huo umewekwa msukumo katika kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza ikiwamo kupitia upya mfumo wa kitaasisi, kisera na kisheria pamoja na kanuni zake ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo.

Kipaumbele cha tano ni kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango, ambapo alisema miradi itakayotekelezwa inalenga kuimarisha mifumo na taasisi za utekelezaji wa mpango, kuweka mfumo utakaowezesha upatikanaji wa uhakika wa rasilimali fedha na kuweka vigezo vya upimaji wa mafanikio ya utekelezaji.

### HATIMA PROF.ASSAD, MDEE

Baada ya Kamati ya Bunge ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge kukamilisha kumhoji CAG na Mdee kufuatia kauli ya kuliita bunge dhaifu na kuikabidhi taarifa kwa Spika, katika mkutano huo kama Spika ataridhia kuwasilishwa taarifa ya kuhojiwa kwao bungeni, hatima yao itajulikana.

### BAJETI ZA WIZARA

Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kifungu 99(1) kinasema katika Mkutano wa Bunge wa Bajeti utakaonza mapema mwezi Aprili kwa kila mwaka, jumla ya siku zisizozidi hamsini na nane zitatengwa kwa ajili ya Bunge kujadili utekelezaji wa wizara zote wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha, pamoja na makadirio ya matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Pia Kifungu cha 99(2) kinasema Mjadala katika Bunge la Bajeti kwa kila mwaka utaanza na Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, na kufuatiwa na hotuba za bajeti za wizara nyingine zote, kwa utaratibu utakaopangwa na Spika, baada ya kushauriana na Kamati ya Uongozi.

### TAARIFA ZA CAG

Aidha, wiki la pili baada ya kuanza Bunge la Bajeti, CAG huwasilisha ripoti yake ya ukaguzi bungeni na hatimaye kuwa wazi kwa umma.

### MSHAHARA WA LISSU

Hivi karibuni Lissu alisema kuwa Bunge limemsitishia mshahara wake jambo ambalo lilizua mjadala.

# JPM ataka TRA itoze watu kodi

INATOKA UK. 2

kwa kusubiri mivutano ya kesi.

Alimpongeza Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, kwa ufuatiliaji mzuri wa fedha za bajeti zinazoelekezwa katika miradi mbalimbali na kuchukua hatua zinazostahili ikiwamo kuzirejesha hazina na kuzielekeza mahali pengine zinapohitajika.

Aidha, Rais Magufuli alimtaka Naibu Katibu Mkuu wa Fedha na Mipango, na Naibu Kamishna Mkuu wa TRA, Mbibo kwenda kurekebisha dosari zote zilizopo katika ofisi zao ikiwa ni pamoja na kuwaondoa watumishi wanaoonekana kuwa kikwazo cha kutekeleza mipango ya serikali.

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan alisema viongozi hao wanatarajiwa kufanya vizuri zaidi katika nafasi walizopewa hivi sasa hasa ikizingatiwa kuwa wanakwenda kufanya kazi katika ofisi zenye mchango mkubwa katika uchumi wa nchi.

Naye Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Kijaji na Kamishna Mkuu wa TRA, Charles Kichere, walimshukuru Rais Magufuli kwa uteuzi wa viongozi hao na wameahidi kwenda kusimamia kwa ukaribu zaidi utekelezaji wa fedha za bajeti na kufanyia kazi changamoto ya kupanua uwigo wa kodi na kuongeza idadi ya walipa kodi.

Wakati huo huo, Rais Magufuli akiwa na mke wake Janeth Magufuli wametoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu Tryphosa Simon Sanga, ambaye ni dada wa Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa na kutoa pole kwa familia ya mbunge huyo aliyefariki dunia Machi 30, 2019 kwa ajali ya gari jijini Dar es Salaam.

# Meneja wa benki aeleza

INATOKA UK. 3

Kaburu, wote kwa pamoja walighushi fomu ya kuhamisha fedha ya tarehe hiyo wakionyesha kwamba Klabu ya Simba inalipa deni la Dola za Marekani 300,000 kwa Rais wake Aveva.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa kuwa Machi 15, mwaka 2016 katika benki ya CRDB tawi la Azikiwe lililopo Ilala, jijini Dar es Salaam, Aveva aliwasilisha fomu ya kuhamisha fedha zilizoghushiwa ya terehe hiyo akinyesha kwamba Klabu ya Simba imeomba kuhamisha Dola za Marekani 300,000 huku akijua sio kweli.

Katika shtaka la tano, ilidaiwa kuwa kati ya Machi 10, 2016 jijini Dar es Salaam, Aveva alijilipa na kutakatisha Dola za Marekani 187,817 kutoka benki ya Barclays tawi la Uhio, huku akijua zimetokana na kughushi.

Kimaro alidai katika shtaka la sita, kati ya Machi 10 na 16, 2016 Kaburu alitakatisha fedha baada ya mshtakiwa huyo wa pili kumsaidia Aveva kupata Dola za Marekani 187,817.

Katika shtaka la saba, kati ya Machi 10 na Mei 30, 2016, jijini Dar es Salaam, Aveva, Kaburu na Poppe walighushi hati ya malipo wakidai wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577, huku wakijua si kweli.

Ilidaiwa katika shtaka la nane kuwa kati ya Machi 10 na Mei 30, 2016 kwa makusudi alionyesha nyaraka za kughushi kwa Levison Kasulwa akionyesha kuwa klabu hiyo imenunua nyasi bandia kutoka Kampuni ya Nina Guangzhou Trading Limited huku akijua si kweli.

# Mashirika 65 yamjia juu Msajili Vyama vya Siasa

INATOKA UK. 2

Alisema wanaitafsiri hali hiyo kuwa ni mwanzo wa kubomoa umoja wa kitaifa na kupoteza amani ya nchi na kwamba iko mifano kadhaa inayoakisi hali duni ya sasa ya demokrasia nchini.

Aidha, alidai kutungwa kwa sheria kandamizi ya vyama vya siasa nchini ambayo asasi mbalimbali ziliipinga tangu mwanzo kwa kwa kuwa inakiuka katiba na haki za kisiasa kwa kiwango kikubwa.

"Sheria hii imekuja kumpa mamlaka makubwa Msajili wa Vyama vya Siasa na kumfanya awe ni nyapara wa vyama vya siasa badala ya kuwa mlezi. Kwa sheria hii msajili anaweza kufuta chama chochote wakati wowote huku yeye akilindwa na sheria kwa maamuzi atakayoyatoa," alisema.

"Msajili kama mlezi wa vyama anapaswa kutokuwa sehemu ya migogoro ya ndani ya vyama," alisema Olengurumo.

Alisema barua ya Msajili wa Vyama vya Siasa yenye kumbukumbu namba HA.322/362/2D/98 ya nia ya kufuta usajili wa kudumu wa chama cha ACT- Wazalendo imeleta mkanganyiko miongoni mwa Watanzania.

Aidha, alisema mikutano ya vyama vya upinzani imekuwa ikivamiwa na kuzuiliwa na vyombo vya dola, ingawa katiba inatoa haki kwa vyama hivyo kufanya shughuli za kisiasa kama mikutano.

Alisema vyombo vya usalama hasa Jeshi la Polisi vilipaswa kuwa sehemu ya ulinzi na usimamizi wa usalama wakati wa shughuli za kisiasa, lakini wamekuwa wakikandamiza vyama vya upinzani.

Olengurumo alisema viongozi wa dini, Bunge, asasi, Baraza la Vyama vya Siasa nchini, wanazuoni, Kituo cha Demokrasia nchini kuendelea kufumbia macho mwenendo wa demokrasia nchini ni tishio jingine kwa amani na umoja wa kitaifa.

Aidha, alisema kitendo cha kuzuia maandamano huku chana kingine kikionekana wazi wazi kufanya mikutano na maandamano huko ni kuwagawa Watanzania na kufanya wengine hawana haki.

"Hofu yetu ni kwamba hali hii ikiendelea tutalijenga taifa lenye kundi kubwa la watu wanaohisi wametengwa na kubaguliwa katika taifa lao," alisema.

Olengurumo alitoa ushauri kwa serikali ihakikishe uhuru wa kujumuika ikiwa ni pamoja na uhuru wa kufanya maandamano ya amani una heshimiwa na kulindwa na vyombo vya usalama kama sheria za nchi zinavyoelekeza.

## HABARI KITAIFA

# Ongezeko watu latishia Hifadhi ya Serengeti, Maasai Mara

**Novatus Makunga,** ARUSHA

JOPO la wanasayansi wa kimataifa linaloundwa na taasisi 11 limeeleza kuwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Hifadhi ya Maasai Mara nchini Kenya zipo hatarini kutoweka kutokana na ongezeko la watu kwa zaidi ya asilimia 400 katika kipindi cha muongo mmoja uliopita.

Wanasayansi hao kupitia mradi unaofahamika kama African Bioservices wakigawanyika katika makundi 13 ukihusisha pia taasisi za utafiti za Tanzania na Kenya, walitoa taarifa ya utafiti wao wa kisayansi katika mkutano na waandishi wa habari jijini hapa.

Katika mkutano huo ambao uliokuwa na wawakilishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (Tawiri), Mtafiti Msimamizi wa mradi huo, Prof. Han Olff, alisema licha ya matokeo ya sasa, pia wametumia matokeo ya utafiti mbalimbali wa kipindi miaka zaidi ya 40 katika ikolojia ya Serengeti-Mara.

**Baadhi ya maeneo kuna ongezeko la watu kwa zaidi ya asilimia 400 katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, huku idadi ya wanyamapori wakipungua kwa asilimia 75 hususani upande wa Kenya.**

Alisema kati ya mwaka 1999 na 2012 kulikuwa na ongezeko la wastani wa asilimia 2.4 la watu kila mwaka.

Aidha, mwanasayansi huyo alisema shughuli za kilimo ziliongezeka kutoka asilimia 37 mwaka 1984 na kufikia asilimia 54 mwaka 2018, huku idadi ya ng'ombe wakiongezeka hasa katika maeneo ya unyevunyevu kandokando ya Ziwa Victoria kwa wastani wa asilimia 4.2 kwa mwaka.

Prof. Olff alieleza pia kumekuwa na ongezeko la mbuzi na kondoo katika ikolojia hiyo ya Serengeti-Mara kwa wastani wa asilimia 38 kwa mwaka.

"Baadhi ya maeneo kuna ongezeko la watu kwa zaidi ya asilimia 400 katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, huku idadi ya wanyamapori wakipungua kwa asilimia 75 hususani upande wa Kenya," alifafanua.

Alisema hivi sasa kuna ugomvi mkubwa wa kugombea nyasi kati ya wanyamapori na mifugo hususani ng'ombe na akashauri serikali za nchi za Tanzania na Kenya kutafuta suluhisho la tatizo hilo.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti cha Serengeti ambacho kipo chini ya Tawiri, Dk. Robert Fyumagwa, alisema ni jukumu la nchi za Kenya na Tanzania kulinda Ikolojia ya Serengeti-Mara.

Alisema hivi sasa upande wa Kenya maeneo ambayo yalikuwa ushoroba wa wanyamapori yamevamiwa na kuchukuliwa kwa shughuli za kibinadamu, ambapo wamiliki wameamua kuzungushia uzio huku wakichimba mabwawa makubwa ya maji, hivyo kuathiri baionuwai ya ikolojia.

Dk. Fyumagwa alisema Mto Mara ambao ulikuwa unategemewa na wanyama umekauka na sasa tegemeo kubwa ni Mto Grumet pamoja na eneo la Magharibi ya Hifadhi ya Serengeti kwenye pori tengefu la Speke Gulf kwa kuwanusuru wanyama wanaohama.

Mkuu wa kitengo cha habari na Mawasiliano katika Wizara ya Maliasili na Utalii, Doreen Makaya, alisema taarifa hiyo ya utafiti imekuja wakati serikali ilishaunda kamati inayopitia vijiji vyote vilivyoko katika maeneo ya hifadhi.

Alisema kamati hiyo imeundwa kufuatia agizo la Rais John Magufuli kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, ambapo aliiagiza iangalie kama kuna maeneo ambayo yalikuwa hifadhi ya wanyamapori lakini kwa sasa hayatumiki wabadilishe sheria, wayamegee na kurasimisha kwa wakulima na wafugaji.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Habari na Elimu wa Tawiri, Dk. Janemary Ntalwila, alisema matokeo ya utafiti huo yamekuja wakati mwafaka, ambapo serikali ya Tanzania inachukuwa hatua muhimu za kutatua kitaifa changamoto katika maeneo ya hifadhi.

"Utafiti huu unatupa matokeo ya kisayansi ya tatizo la kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika ikolojia ya Serengeti-Mara na kwamba ni taarifa muhimu sana inayohitajika sasa na watunga sera na wanasiasa," alisema.

Ikolojia ya Serengeti-Mara yenye eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 40,000 ikitajwa kuwa miongoni mwa maeneo makubwa zaidi ya hifadhi duniani ikihusisha Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Maasai Mara kwa kila mwaka huwa na tukio la nyumbu zaidi ya milioni moja, swala zaidi ya laki tano na pundamilia zaidi ya laki mbili kuhama kutoka katika hifadhi moja hadi nyingine.

## Masasi waombwa mapokezi ya JPM

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WAKAZI wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wameombwa kujitokeza kwa wingi katika mapokezi ya Rais John Pombe Magufuli ambaye anafanya ziara ya kikazi mkoani hapa, kwa ajili ya kuona shughuli mbalimbali za maendeleo.

Miongoni mwa shughuli atakazozifanya Rais Magufuli ni kuweka jiwe la msingi katika Kituo cha Afya cha Mbonde kilichopo katika Kata ya Mbonde Halmashauri ya Mji Masasi.

Wito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ziara hiyo ya Rais Magufuli anayoifanya wilayani hapa Aprili kesho.

Aliwataka wananchi wote wa Masasi bila kujali itikadi ya vyama vya kisiasa kujitokeza kwa wingi katika mapokezi hayo.

Alisema baada ya kuwasili Masasi ataelekea katika Kijiji cha Mbonde kilichopo Kata ya Mbonde kwenye Halmashauri ya Mji wa Masasi kwa ajili ya kufungua ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mbonde.

Mzee alisema ni fursa pekee kwa wananchi wa Wilaya ya Masasi kutembelewa na Rais Magufuli, hivyo waonyeshe hamasa kubwa ya kumpokea na kumkaribisha Masasi.

"Nawaomba wananchi wote wa wilaya ya Masasi kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kumpokea Rais Magufuli," alisema Mzee.




Magari yakipita kwenye njia ya mchepuko upande wa kulia kupisha ujenzi wa daraja kubwa katika eneo la Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam jana. Hiyo ni awamu ya kwanza ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha mkoani Pwani yenye urefu wa kilomita 19. **PICHA: JOHN BADI**

## Katavi kupata umeme wa gridi mwakani

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

WAKAZI wa Mkoa wa Katavi wataanza kutumia umeme wa gridi ya taifa mwakani, hivyo kuwawezesha kupata nishati hiyo kwa uhakika.

Neema hiyo watakayoipata kuanzia Juni, itawaondoa katika adha ya kutumia umeme wa jenereta ambao si wa uhakika, na unaigharimu serikali fedha nyingi.

Waziri wa Nishati, Dk. Medadi Kalemani, ndiye aliyetangaza neema hiyo jana wakati akihutubia wananchi wa wilaya za Mpanda na Tanganyika, alipokuwa akizindua kuwasha umeme wa REA Awamu ya Tatu katika vijiji vya Mchakamchaka na Ifukutwa katika Wilaya ya Tanganyika na kijiji cha Kapalala wilayani Mpanda.

Alisema ili mkoa huo uwe na umeme wa uhakika, serikali imeanzisha mradi wa kupeleka umeme mkubwa mkoani Katavi wa gridi ya taifa kutoka mkoani Tabora hadi mkoani Katavi, hatua ambayo itaufanya mkoa huo kuwa na umeme wa uhakika.

Dk. Kalemani alisema lengo la serikali ni kuangalia namna mkoa wa Katavi utakavyopata umeme na kuwa na umeme wa uhakika wa gridi ya taifa kama ilivyo kwa mikoa mingine nchini.

Aliwataka wakazi wa mkoa huo kuhakikisha wanatumia fursa hiyo ya kutumia umeme huo utakapokuwa umefika kwa kuanzisha viwanda kwa kuwa watakuwa na umeme wa uhakika.

Alisema serikali imepanga kufikisha umeme kwenye vijiji 177 vya Mkoa wa Katavi na kwenye vitongoji vyake vyote na taasisi mbalimbali bila kuruka eneo lolote lile ili kila mwananchi apate umeme wa uhakika.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Amos Makalla, alisema mkoa huo ulikuwa unatumia megawati 2.5 za umeme, lakini baada ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kuongeza jenereta, mkoa una umeme wa megawati 3.7, hivyo wanao umeme wa ziada.

Makalla alisema kuwa Mkoa wa Katavi umeshindwa kutimiza azima ya kuwa na viwanda kutokana na kutokuwa na umeme wa uhakika, lakini baada ya kufikiwa na umeme wa gridi ya taifa mwakani, azima ya kuwa na viwanda itatimia.

# Waathirika wa wanyamapori wafidiwa

**Na Beatrice Shayo,** aliyekuwa RUFIJI

WATU 15 wamelipwa fidia ya Sh milioni 11.6 baada ya kujeruhiwa na wengine kuuawa na wanyamapori katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani.

**Kuanzia 2005 hadi 2008 zaidi ya watu 48 wameathiriwa na wanyamapori ikiwamo kusababishiwa vifo na majeruhi wilayani Rufiji.**

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano, Mhifadhi wa Wanyapori Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Robert Kiondo, alisema fidia hiyo ni kwa matukio ambayo yametokea kuanzia mwaka 2016 hadi 2018.

Alisema serikali imefanya jitihada mbalimbali katika kuzuia matukio kwa wanyama pamoja na hasira za wananchi dhidi ya wanyamapori.

Alisema serikali imeona ni vyema kutoa kifuta machozi kwa mwananchi yeyote ambaye amepata madhara kutoka kwa wanyamapori.

"Sio kwamba inaondoa lile tatizo, lakini angalau inasaidia kufuta machozi, hivyo wiki mbili zilizopita serikali ya Rais John Magufuli imewawezesha kutoa kifuta machozi kwa ndugu wa mtu aliyefiwa ambapo aliyeuwawa na mnyama ndugu amelipwa Sh. milioni moja na yule aliyejeruhiuliwa amepatiwa Sh. 200,000,kama kifuta machozi (ubani)," alisema.

Kiondo alisema wamefanikiwa kulipa watu 15 katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, lengo ni kuwahamasisha wananchi waone kuwa serikali yao inawajali licha yakupata madhara yanayosababishwa na wanyamapori kwenye maeneo yao.

"Ninamshukuru Rais Magufuli kwa kuwa jambo hili ni nzuri na hata sisi wahifadhi inakuwa rahisi wananchi kutuelewa hasa lengo la serikali ni nini maana kama huwalipi kifuta machozi wanaona wanyama ndio wanaopendwa kuliko watu, kumbe serikali inajali wananchi wake pamoja na wanyamapori," alisema.

Aidha, alisema serikali inafanya jitihada mbalimbali katika kuhakikisha matukio ya wanyama kwa binadamu yanadhibitiwa kwa kushirikiana na wananchi wenyewe ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea.

Alisema kuanzia 2005 hadi 2008 zaidi ya watu 48 wameathiriwa na wanyamapori ikiwamo kusababishiwa vifo na majeruhi wilayani Rufiji.

"Wilaya inafanya jitihada kudhibiti matukio haya kwa kutoa elimu kwa wananchi pamoja na kudhibibiti matukio ya wanyama wakali kabla yakuleta madhara," alisema.

Alisema ili mwananchi kulipwa fidia, ni lazima taarifa za tukio zitolewe kupitia watendaji wa vijiji husika na baadae kupelekwa wilayani ambapo fomu maalumu ya kifutamachozi itajazwa nakuwasilishwa wizarani kwa hatua zaidi.

Aidha, alisema wananchi wanatakiwa kutoa taarifa pale wanapopata matukio hayo kwa wakati kwa kushirikiana na watendaji wa vijiji ili wazipate na kulipwa kifuta machozi. Kiondo alisema bado kuna haja ya kutoa elimu kwa wananchi ili wasiwe wanaingia hifadhini kinyemela.

Alisema wapo ambao hukutana na madhara ikiwamo kushambuliwa na wanyama wakali kama simba, tembo na chui, huku wananchi wengine wakiweka hisia tofauti dhidi ya wahifadhi.



Meneja wa Vodacom Tanzania (PLC), mkoani Mtwara, Charles Minungu (kushoto), akiwa na Meneja wa Vodashop Mtwara, Frank Daud, wakimkabidhi mfano wa hundi ya shilingi 500,000/- mmoja wa washiriki wa kampeni ya Vodacom M-Pesa Tuzo Points, Eladius Rutha mkazi wa Naliendele, katika hafla iliyofanyika Mtwara mwishoni mwa wiki. Kupitia kampeni hii wateja 140 wa Vodacom walizawadiwa shilingi 25,000/- kila mmoja na baada ya kampeni kumalizika wateja 10 wa Vodacom nchi nzima watazawadiwa shilingi 500,000/- kila mmoja. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara wakarabati sokoni

**Na Ibrahim Yassin,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wa soko la Uhindini (Sokoine) katika Manispaa ya Mbeya, wamekarabati barabara ya soko hilo,kutokana na msaada wa Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson.

Naibu Spika huyo alitembelea soko hilo na kukabidhi shilingi milioni moja, baada ya kupokea ombi la wafanyabiashara hao.

Awali wafanyabiashra hao baada ya kuona barabara za kuingia na kutoka katika soko hilo ni mbovu, waliamua kujipanga kutafuta namna ya kuikarabati badala ya kusubiri serikali ifanye, huku wakiomba kusaidiwa na Naibu Spika.

Akizungumza jana na gazeti mwenyekiti wa soko hilo,Joseph Mwakitalima alisema kamati ya soko iliketi na kuamua kuikarabati barabara hizo ambapo pia waliandika barua kuomba msaada kwa Naibu spika ambaye tayari amekabidhi milioni moja.

Alisema wateja wanaoingia katika soko hilo wamekuwa wakipata shida hasa wakati wa mvua za masika barabara zinazotoka na kuingia hazipitiki ambapo mbali na changamoto hiyo, waliiomba serikali kwa maandishi kutaka kujenga barabara hiyo, lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea.

"Tumeomba mara nyingi serikalini tukarabatiwe barabara ya soko hili, lakini maombi yetu hayakutekelezwa, hivyo kitendo cha Naibu Spika kutupatia pesa kwa ajili ya barabara na sasa tayari ukarabati umefanyika," alisema.

Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacquelline Boaz, alipotembelea wafanyabiashara hao,aliwapongeza kwa kuzitendea haki pesa walizopewa na kusema taasisi hiyo itaendelea kusaidia jamii katika utatuzi wa kero mbalimbali pindi watakapohitajika.

Awali, wafanyabiashara hao pia walimuomba Naibu Spika kutatua changamoto ya nyaya za umeme mkubwa wa Tanesco iliyopo katika soko hilo, ombi ambalo lilikubaliwa na na Meneja wa Taasisi hiyo, akisema atawasiliana na Dk,Tulia ili changamoto hiyo itatuliwe.

# TFS yahimiza upandaji miti

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), umeiomba jamii kuwekeza nguzu zaidi katika upandaji miti ili kupambana na tishio la kupotea mvua na mabadiliko ya tabianchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kaimu Mtendaji Mkuu wa TFS, Zawadi Mbwambo, katika kilele cha kupanda miti kitaifa katika eneo la Kilongawima, Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Mbwambo alisema bado ipo changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira hususan katika vyanzo vya maji ambayo inachangia kwa kiwango kikubwa kupotea mvua na mabadiliko ya tabianchi.

"Mnafahamu changamoto kubwa iliyopo katika uharibifu wa mazingira, siyo kwa mikoani tu hata katika Jiji la Dar es Salaam, tunashuhudia uharibifu mkubwa wa mazingira ambao unasababisha mvua kupotea, na sasa imefikia mahali viongozi wa dini kwenda misikitini na makanisani kuomba mvua, haya yote yanasababishwa na uharibufu wa mazingira," alisema Mbwambo.

Aliongeza: "Mvua imepotea si kwa sababu nyingine, isipokuwa binadamu tunaharibu mazingira mpaka sasa inachangia mfumo wa mvua kubadilika na mabadiliko ya tabianchi na hiyo yote ni kwa sababu ya uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu."

Alisema ni muhimu Watanzania wakabadilika na kuacha tabia ya kuharibu mazingira na kujenga tabia ya kupanda miti katika maeneo mbalimbali yanayowazunguka ikiwa ni katika mazingira ya nyumbani, shambani na katika maeneo mengineyo.

Meneja Misitu Wilaya ya Kinondoni na Ubungo, Doto Ntumbikwa, alisema upandaji na utunzaji wa miti au misitu bila ushirikiano na wananchi hususani wanayoizunguka hakuwezi kuleta mafanikio makubwa katika kupambana na uharibifu wake.

# Wamwangukia waziri tozo kuingiza pembejeo

Na Mwandishi Wetu, ARUSHA

CHAMA cha Wakulima wa Tanganyika, (TFA), kimemwangukia Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, kikimlalamikia utozaji wa tozo ya kuingiza pembejeo na viuatilifu kwa kutumia dola za Marekani badala ya shilingi.

Mwenyekiti wa chama hicho, Peter Sirikwa, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati aliposoma risala ya chama kabla ya Waziri Hasunga kufungua mkutano mkuu wa mwaka wa wanachama jijini hapa.

**Iwapo itatozwa kwa fedha ya shilingi itafanya bei ya pembejeo kutobadilika badilika.**

"Utozaji wa tozo kwa bei ya dola za Marekani bandarini unasababisha pembejeo na viuatilifu kuwa ghali sana.

"Iwapo itatozwa kwa fedha ya shilingi itafanya bei ya pembejeo kutobadilika badilika," alieleza.

Katika hatua nyingine, Sirikwa, alimwomba Waziri Hasunga kuwapatia maeneo ya kulima ili chama hicho kijitike katika kilimo cha kisasa na darasa kwa wakulima.

"Tunaomba kupata mashamba yatakayotumika kama mashamba darasa," alisema na kupendekeza mashamba toka mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Songwe na Mbeya.

Akijibu Waziri Hasunga alisema, serikali kwa kushirikiana na wadau imejizatiti kuwekeza katika viwanda vya pembejeo na viuatilifu.

Alikitaka chama hicho nacho kuweka malengo ya kuanzisha viwanda vya aina hiyo, hatua ambayo itafanya pembejeo na viuatilifu kuwa vya gharama nafuu.

Alisema wanataka kuona mbolea yote inazalishwa hapa hapa nchini.

# Pinda achekelea kuvuna wanachama wapya CCM

Na Mwandishi Wetu, SIMANJIRO

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameendelea kuzoa wanachama wa Chadema wilayani Simanjiro baada ya watu 208 kujiunga na CCM, mwishoni mwa wiki iliyopita.

Wanachama waliojiunga na CCM, wametokea Kijiji cha Lerumo, Kata ya Ruvu Remit, ambapo ilikuwa ngome kubwa ya Chadema.

Katibu wa CCM Wilaya ya Simanjiro, Ally Kidunda, alisema wanachama hao wamerudisha kadi hizo ili kumuunga mkono Rais John Magufuli, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, James ole Millya na diwani wa kata hiyo Lomayan ole Ranga.

Alisema wanachama hao wameondoka Chadema na kujiunga na CCM baada ya kuona utendaji wa kazi nzuri inayofanywa na viongozi wa chama hicho.

"Baada ya Pinda mlezi wetu wa CCM Mkoa wa Manyara kuwapa kadi wanachama hao akiwamo aliyekuwa Katibu wa Chadema wilayani Simanjiro, Frank Oleleshwa, wananchi wa Lerumo nao wameamua kutuunga mkono," alisema.

Alisema hivi sasa wanaendelea na kazi ya kupokea wanachama wapya wa CCM kutoka vyama vya upinzani, wakijiandaa ipasavyo na uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

"Pamoja na hayo hivi sasa nguvu kubwa ya uandikaji kadi kwa njia ya kielektroniki katika maeneo ya Bwawa la Nyumba ya Mungu kwani bado Simanjiro tunaongoza mkoani Manyara kwa kusajili wanachama wengi," alisema.

Mmoja wa wanachama wa CCM wa kijiji hicho, Issaya Leshule, alisema dhana ya CCM ni salama kwenye eneo la Lerumo haikuwa sahihi kutokana na wingi wa wanachama hao wa Chadema.

"Kwa kweli katibu wetu Kidunda amefanya kazi kubwa kwani kuwarudisha wanachama 208 siyo jambo dogo kwa kweli," alisema.



Katibu wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (Marema), tawi la Mirerani, Dk. Curtius Msosa, akielezea uteuzi wake juzi wa kuwapo kwenye chombo cha juu kinachosimamia mradi wa kupambana na TB na Silikosis yanayotokana na uchimbaji madini kwa nchi za SADC. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC Chaula 'awapiga mkwara' wamiliki wa migodi

Na Mwandishi Wetu, SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, amewaagiza wamiliki wa migodi ya tanzanite kuwasilisha ofisini kwake majina ya wafanyakazi na vibarua ili kuepusha kuwatelekeza hospitalini wanapougua au kufariki dunia.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki, kufuatia kutelekezwa kwa mwana apolo mmoja katika Hospitali ya Kibong'oto, wilayani Siha, alikokuwa akipata matibabu ya ugonjwa wa kifua kikuu.

Alisema ili kuepuka tukio kama hilo lisijitokeze tena ameagiza wamiliki wote wa migodi ya tanzanite kufikisha ofisini kwao majina yote ya wafanyakazi wao.

"Wamiliki watupe orodha ya mikataba ya wafanyakazi wao wote ili lolote likitokea wapate sehemu ya kuanzia kuliko hivi sasa wanakuwa na wakati mgumu," alisema.

Hata hivyo, Mratibu wa Shirika lisilo la kiserikali la Mapambano ya Kifua Kikuu na Ukimwi Tanzania (Mkuta), Thobias Magati, alithibitisha tukio hilo.

Magati alimtaja mwana apolo huyo ambaye hadi sasa mwili wake upo Kibong'oto kuwa ni Amos William Mnyanyeri.

Alisema alimpeleka Mnyanyeri kutoka mji mdogo wa Mirerani ili akapate vipimo Hospitali ya Kibong'oto, Novemba 15, mwaka jana.

Alisema baada ya kufanyiwa vipimo hospitalini hapo Mnyanyeri alibainika kuwa na kifua kikuu, hivyo akaanza matibabu siku hiyo ila waliruhusiwa kurudi nyumbani. Alisema baada ya muda Mnyanyeri alirudi hospitalini hapo na kulazwa huku akiendelea na matibabu hadi alipofariki dunia.

"Mnyanyeri aliandika kuwa alikuwa anafanya kazi kwenye mgodi wa Edison Mwalemba uliopo kitalu D, lakini mmiliki huyo alisema alishaacha kazi hapo kwake," alisema Magati.

Alisema mmiliki huyo Mwalemba alisema Mnyanyeri aliacha kuchimba madini ya tanzanite kwenye mgodi wake muda mrefu na kuwa mchoma mkaa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara, (Marema), Tawi la Mirerani, Shwaibu Mushi, aliwataka wamiliki wa migodi waliokuwa wakimtumia kijana huyo kwenda kuchukua mwili wake.

Alisema mwana apolo huyo alifariki dunia miezi mitatu iliyopita hospitalini hapo wakati akipatiwa matibabu ya ugonjwa wa kifua kikuu.

Alisema mmiliki wa mgodi aliyempa nauli mwana apolo huyo anafahamika ila amedai yeye alijitolea kibinadamu wala hamfahamu kwa kuwa huwa ana kawaida ya kusaidia wengine.

Alisema hadi hivi sasa imepita miezi mitatu baada ya mwana apolo huyo kufariki dunia hospitalini hapo huku ndugu zake hawajajitokeza.

"Aliyetoa nauli yupo na nimemfuata kuzungumza naye juu ya kwenda kuchukua mwili huo ili azikwe, lakini amedai hamfahamu kwa kuwa alijitolea kama msamaria mwema," alisema.

Alisema hata Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Chaula, amesisitiza mara nyingi wajitokeze kwenda kuchukua mwili huo ili ukazikwe lakini hakuna mmiliki yeyote wa migodi aliyefanya hivyo.

# Askofu Shoo awananga wastaafu wapenda raha

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo, amesema mipango mibaya ya baadhi ya wastaafu kufikiria kujilimbikizia mali wakati wakiwa kazini ili waishi kwa raha mitaani baada ya kustaafu ni tatizo kubwa katika jamii linalohitaji tafakuri.

Dk. Shoo ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini, alikuwa akizungumza na waumini wa dhehebu hilo katika Usharika wa Longuo, wakati wa ibada maalum ya kumsimika Mkuu wa Jimbo la Kilimanjaro Kati, Mch. Javason Mrema na Mkuu wa pili wa jimbo hilo Mch. Israel Moshi.

"Siyo vibaya kuweka mipango yako vizuri kwa ajili ya kustaafu, lakini siyo vizuri pia kuweka pembeni kazi ya Mungu. Watu wanapanga wakistaafu waishi kwa raha, narudia kusema tena mipango mibaya ya kujiwekea akiba kwa wastaafu ni tatizo katika jamii yetu," alisema askofu huyo.

**Kutokana na baadhi ya wastaafu kutoa ovyo fedha hizo, uwekezaji usiokuwa na uzoefu wa kuleta tija iliyokusudiwa kunawafanya kuishi bila matumaini yoyote.**

"Watumishi wa Mungu mnapaswa kutambua kuwa mmeitwa kuhubiri ukweli na siyo utajirisho, wapo watu wanadanganyika na kukutwa na injili ya utajirisho jambo ambalo ni kinyume na kusudio la Mungu."

Kwa kauli ya Dk. Shoo, kuna haja serikali na sekta binafsi kutoa elimu kwa wastaafu kila mara kwa ajili ya maandalizi na mipango mizuri inayohitajika kufanikisha jambo lolote, baada ya kuzikabili changamoto zitakazojitokeza.

Inaelezwa kuwa wastaafu wengi nchini huishi maisha ya dhiki, hasa wanapomaliza mafao waliyolipwa baada ya utumishi wa muda mrefu na ni ukweli usiopingika kuwa wastaafu huingia kwenye matumizi mabovu ya fedha, pindi wanapopata malipo yao ya kustaafu kwa mkupuo.

Kutokana na baadhi ya wastaafu kutoa ovyo fedha hizo, uwekezaji usiokuwa na uzoefu wa kuleta tija iliyokusudiwa kunawafanya kuishi bila matumaini yoyote.

Akitoa itikio la kukubali kushika wadhifa huo, Mkuu wa Jimbo la Kilimanjaro Kati la KKKT, Mchungaji Javason Mrema alisema katika utumishi wake atahakikisha anashirikiana na viongozi wengine wa jamii ikiwamo serikali ili kuwahudumia watu wao.

Awali, Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, Arthur Shoo, akitangaza hati ya uapisho huo, alisema Kanuni ya 18, Kifungu (I) 'C' kinasema jimbo litaongozwa na Mkuu wa Jimbo ambaye stahili zake katika jimbo zitaoteshwa katika sheria.



Mkurugenzi wa Shule za Feza, Ibrahim Yunus (kushoto), akiwakabidhi Bendera ya Taifa washiriki wa shindalo la Hesabu katika mashindano ya Afrika yanayofanyika nchini Afrika ya Kusini, wakati wa hafla ya kuwaaga iliyofanyika, jijini Dar es Salaam jana. Washindi hao, wanne waliodhaminiwa na shule hiyo wametoka katika shule tofauti za hapa nchini. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Vijana 'pasua kichwa' kujiunga katika vikundi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MANISPAA ya Moshi imesema tatizo la vijana kutoshirikiana kupitia vikundi ili waweze kukopesheka limezidi kuwa kubwa hatua ambayo inarudisha nyuma maendeleo yao kwa jamii.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa hiyo, Danford Kamenya, alieleza hayo jana, kabla ya Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, kukabidhi hundi za Sh. milioni 97 kwa vikundi 16 vya wanawake na vikundi vitatu vya vijana katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019.

"Tatizo limekuwa kubwa hasa kwa vijana wa kiume kutokuwa na mwamko wa kufanya kazi katika vikudi, hata hivyo manispaa yetu kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, inaendelea kuhamasisha vijana wa kiume wajiunge kwenye vikundi na kufanya kazi kwa kushirikiana badala ya kutaka kupewa fedha binafsi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba akizungumza kabla ya kukabidhi mikopo hiyo, alitoa wito kwa wanufaika kuhakikisha kuwa fedha wanayopewa inakwenda kutekeleza miradi, biashara walizokusudia na kujenga tabia ya kuzirejesha kwa wakati ili ziweze kunufaisha vikundi vingi zaidi kama inavyotarajiwa.

"Nyinyi leo mnanufaika na mikopo hii isiyo na riba inayotolewa na serikali na mnayo nafasi kubwa ya kujikwamua kiuchumi na kuzisaidia familia zenu pamoja na kuhakikisha kuwa manispaa na wilaya yetu ya Moshi ina kua kiuchumi.

Zaidi aliongeza: "Tunategemea baada ya muda mfupi mtakua kiuchumi na sisi tutahikisha tunawaunganisha na taasisi kubwa za kifedha ili muweze kukopa fedha zaidi."

Awali, Mkuu wa Idara Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii, Rose Minja, alisema zoezi la utoaji wa mikopo hiyo isiyo na riba limezingatia masharti ya utoaji wa mikopo ambapo vikundi vyote ni lazima viombe mikopo kupitia kata husika.

# Uhaba wa maji wakwamisha ujenzi hospitali ya serikali

**Na Paul William,** ROMBO

TATIZO la uhaba wa maji katika Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro limeanza kukwamisha kazi ya ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo inayojengwa kwa fedha za serikali katika kijiji cha Kiwanda, Kata ya Kirongo Samanga.

Msimamizi Mkuu wa mradi huo, Mhandisi Boniface Vedasto, ameeleza kuwa ujenzi huo kwa sasa unasuasua kutokana na changamoto ya uhaba wa maji ambao unasababisha mafundi kusimamisha shughuli zote za ujenzi kila siku, ifikapo saa 7:00 mchana.

Jana, mhandisi huyo alikuwa akitoa taarifa kwa wajumbe wa kamati ya utekelezaji ya Umoja wa Vijana Mkoa wa Kilimanjaro (UVCCM) walipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa hospitali hiyo.

"Kwa sasa tupo katika zoezi la kumwaga zenge na kushindilia na kimsingi kazi hii inahitaji maji ya uhakika, lakini tunakwama kwa sababu ya changamoto ya uhaba wa maji. Kila inapofika saa 7:00 mchana maji hukatika na inatulazimu sisi kusimamisha shughuli zote hadi siku inayofuata," alisema.

Serikali imetoa kiasi cha Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo na tayari awamu ya kwanza ya fedha hizo Sh. milioni 500 zimeshapokelewa.

Fedha hizo zinagharamia ujenzi wa majengo sita ambayo ni jengo la utawala, jengo la kufulia, stoo ya dawa, jengo la wagonjwa wa nje, maabara na jengo la mionzi.

Katika taarifa yake, Mhandisi Vedasto amesisitiza mbele ya wajumbe hao kuwa kama changamoto hiyo ya maji ikishindwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka, inaweza kusababisha ujenzi huo wa hospitali ya wilaya kutokukamilika kwa wakati uliopangwa.

Alipoulizwa kuhusu changamoto hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Arbogast Zacharia, alisema kukosekana kwa maji katika eneo hilo la ujenzi wa hospitali ya wilaya wanalijua na kwamba wako katika majadiliano na kampuni ya maji ya Kili Water inayotoa huduma katika eneo hilo kuona inawezaje kuacha maji yakapatikana kwa muda wote eneo la ujenzi.

"Unajua awali eneo hili lilikuwa halina maji na halmashauri ilitenga fedha shilingi milioni 67 za kuvuta maji yaliyokuwa umbali wa kilomita tano kutoka chanzo hicho kilipo, lakini kutokana na ukame ulipo kwa sasa chanzo hicho kimeanza kukauka," alijitetea mkurugenzi huyo.

Akitoa ushauri wake, Katibu wa UVCCM Mkoa wa Kilimanjaro, Abdulrahim Hamid, aliitaka halmashauri ya wilaya hiyo kufikiria umuhimu wa kuchimba kisima cha chini katika eneo hilo ili maji yatakayopatikana yasaidie kuendesha shughuli za ujenzi wa hospitali hiyo.

Katika hospitali yoyote vitu muhimu vinavyohitajika ni umeme wa uhakika pamoja na maji, hivyo uwepo wa kisima kitakachochimbwa kitasaidia kasi ya ujenzi kuongezeka na pindi ujenzi utakapokamilika maji hayo yataendelea kutoa huduma kwa wagonjwa," alisema Hamid.

# Nipashe TESA

Jumanne Aprili 2, 2019

TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI



Ukurasa 18

## JE, WAJUA?

PAKA SHUME NA MBWA KOKO WANALAUMIWA KWA KUHARIBU




## Mrima, Bara walivyovuruga Kiswahili cha Unguja, Pwani

Ukurasa 15



# Utatuzi migogoro nje ya Mahakama, nuru kwa pande zinazotofautiana

Ukurasa 16



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Upotoshwaji wa maneno ya Kiswahili

SHAKA (hali ya kuwa na wasiwasi juu ya jambo) yangu ni jinsi Kiswahili kinavyoborongwa (haribu kazi kwa kasi; atili, banganga) na waandishi wa magazeti yetu ya Kiswahili!

Matokeo yake sasa hata kuandika sentensi zenye mtiririko unaoeleweka zatushinda waandishi. Kwa muktadha huu, 'maana' ni dhana inayowakilishwa na neno; ufafanuzi wa kitu au jambo. Kinyume chake ni upotoshaji yaani kitendo cha kufanya mtu mwingine afanye jambo lisilokuwa sahihi.

Ingawa yapo baadhi ya maneno yenye maana zaidi ya moja, sioni sababu ya waandishi kupotosha maana halisi ya maneno ilhali yapo maneno sahihi lakini hatuyatumii. Badala yake twatumia maneno yaliyo tofauti na maudhui (wazo kuu linaloelezwa katika maandishi au katika kusema) ya kazi zetu.

'Mwisho' ni ukomo wa jambo; kikomo, hitimisho; hali ya kumalizika, tamati. Kwa hiyo isemwapo "mwisho wa siku" maana yake ni mwisho wa siku husika. Soma sentensi ifuatayo:

"Akizungumza na ... (jina la gazeti) jana, Katibu Mkuu wa Klabu ya Lipuli, Julius Leo, alisema walikuwa wamemtengea dau Boban na alikubali kwenda kusaini mkataba, lakini mwisho wa siku wakasikia amechukuliwa na Yanga."

"Mwisho wa siku" hutumiwa na watu wengi kiasi cha kuonekana ni maneno sahihi kumbe sivyo. Badala ya kuandika "mwisho wa siku" ingeandikwa 'mwishowe' au 'hatimaye.'

"Makambo alifunga bao lake la tisa msimu huu wakati Yanga ikipata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Ruvu Shooting katika pambano lililopigwa Uwanja wa Taifa ambapo msemaji wake, Masau Bwire aliamua kuchomoa bastora ili kuwatawanya mashabiki wa Yanga waliokuwa wakimzonga mara baada ya pambano hilo kali."

Waandishi wa michezo wamezoea sana kuandika "pambano lilipigwa ..." Pambano 'halipigwi' bali huchezwa. Kosa la pili la mwandishi ni kuandika kuwa Masau Bwire alichomoa 'bastora,' neno lisilokuwa na maana yoyote kwa Kiswahili! Neno sahihi ni 'bastola' yaani bunduki ndogo fupi ambayo aghalabu hufichwa mwilini bila ya kuonekana.

"Simba yazidi kutetema Bara" ni kichwa cha habari kwenye gazeti mashuhuri la michezo nchini. Je, ni kweli kuwa Simba ilitetema? Maana ya 'tetema' ni kitendo cha kutikisika, harakaharaka; tetemeka. Ingeeleweka kama ingeandikwa "Simba yatetemesha Ligi Kuu."

Kichwa kingine cha gazeti hilohilo kiliandikwa: "Kitendo cha mashabiki kuvamia uwanjani lidhibitiwe mapema." Mwandishi angeandika "Kitendo cha mashabiki kuvamia uwanja kidhibitiwe mapema" badala ya "kitendo ... lidhibitiwe." 'Kitendo' ni kundi la maneno yanayotaja matendo kama vile lala, tembea, pumua n.k.

Waandishi tunavyoharibu maneno: "Mara baada ya kuanza kwa Ligi Kuu Bara kikosi cha Yanga hakikuwa kikipewa nafasi kubwa ya kutamba kutokana na kuwa na wachezaji wengi wa kawaida, huku mafundi wakiwa ni wachache mno." Sentensi ya maneno 31 yaliyoandikwa shelabela (hali ya kukosa mpango maalumu)!

Ingeandikwa: "Ligi Kuu ya Bara ilipoanza, Yanga haikupewa nafasi kubwa ya kufanya vizuri kwani wachezaji wengi walikuwa wa kawaida wakati mahiri wakiwa wachache." (Maneno 22). 'Mahiri' ni -enye uhodari wa jambo fulani.

Sentensi ya mwisho ya habari hiyo haikumalizika; kwa hiyo haikueleweka! "Mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba, wanashika nafasi ya tatu baada ya kujikusanyia pointi 27 kutokana na" (Mwandishi alikomea hapo bila kueleza ni kutoka na nini.) Haraka haraka haina baraka! Wanaodurudusu (wanaopitia maandiko ili kusahihisha) hawakuwa makini katika kazi yao.

"Kikosi changu ni kizuri na tunatambua tunaenda kucheza na timu nzuri lakini mara nyingi huwa kikosi cha ushindi katika timu yoyote hakibadilikagi," alisema Aussems ambaye alichukua mikoba ya kukinoa kikosi cha Simba kutoka kwa Pierre Lechantre. (Maneno 36 katika sentensi moja).

'Haibadilikagi' si Kiswahili sanifu (-enye kufuata vigezo vilivyokubalika.) 'Mikoba' ni wingi wa 'mkoba' na maana yake ni chombo cha kusukwa au kushonwa cha kutilia vitu; mkoba wa ukili. Pia ni mfuko wa mganga wa kuwekea zana zake za kazi. Ina maana kocha wa Simba alikabidhiwa mikoba ya uchawi!?

Ingeandikwa: "Kikosi changu ni kizuri na tunakwenda kupambana na timu nzuri. Hata hivyo, mara nyingi kikosi cha ushindi hakibadiliki," alisema Aussems aliyechukua nafasi ya Pierre Lechantre. (Maneno 25 katika sentensi mbili).

"Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alisema beki wao kisiki Juuko amebadilika si kinizamu yaani nje ya uwanja na hata ndani katika kushindania namba anapokuwa mazoezini." (Maneno 31). Neno 'kinizamu' si Kiswahili!

Sentensi imekorogwa sana na kumfanya msomaji arudie kuisoma ili aelewe kilichoandikwa! Ingeandikwa: "Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alisema beki wao mahiri, Juuko, ana nidhamu nzuri mazoezini na nnje ya uwanja." (Maneno 23).

"Hakuna siri mashabiki wa Simba wameanza kumsahau kabisa Haruna Niyonzima kwa sababu ya mavitu ya Clatus Chama ..." Inapoandikwa 'mavitu' ina maana gani? Wingi wa 'kitu' ni 'vitu' sio 'mavitu' kama ilivyoandikwa.

"Makosa hayo ya kimaadili yaliyomtia hatiani Wambura ni pamoja na makosa hayo ni kupokea/kuchukuwa fedha za TFF za malipo ambayo hayakuwa halali, kugushi barua ya kueleza alipwe malipo ya Kampuni ya Jeke System Limited huku akijua malipo hayo sio halali na kufanya vitendo vinavyoshusha hadi ya shirikisho." (Maneno 48 katika sentensi moja iliyoandikwa ovyo!)

Ingeandikwa: "Makosa yaliyomtia Wambura hatiani ni kupokea malipo yasiyo halali, kughushi barua ili apewe malipo ya Jeke System limited na kufanya vitendo vinavyoshusha hadhi ya TFF." (Maneno 25).

**Methali: Pauliwapo nyoka hapaachi ndombezi.**

***marobarnabas@yahoo.com***
***0715/0784 33 40 96***

## ELIMU KUTOKA POLISI



Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Ahmed Msangi. **PICHA: MTANDAO**

# Mchango wa viongozi wa dini katika kuzuia uhalifu

UHALIFU wowote unaotokea katika jamii, unaweza kuzuilika na kutokomezwa, endapo kutakuwa na ushirikiano thabiti kati ya Jeshi la Polisi na viongozi wa dini, kutokana na fursa walio nayo viongozi hao ya kuwa karibu zaidi na kusikilizwa na waumini wao.

Viongozi wa madhehebu mbalimbali, wanaonekana kupata kibali kwa waumini wao na wanajamii kwa ujumla kwani baadhi ya wananchi wamekuwa wakizingatia kwa uaminifu mafundisho na mawaidha wanayopewa na viongozi wao wa kiroho na kuyafanyia kazi kikamilifu na kwa nidhamu ya hali ya juu.

Kwa hiyo, wanaweza kutumia fursa hiyo, kubadili tabia na mienendo ya waumini wao ili kujenga jamii isiyo na uhalifu.

Viongozi wa dini wana mchango mkubwa katika suala zima la kuzuia uhalifu ndani ya jamii, pamoja na kutoa mafundisho kwa jamii yenye kujenga maadili mema, pamoja na kuzuia mmomonyoko wa maadili katika jamii, kwa lengo la kujenga kizazi chenye kuchukia uhalifu.

Kwa kutambua umuhimu wa viongozi wa dini na mchango wao katika maendeleo na usalama wa nchi yetu, hivi karibuni Rais Dk. John Magufuli, mnamo Januari 23 mwaka huu, alizungumza na viongozi wa madhehebu mbalimbali Ikulu jijini Dar es salaam. Lengo lilikuwa ni kusikia kutoka kwao mchango wao katika kuleta maendeleo katika nchi, kukuza uchumi pamoja na mbinu mbalimbali za kutatua kero za kijamii likiwamo suala la uhalifu.

Baadhi ya viongozi wa dini walieleza kuwa kuongezeka kwa nyumba za ibada na mafundisho mazuri ya dini na maadili yakitolewa kwa vijana na jamii kwa ujumla yatapelekea kuzaliwa kwa jamii yenye maadili mema ambayo yatachangia katika kuzuia uhalifu.

Jeshi la Polisi, likiendelea kuimarisha ushirikiano na viongozi wa dini wataweza kung'oa mizizi yote na mazalia ya vitendo vya uhalifu katika jamii.

Itakumbukwa kuwa, Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, wakati wa ziara zake katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, alipata fursa ya kuhudhuria ibada ya kubariki kanisa la Mtakatifu Petro Kigango cha Kiloleli, Parokia ya Ilumya Wilayani Busega mkoani Shinyanga.

Katika kusanyiko hilo la ibada, aliwaeleza waumini kuwa amani ni msingi wa maendeleo wa taifa lolote duniani hivyo, viongozi wa dini kote nchini wanatakiwa kuendelea kuhubiri amani ili kuimarisha utulivu na usalama.

IGP Sirro alisema kuwa, suala la amani na utulivu ni la msingi sana katika nchi yetu na kwa kuwa kila mwananchi ana dini yake na tunaamini kuwa viongozi wa dini, ni kundi la watu wanaosikilizwa sana na waumini hivyo wakikemea uhalifu kwa msisitizo, taifa, jamii zetu zitaendelea kuwa salama.

"Vitendo vingi vya uvunjifu wa amani ikiwamo mauaji ya vikongwe yanachangiwa na watu kukosa hofu ya Mungu, hivyo nyumba za ibada zikiwemo makanisa na misikiti zinapojengwa kwa wingi zitakuwa msaada mkubwa kwa watu," anasema IGP Sirro.

Polisi pekee hawezi kukabiliana na uhalifu, bila ya kushirikiana na jamii wakiwamo viongozi wa dini, ili kuushinda uhalifu. Viongozi wa dini ndio wadau wakubwa wa kuimarisha amani, kutokana na ushawishi walio nao kwa waumini.

Sote tuna jukumu la kufichua uhalifu na wahalifu kupitia taarifa za waumini wetu, hasa kwa viongozi wetu wa dini kuendelea kuhubiri na kutoa mawaidha katika maeneo yao ya ibada, kwani bila amani, hakutakuwapo na shughuli zozote za maendeleo.

Wahalifu wa siku hizi wamekuwa wajanja na wanatumia mbinu nyingi za kisasa, silaha kubwa inayoweza kusaidia katika mapambano dhidi ya uhalifu ni mshikamano wa dhati kutoka kwa viongozi wa dini katika kuwafichua wahalifu, ili hatua kali za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

Jukumu la viongozi wa dini ni kuwafichua wahalifu waliopo katika maeneo yao, kwa kutoa taarifa ya viashiria vyovyote vya uhalifu. Pia, kuendelea kuziboresha kamati za ulinzi zilizoundwa kwenye nyumba za ibada, ili ziweze kuwa na tija na upekee katika kudumisha amani.

Nihitimishe kwa kusema kuwa, viongozi wa dini wana dhamana kubwa katika kuhakikisha vitendo vya kihalifu vinadhibitiwa nchini kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, katika kuwaelimisha waumini wao na jamii kwa ujumla juu ya madhara ya uhalifu kwa kuwapa mafundisho yanayolenga kujenga na maadili mema, kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**S.L.P 9141**
**Dar es Salaam.**
**Baruapepe:habariphq@yahoo.com**
**habari.phq@tpf.go.tz**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Mrima, Bara walivyovuruga Kiswahili cha Unguja, Pwani

WAKATI takriban kila Mtanzania anajivunia lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa, na baadhi ya wasomi wanaopigania lugha hiyo itumike kufundisha kuanzia chekechea hadi chuo kikuu wanadai ni lugha ya kuzaliwa ya Watanzania walio wengi, yapo matatizo tena si madogo katika Kiswahili.

Nje ya kuundwa kwa misamiati bunifu inayoongewa na kikundi kidogo cha wataalamu wanaofanya utafiti na 'usawiri' maneno, halafu watake kuibebesha jamii maneno yao ya kitaaluma, yapo matatizo pia ya watumiaji wa kawaida.

Kimsingi hilo lingekuwa eneo halisi la utafiti katika taasisi za Kiswahili lakini hazifanyi hivyo, zinajibidiisha kukiondoa Kiingereza kabisa.

Kwanza kuna tatizo limejichimbia la watumiaji wa Kiswahili Bara kushindwa kutofautisha herufi 'l' na 'r' na tatizo hilo kuwa ugonjwa ambao unaenea kwa kasi.

Inakuwa hakuna haja ya kuonyesha tatizo kama hilo linapotokea katika maandishi kwani ni kama udhaifu wa kimsingi miongoni mwa watumiaji Bara, kwani wanajaribu kwa njia zote kuweka 'r' pale ambalo ipo 'l,' na kinyume chake vile vile; yaani lazima wakosee.

Mtu anapojua Kiingereza kwa kiasi fulani, hahitaji kusaidiwa kuandika 'Michael,' au 'John.'

Ukiangalia chimbuko la tatizo hilo unalikuta linaanza kwa kiwango fulani wakati wa uhuru, ambako utamaduni wa Kiswahili jijini Dar es Salaam ulikuwa kitu kimoja na ule wa Zanzibar, Tanga na Mombasa, wakati wakazi wa Bara walikuwa wageni tu, Kiswahili chao hakisikiki kiasi hicho.

Punde baada ya uhuru hali ikabadilika, likaanza kuwapo kundi la watu wanaoitwa 'viongozi,' ambao hawakuwa tena wanajitambulisha wakiwa na makundi ya wakazi asili wa jiji au wazee na wasomi wenye utamaduni huo wa pwani.

Wakawa huru zaidi kuongea kwa jinsi wanavyojisikia, na wakaanza kuongezeka wanaotoka maeneo ya mbali Bara, Kiswahili kipya kikachipukia hapo.

Ila ni wakati wa Azimio la Arusha ambako tatizo hilo lilianza kuota mizizi, hasa kwa kuanza kufifia lugha ya Kiingereza, wafundishaji kutoka nje wakiondoka nchini kwa haraka baada ya shule kutaifishwa.

Juhudi zikaanza katika 'Wizara ya Elimu ya Taifa' kubadilisha mifumo ya masomo (yakatungwa maneno mapya kama 'mitaala') iliyokuwepo, ikaitwa ni ya kikoloni, wakati viashiria vya ukoloni vilishaondolewa kuanzia mapema 1962, na wakati huo ni miaka mitano baadaye. Kwa mfano watoto shule za msingi walikuwa wanaimba 'When I was a little boy/My mother kept me well/Now I am a big boy/Soldier fighting for the Queen,' ambao ulifutwa shuleni.

Kilichokuwa kinaondolewa wakati huo haikuwa ukoloni au hisia za aina hiyo bali Kiingereza na chochote kile ambacho kinaonyesha ukaribu na Uingereza au uzungu kwa jumla, ikiwa ni pamoja na historia ya dunia, hatua kwa hatua ikafutwa ikabaki ya Afrika.




Makao Makuu ya Wizara ya Elimu Zanzibar, inayosimamia uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kwa upande wa Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

> Kwa upande mwingine, Kiswahili kimebebeshwa matatizo ya hitilafu au tofauti za matamshi kati ya makabila na hata koo tofauti, jinsi tatizo hilo la jumla la 'l' na 'r'

Ukiona vijana hawajui kufikiri vyuo vikuu ni kwa vile hawana ufahamu wa dunia ilivyo na hisia ya jema inavyokua au ilivyojengeka katika historia, hawana mifano ya himaya zilizoinuka na kuanguka na mijadala au fikra zinazohusiana na kilichotokea katika nyakati hizo.

Ilikuwa ni kuingiza mfumo wa kufikiri unaoijua Tanzania na Afrika kama bara la watu weusi wakipinga ukoloni; hatukuwa sehemu ya dunia.

Kufuta udhaifu huo wa kufikiri ndiyo tatizo siyo la Tanzania peke yake bali nchi nyingi tu, licha ya kuwa nchi kama Kenya hazikuvuruga mifumo ya awali baada ya uhuru - kuondoa tu viashiria vya ukoloni lakini kubakiza ufahamu mpana wa dunia na hisia ya jema katika historia.

Ndani ya mabadiliko hayo vizuizi vya kuongeza hisia au maneno ambayo mwanzoni yangechujwa ikaondoka, wakaanza kujenga Kiswahili kwa kuchota maneno ya Kiarabu kwa upande mmoja na lugha za makabila ya mikoa ya pwani ambao kimsingi ni mrima, si pwani asilia, kama Wazaramo na Wadengereko.

Udhaifu wao wa kuongea Kiswahili ukawa sasa ndiyo nembo ya lugha hii.

Ni katika mazingira hayo ambako suala la kutumia Kiswahili kwa usahihi lilianza kufifia kidogo kidogo, licha ya kwamba limekuwa tatizo sugu katika vizazi vya baadaye, visivyopitia shule za baada ya uhuru ila 'baada ya miaka 50' kama alivyosema Shaaban Robert.

Kile cha kuongea barabarani miongoni mwa watu wa Bara ndiyo Kiswahili; hawajui tofauti ya 'mtoto' na 'mwana' na hawawezi kuandika kwa usahihi jina la Kilatini, ni kazi.

Kwa upande mwingine, Kiswahili kimebebeshwa matatizo ya hitilafu au tofauti za matamshi kati ya makabila na hata koo tofauti, jinsi tatizo hilo la jumla la 'l' na 'r'

Kwa vile kila jina nchini lina mtu wake aliyeliwezesha kushika kasi ya kufahamika miongoni mwa watu, hata kama si kwa kwanza kusikika katika vyombo vya habari akiwa na jina hilo, anavyolitumia inakuwa kanuni ya kuandika jina hilo.

Ila kwa kusema kweli, baadhi ya matatizo haya yanaanzia mbali, kuwa mfumuko wa lugha kutoka Babeli kuwa lugha maridhawa badala ya moja waliyokuwa wakiongea familia ya Nuhu katika safina (baadhi wanadhani kuwa hizi ni hadithi tu) ni hitilafu hizo za matamshi.

Kuna kisa wakati wana wa Yakobo wanaingia nchi ya ahadi na lugha yao inafanana na ya wana wa Kanaani (Waamori, majirani wa Ibrahimu, ni Wamasai wa asili, mori ni kupandwa na shauku muhimu, walikuwa na jadi hiyo), na hivyo ikawa rahisi kujichanganya.

Waisraeli wakatoa ishara kwa makamanda wa vita kuwa mgeni akija anasema ni Mwisraeli atamke 'shibolethi'; akisema 'sibolethi' anadakwa.

Wanajua ni jasusi anajaribu kupenya lakini hana matamshi ambayo kila Mwisraeli anaweza kirahisi.

SHERIA

**NA FRANSISKO MPANGALA**

# Utatuzi migogoro nje ya Mahakama, nuru kwa pande zinazotofautiana

## ■Unaokoa muda, gharama

KUGOMBANA au kutofautiana kwa Wanadamu ni jambo la kawaida kutokea katika maisha yetu ya kila siku.

Lipo kundi la Wanahistoria wanaoamini kuwa chanzo cha wanadamu kutofautiana kulianzia pale mfumo wa kumiliki mali kwa mtu binafsi ulipoanza.

Kwamba hapo mwanzo wanadamu wote walikuwa sawa, kila mtu alikuwa na umiliki sawa kwa kila kilichopo kwenye jamii aliyokuwa akiishi na kila mali iligawanywa sawa kwa watu wote (ardhi, wanyama).

Wanahistoria hawa wanaamini kuwa, endapo mfumo wa kumiliki mali usingekuwapo (private ownership), basi dunia isingekuwa na mgogoro wowote.

Mbali na mtazamo huu wa kihistoria, zipo sababu mbalimbali zinazosababisha migogoro kutokea katika jamii zetu.

Mahusiano mabaya baina ya pande mbili, kutoridhishwa na matendo au maneno ya upande mmoja dhidi ya mwingine, dhuluma, uonevu ni kati ya sababu chache za migogoro kutokea katika jamii zetu.

Migogoro inatafsiriwa kuwa ni hali ya kugombana kati ya pande mbili (au zaidi) juu ya jambo fulani.

Migogoro isipotatuliwa kwa mbinu au njia sahihi, upo uwezekano wa madhara mbalimbali kutokea.

Madhara kama uvunjifu wa amani, vifo, chuki, vurugu, uharibifu wa mali ni kati ya mambo yanayoweza kutokea endapo hatua za haraka hazitachukuliwa kutatua migogoro inayojitokeza.

Kwa maana hii, migogoro haipaswi kudharauliwa au kupuuzwa pale inapotokea katika jamii zetu.

Dawa ya mgogoro wowote ni utatuzi, hakuna mbadala.

Kwa kuwa watu wanafahamu madhara ya kutotatua migogoro yao, chombo maarufu ambacho watu wengi hupenda kukitumia kutatua migogoro na kupata haki zao ni Mahakama.

Mahakama ndio mhimili wa dola uliopewa mamlaka na katiba ya nchi kutatua migogoro inayojitokeza kati ya pande mbili.

> Ingawa njia ya upatanishi inategemea maafikiano ya wahusika walio kwenye mgogoro kuitumia, ipo migogoro ambayo ni lazima itatuliwe kwa njia ya upatanishi kama njia ya awali kabla mgogoro haujapelekwa mahakamani.

**CHANGAMOTO**

Pamoja na kwamba Mahakama ina umuhimu mkubwa na nafasi ya kipekee katika kutatua migogoro na kutoa haki kwenye jamii, mchakato wa kutoa haki na kutatua migogoro unaofanywa na Mahakama unakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Changamoto ya kwanza ni kuwa mchakato wa kutatua mgogoro mahakamani unahusisha gharama za kifedha kwa wahusika waliopeleka mgogoro wao mahakamani.

Wahusika wanapaswa kujiandaa kuwalipa mawakili, kulipia malazi (maeneo ya kulala) kama mahakama ipo mbali na makazi yako, kulipia gharama za nauli za kwenda mahakamani na kurudi makwao kwa siku ambazo watahitajika mahakamani.

**MUDA**

Changamoto ya pili ya kutatua mgogoro mahakamani ni kuwa mchakato wake unagharimu muda (mrefu au mfupi) kwa wahusika waliopeleka mgogoro wao mahakamani.



Usuluhishi nje ya Mahakama una mchango mkubwa wa kuepusha migogoro mbalimbali ikiwamo ya ardhi unaozikumba jamii mbalimbali nchini kama ilivyo kwa wakazi hawa wa Simanjiro. **PICHA: MTANDAO**

Wahusika waliopeleka mgogoro wao mahakamani wanapaswa kwenda mahakamani kusikiliza mwenendo wa shauri lao kila wanapohitajika, kusubiri upelelezi kukamilika, kutoa ushahidi kwa awamu kwa pande zote mbili zilizo kwenye mgogoro.

Haya ni mambo yanayogharimu muda kwa wahusika waliopeleka mgogoro wao mahakamani.

**UTAALAMU WA KISHERIA**

Changamoto ya tatu ni kuwa mchakato wa kutatua mgogoro mahakamani unatumia mbinu, ufundi na utaalamu mwingi wa kisheria katika kuendesha kesi zake.

Ingawa kutojua sheria sio hoja ya utetezi, lakini ukweli ni kuwa watu wengi hawazijui sheria za nchi vizuri. Japokuwa wahusika wanaweza kupewa msaada wa kisheria, upo uwezekano wa mtu kupoteza haki yake kwa kuwa tu hazifahamu mbinu na taratibu mbalimbali za kuendesha na kushinda kesi husika.

Uwepo wa changamoto hizi katika mchakato mzima wa kutatua mgogoro mahakamani, umewafanya baadhi ya watu kupendelea kutatua migogoro yao nje ya Mahakama.

**UPATANISHI**

Natambua uwepo wa njia na mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kutatua migogoro nje ya Mahakama.

Hata hivyo, makala hii itajadili njia ya upatanishi (mediation) kama moja ya njia ninayoiona kuwa na ufanisi mkubwa katika kutatua migogoro nje ya Mahakama.

Upatanishi ni hali ya kusuluhisha pande mbili au zaidi zilizo na ugomvi au mgogoro.

Hapa pande mbili (au zaidi) zilizo na mgogoro huamua kukutana na kumchagua mpatanishi au mtu wa tatu asiye na maslahi yoyote katika mgogoro husika, atakayezisaidia pande zilizo na mgogoro kupata suluhu.

Kazi kubwa ya mpatanishi ni kuponya mahusiano yaliyoathiriwa na mgogoro uliojitokeza na kuhakikisha pande mbili zilizo na mgogoro zinapatana.

Zipo faida mbalimbali za kutatua migogoro kwa njia ya upatanishi. Kwanza, upatanishi ni njia inayotumia muda mfupi kutatua migogoro.

Taratibu za kufungua kesi, kuita mashahidi, kusubiria upelelezi ukamilike, kuanza kutoa ushahidi kwa awamu, matumizi ya mbinu na ufundi mwingi ni vitu visivyokuwapo kwenye upatanishi tofauti na inavyofanyika mahakamani.

**GHARAMA NDOGO**

Faida ya pili ni kuwa, njia ya upatanishi hutumia gharama ndogo katika zoezi zima la kupata suluhu ya mgogoro.

Mbinu hii haihitaji kuajiri mawakili, kulipa nauli za kwenda na kurudi mara kwa mara kusikiliza kesi husika na nyakati nyingine kuingia gharama za malazi na chakula kama Mahakama ipo mbali na makazi.

**KUJIELEZA**

Faida ya tatu ni kuwa, kutatua migogoro kwa njia ya upatanishi kunatoa uhuru mkubwa zaidi wa kujieleza kuliko ule unaotolewa mahakamani katika kutatua mgogoro.

Sisemi kuwa Mahakama haitoi uhuru wa kujieleza, lakini njia ya upatanishi kutokana na mazingira na utaratibu wake, inatoa uhuru zaidi kwa pande zilizo kwenye mgogoro kujielezea kwa uhuru zaidi.

Upatanishi hauhitaji kutumia mbinu nyingi za kisheria, hauna haja ya kutumia lugha rasmi ambazo ni Kiingereza na Kiswahili tu kwa upande wa Mahakama (lugha yoyote kama Kingoni, Kisukuma kinaweza kutumika kupatanisha).

Uwepo wa idadi ndogo ya watu katika mbinu hii kunawatengenezea mazingira rafiki kwa wahusika kufunguka kiundani zaidi.

Isitoshe, mfumo wa kutoa haki mahakamani ni aidha upande mmoja ushinde na mwingine upoteze (adversarial system).

Mfumo huu unalenga kutenda haki kwa upande unaostahili.

Hata hivyo, mfumo wa mmoja kupoteza na mwingine kushinda unaweza kujenga kinyongo kwa upande ulioshindwa kesi.

Upatanishi ni mbinu ya kusuluhisha mgogoro kwa haraka na amani kwani hakuna upande unaoondoka na ushindi katika usuluhishi, wote mnapata kidogo na kupoteza kidogo (win-win situation).

Ingawa njia ya upatanishi inategemea maafikiano ya wahusika walio kwenye mgogoro kuitumia, ipo migogoro ambayo ni lazima itatuliwe kwa njia ya upatanishi kama njia ya awali kabla mgogoro haujapelekwa mahakamani.

**REJEA**

Katika kesi ya Hector Sequeiraa dhidi ya Kampuni ya bia ya Serengeti iliyosikilizwa katika Mahakama Kuu kitengo cha kazi (Lalamiko la kazi Namba 20 la mwaka 2009), Mahakama iliyatupilia mbali malalamiko ya kikazi yaliyofunguliwa kwa sababu mlalamikaji alishindwa kufuata utaratibu wa kisheria unaotaka migogoro ya kikazi kufanyiwa upatanishi kabla ya kupelekwa mahakamani kama inavyoelekeza Kanuni ya 20 kwenye tangazo la Serikali Namba 67.

**KASORO**

Hata hivyo, hakuna zuri linalokosa kasoro.

Moja ya changamoto kubwa inayoukabili upatanishi kama njia ya kusuluhisha migogoro ni kutoweza kumbana au kujenga mazingira thabiti ya kulazimisha makubaliano yaliyofikiwa kufuatwa barabara.

Ingawa msuluhishi anapaswa kuyaandika makubaliano yaliyofikiwa na kusainiwa na pande zote baada ya kuafiki kilichoandikwa, bado uwezekano wa kutofuata makubaliano ni mkubwa.

Isitoshe mara nyingi upatanishi unafanywa kienyeji sana, ukitegemea nia njema ya pande zilizo katika mgogoro kufuata makubaliano waliyofikiwa.

Pamoja na changamoto hii, upatanishi ni njia muafaka sana ya kutatua migogoro mingi inayojitokeza kwenye jamii zetu.

Endapo njia hii itatumiwa ipasavyo, itasaidia sana kupunguza mrundikano wa kesi nyingi katika mahakama zetu, kwani ipo baadhi ya migogoro inayoweza kupatiwa ufumbuzi bila kuipeleka mahakamani.

Barua pepe: fransiscompangala08@gmail.com

JIELIMISHE



Utafiti huu ni msaada mkubwa kwa wagonjwa wa kifafa, ili kuubaini mapema kabla ya athari kujitokeza. **PICHA: MTANDAO**

# Mbwa wabaini dalili za kifafa kwa kunusa

WANASAYANSI wa Ufaransa wanasema wana ushahidi wa kitafiti kuwa mbwa anaweza kuhisi dalili za ugonjwa wa kifafa.

Timu ya Chuo Kikuu cha Rennes nchini humo ina matumaini kuwa uvumbuzi wao utawezesha wataalamu kubaini mtu mwenye dalili za ugonjwa wa kifafa.

Inaweza kuwa mbwa au pua za 'kielektroniki' zinazoweza kunusa harufu inayotoka kwa mtu mwenye dalili ya ugonjwa wa kifafa.

Utafiti huu ni msaada mkubwa kwa wagonjwa wa kifafa, katika kubaini mapema kabla ya athari kujitokeza.

Awali, mbwa walionyesha kuwa na uwezo wa kunusa harufu zinazoashiria kuwapo kwa dalili ya maradhi kadhaa ikiwamo saratani, malaria na kisukari.

Baadhi ya watu wenye kifafa huwategemea wanyama.

Mnyama mmoja akiwa kwenye chumba alicholala mtoto, anaweza kuitahadharisha familia kuwapo kwa dalili ya kifafa wakati wa usiku wa manane.

Katika utafiti wa hivi karibuni, ulioandikwa katika jarida la ripoti za kisayansi, mbwa watano walipata mafunzo nchini Marekani kubaini harufu ya jasho la mtu aliye na kifafa.

Mbwa wawili kati yao walibaini dalili za kifafa karibu kiasi cha theluthi mbili na wengine watatu walikuwa wamepatia kwa asilimia 100.

Ripoti inasema kuwa majibu yako wazi kabisa na ilihusisha kubaini harufu ya mtu mwenye dalili ya kifafa.

Hata hivyo, haijulikani ni kwa vipi dalili za kifafa zinaonekana katika mabadiliko ya harufu.

Dk. Amelie Catala wa Chuo Kikuu cha Rennes ameiambia BBC kuwa: "Utafiti zaidi unahitajika lakini inawezekana kuwa mabadiliko mwilini husababisha kutoka kwa homoni zinazosababisha kutoa harufu ya aina ya tofauti, lakini nadharia hii bado iko kwenye majaribio."

Utafiti huu unaelezwa kuwa msaada mkubwa kwa wagonjwa.

Ripoti inasema utasaidia kuboresha namna ya kutambua dalili za kifafa mapema zaidi, hali itakayoweza kumsaidia mtu kuomba msaada au kujiondoa kwenye maeneo ya hatari kabla ya kuanguka na kifafau.

**BBC**

UTAFITI

# Je, ni wakati gani ambao mtu anafaa kuitwa mzee?



Utafiti unasema umri ni suala la tarakimu na si vinginevyo. **PICHA: MTANDAO**

MWANAMKE wa umri wa miaka 45 anayeishi Papua New Guinea atahisi kuwa na umri wa miaka 76 nchini Ufaransa ama Singapore.

Na atahisi kuwa na umri kama huo anavyohisi mwanamke wa miaka 65.

Hayo ndio matokeo ya utafiti mkubwa uliofanywa na wanasayansi wa kimataifa na kuchapishwa katika jarida la Lancet.

Watafiti hao walichanganua takwimu za afya kutoka mataifa 195 na kubaini kwamba kwa ujumla watu huwa na wasiwasi wa umri wanapofikisha miaka 65.

Walibaini kuwa matatizo ya kiafya kama vile ukosefu wa kusikia vizuri, mshtuko wa moyo, majeraha ya mara kwa mara na magonjwa ya neva yanaweza kuathiri katika viwango tofauti vya miaka kulingana na eneo mtu analoishi.

Na tofauti kati ya wale wanaozeeka vizuri pamoja na wale wanaozeeka mapema inaweza kuwa ya miongo, mitatu ama hata zaidi.

Utafiti huo pia unaangazia mzigo wa magonjwa yanayohusishwa na umri mtu anapozidi kuzeeka.

Utafiti huo unaonyesha kuwa maisha marefu katika umri wa uzee unaweza kuwa fursa ama tishio la idadi ya watu, kulingana na magonjwa yanayohusishwa na afya, kulingana na Dk. Angela Chang, kiongozi wa utafiti huo.

Watafiti hao walitafuta magonjwa 92, ambayo husababisha madhara katika afya ya maungo na yale ya kiakili.

Magonjwa mengi ni yale yanayohusisha moyo na saratani.

Hesabu hiyo imeongezwa kutokana na maeneo ya watu wanayoishi ikizingatia hatua zilizopigwa na kila taifa kimaendeleo.

Inatokana na kiwango cha mapato, elimu, kiwango cha rutuba ya uzazi.

Lakini huku mataifa yaliyoendelea yakiwa na kiwango kifupi cha maisha bado yanahisi athari za kuzeeka.

Uchanganuzi huo unaonyesha kwamba magonjwa yanayohusishwa na umri ndio tatizo kubwa la watu wanaozeeka duniani.

Matatizo ya umri yanayosababishwa na umri yanaweza kumfanya mtu kustaafu mapema, kusababisha gharama ya juu ya kimatibabu, huku viongozi wa serikali wakitakiwa kuangazia suala hilo wakati watu wanapoanza kuathirika, Chang anaongeza.

Wanasayansi sasa wanatafuta njia za kuzuia sababu zinazoweza kuchelewesha mtu kuzeeka.

Zinaweza kuwa sababu kadhaa kutoka zile za maungo, kuacha kuvuta sigara hadi mipango bora ya mifumo ya kiafya.

Kuelewa haya ni muhimu katika changamoto za kukabiliana na watu wanaozeeka.

**BBC**

JE, WAJUA?

# Paka shume na mbwa koko wanalaumiwa kwa kuharibu



Paka shume wanaweza kuua baadhi ya wanyama mwituni. **PICHA: MTANDAO**

WANASAYANSI wanapigia chapuo kutengwa ama kutokomezwa kabisa kwa kwa paka shume, mbwa koko, panya, mbuzi na nguruwe katika baadhi ya maeneo ili kulinda viumbe vilivyo hatarini kutoweka.

Endapo wanyama hao wataondoshwa kwenye zaidi ya visiwa 100 kunaweza kulinda viumbe waliyomo hatarini kutoweka, wanashauri timu ya wanasayansi wa kimataifa.

Visiwa mbali mbali duniani vimepoteza zaidi ya asilimia 75 ya ndege, wanyama wa nchi kavu na majini katika ndani ya miaka 500 iliyopita.

Upotevu huo kwa kiasi kikubwa umechangiwa na wanyama ambao walipelekwa na binadamu katika maeneo hayo, mathalan paka na mbwa.

Wanyama hao wa kufugwa majumbani sababu hawana asili ya maeneo hayo, huwa tishio kubwa kwa viumbe vyenye asili ya maeneo hayo.

“Kuwatokomeza wanyama wawindaji katika visiwa ni moja ya njia kubwa ya kuondosha hatari ya viumbe wa visiwani kutokutokomea na kulinda baioanuwai,” amesema Dkt Nick Holmes, kutoka kwenye kundi la wanasayansi la Island Conservation.

Utafiti wao umebainisha visiwa 107 ambavyo iwapo wanyama wawindaji wakiondoshwa kutasaidia kutunza asilimia 9.4 ya viumbe vilivyo kwenye hatari ya kutoweka duniani.

Stuart Butchart, mwanansayansi mkuu wa Birdlife International, amesema iwapo hatua hizo zitachukuliwa itasaidia pakubwa kuwalinda “viumbe wa kipekee ambao wamekuwa kwa upekee na katika mazingira yao binafsi ambao hupatikana katika visiwa vya mbali kabisa.”

Tayari baadhi ya visiwa vimeshaanza kutekeleza mangamizi hayo. Programu kubwa zaidi ya kutokomeza panya hivi karibuni ilitangazwa kufanikiwa katika visiwa vya South Georgia. Visiwa hivyo ambavyo ni milki ya Uingereza kusini mwa bahari ya Atlantiki kwa mara ya kwanza katika miaka 200 havina panya kabisa.

“Utafiti huu unaonesha namna gani ni muhimu kuondosha wanyama wavamizi ili kuzuia kutomea zaidi kwa viumbe asilia na vilivyo kwenye hatari. Kinachohitajika sasa ni utashi wa kisiasa na fedha ili kutekeleza miradi hii ili kuvirejeshea visiwa hivi sura yake asili ya kimazingira inayovutia,” amesema Jonathan Hall ambaye ni Mkuu wa milki zote za Uingereza zilizopo maeneo ya mbali. **BBC**

# ELIMU

## NA DANIEL COYLE

UWEZO, kipaji na ujuzi kuimarika kunahitajika miongozo au kanuni za kumfanya mtu ajiendeleze katika ujuzi au uwezo rahisi au mgumu (soft skills or hard skills).

"The Little Book of Talent" by Daniel Coyle ni kitabu kinachotoa miongozo ipatayo 52 ya kuendeleza kipaji, uwezo, ujuzi ndani ya mtu).

Mwandishi amedadavua kwa undani sana namna ya kukuza huu uwezo ndani ya mtu mwenyewe.

Katika hatua yoyote ile ya imarisho la kipaji au uwezo fulani wa mtu huwa na hatua tatu, mosi kuanza kwacho, kujiboresha na tatu kuendelea kuwa imara katika kuanzisha hicho kitu (mf. Kipaji au ujuzi fulani uliojifunza mpaka ukajua.

Kila mmoja ana kitu au uwezo fulani wa kufanya kitu au kukielewa kitu fulani kwa upekee wake, ila namna gani ya kujiboresha au matumizi kwa upana wake kwa wengi, imekua ni changamoto kubwa sana.

Pale unapotumia muda mchache katika siku yako kila siku kwa ajili ya kujiendeleza katika ujuzi fulani au kipaji fulani, kwa kuwa na usikivu wa milango ya fahamu kusikia na kuona, ndivyo jinsi kipaji hukua na kuwa na matokeo makubwa.

Watu mfano wanaopiga muziki kama kinanda, huanza kwa kusikia namna mapigo na kufuata funguo katika kinanda kwa umakini.

Hii ni katika kuleta uungaji wa kinachosikika na kuonekana na mwanafunzi wa muziki.

Nunua notibuku yako ya kuandika maendeleo ya ujuzi wako kila baada ya muda.

Na hii ndio siri waliogundua watu wote wanaofanya vizuri katika maeneo yao ya vipaji na ujuzi kwa sehemu ya kujikumbusha mara kwa mara katika ukuaji wa vipaji vyao.

Kabla ya kuanza au kutengeneza au kujiboresha katika ujuzi, jua ni ujuzi gani mgumu na rahisi kwako?

Ujuzi mgumu unahitaji mazoezi endelevu na nidhamu ya hali ya juu sana na pengine huwa haufurahishi sana.

Wakati ujuzi rahisi ni wenye kufurahisha na wenye uhitaji mdogo tu wa mazoezi.

Kujenga ujuzi mwepesi au rahisi ni kama kushuka mteremkoni, na mara nyingi ujuzi mwepesi huambatana na kufurahia jambo kulifanya.

Kujenga ujuzi mgumu au nidhamu ngumu ni kama kazi ya seremala hodari aanzaye kwa udogo wa vitu, licha ya maboresho katika kazi, huwa haachi kufanya mpaka kamilisho la picha kubwa lifike.

Njia pekee ya kukufanya uwe bora na kuimarika katika ujuzi kuwa ni kama vile na subira ya ukuaji wa mti ulivyo.

Hali ya mazoea ni kikwazo kikubwa sana katika ukuaji wa ujuzi wako au kuendeleza kipaji chako.

Kila siku endelea kunyumbua nyumbua kidogo kidogo, kujiboresha katika ujuzi na kipaji chako kwa kujiboresha zaidi ya ushindi wako wa jana.

Kusogea hatua nyingine zaidi katika kujiboresha huambatana na kutojisikia vizuri, usiache hapa ukikutana na hali hii huenda ni kujifunza muziki au chombo cha muziki, toka katika eneo ulilolizoea "move out of comfort zones".

Jijengee nidhamu ya kuendelea kufanya kwa ubora na kutafuta ubora wa eneo lako kwa undani




Bidii ya kujifunza kama hii inasaidia kumiliki uwezo wa kazi na hivyo ufanisi katika maisha ya kila siku. **PICHA: MTANDAO**

# THE LITTLE BOOK OF TALENT

## Kitabu kidogo kuhusu Kipaji

> Hili hufananishwa na kitendo cha kujifunza katika kitabu kwa kukifunga kitabu na kusoma kurasa 10 zaidi ya mara 4, Kisha unajaribu kuyarudia kukumbuka.




Jisahihishe katika makosa yako na kuwa tayari kuendelea kujiboresha katika ujuzi unaofundishwa au kujifundisha.

Endelea kuwa na mazoezi madogo katika eneo dogo kwani yanaboresha kina cha mazoezi ya kipaji chako na kuongeza uwezo zaidi, na hii imekua inatumiwa na timu mbalimbali ikiwepo timu ya Fc Barcelona.

Moja ya tosheko kihamasa moyoni katika kufanya mazoezi ya ujuzi au kipaji ni pale unapopatia katika kurudia kile ambacho umefundishwa na Mwalimu.

Hili hufananishwa na kitendo cha kujifunza katika kitabu kwa kukifunga kitabu na kusoma kurasa 10 zaidi ya mara 4, Kisha unajaribu kuyarudia kukumbuka.

Kuendeleza Kipaji au ujuzi ni kuchukua Safari ndefu yenye changamoto, mabonde na milima, hamasa na kukata tamaa.

Ila ili uendelee kuwa imara ni muhimu kuwa tayari kukubali vikwazo na kuvishinda.

Njia ya kuendelea kuimarika zaidi katika ujuzi ulioanza nao ni kurudia rudia mara nyingi mpaka uweze kujua kiundani zaidi.

Fikiri kama mtunzaji bustani, na fanya kazi kama seremala, Ukweli upo hivi Kipaji au Ujuzi fulani unakua taratibu kama mimea bustanini.

Na hauwezi shurutisha mmea mdogo ukue kwa haraka.

Nenda kufanyia kazi haya ambayo umeyajua, ukijua kuwa kwa kanuni ya kurudia rudia ndivyo unavyoweza kuwa bora kwa kipaji chako.

Kipaji chako lazima kiweze kunolewa kila siku ili kiweze kukufungulia milango na fursa tele.

Kitakuwa na nguvu pale utakapokifanya mazoezi kwa nidhamu ili kiwe na faida kwako.

Kama wewe ni mwandishi, basi kila siku andika na ndivyo utakavyoweza kuwa mwandishi bora.

Na hivi ndivyo hata maeneo mengine ya maisha utakuwa bora kwa kufanyia mazoezi kila siku kwa unachokifanya.

**Dk. Raymond Nusura Mgeni, ni mchambuzi wa vitabu, anapatikana kupitia simu namba +255 676 559 211 raymondpoet@yahoo.com**



WADAU
**SABATO KASIKA**

# UTOVU wa nidhamu ni moja ya matatizo yanayowakabili baadhi ya wanafunzi, hali inayoweza kusababisha washuke kitaaluma.

Wadau wanasemaje?



**MADINA MUSSA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KITAALUMA mimi ni mwalimu na niseme kwamba kama kuna kitu muhimu katika suala zima la elimu shuleni, basi nidhamu ni jambo la muhimu kwa ajili kufanikisha elimu bora.

Katika mazingira ya shule, nidhamu inahitajika sana si tu wanafunzi kwa walimu wao bali hata walimu kwa wanafunzi wao.


Kikubwa ni kwamba mwanafunzi anahusika sana kuwa na nidhamu ya hali ya juu kwa mwalimu wake, lakini mwalimu naye asipozingatia kuwa pia anahitajika kuwa na nidhamu kwa mwanafunzi wake, anaweza kuwa chanzo kikuu cha kuvuruga ufanisi katika elimu shuleni.

Vilevile nieleweke kwamba mwalimu ana jukumu kubwa la ulezi kuhakikisha anamchukulia mwanafunzi kama mtoto wake katika suala zima la malezi, hivyo asithubutu kufikiria kufanya jambo ambalo ni kinyume cha maadili ya ualimu kwa kuwa yeye ni kioo cha jamii na ni mzazi wa pili.

Kwa ujumla, heshima ambayo mwanafunzi anatakiwa kutoa kwa mzazi wake, ndio hiyo ambayo pia anatakiwa kuionyesha kwa mwalimu wake.

Lakini cha kushangaza hilo halipo tena, mwanafunzi hana adabu na mwalimu naye hana adabu.

Katika mazingira hayo ni heshima kushuka na mwisho wake ndiyo hayo ya mwalimu kumpa mimba mwanafunzi au mwalimu wa kike kujihusisha kimapenzi na mwanafunzi wake. Ushauri wangu, jamii irudi kwenye maadili.



**GODSON MHEMA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KADRI miaka inavyokwenda ndivyo nidhamu inazidi kushuka kwa baadhi ya wanafunzi.

Baadhi ya wazazi wanachangia watoto wao kuwa hivyo, kwani wengine hawana ushirikiano mzuri na walimu katika kumkuza mtoto kinidhamu.

Mwanafunzi anaweza kumtukana mwalimu au kufanya jambo lolote baya kwa mwalimu na anapofika nyumbani anaweza akabadilisha maneno ili mwalimu aonekane ana makosa, halafu mzazi bila kufuatilia ili kujua ukweli, anakwenda kumfokea mwalimu.

Kwa hali kama hiyo ni sawa na kumfanya mtoto awe na kiburi na anaweza kumfanyia mwalimu jambo lolote akijua kuwa mzazi yupo atamtetea, hali inayosababisha heshima ya mwalimu kushuka na hivyo kudharauliwa na mwanafunzi.

Jambo la msingi hapa ni wazazi kushirikiana kwa karibu na walimu ili kuhakikisha watoto wanakuwa na maadili mema wawapo nyumbani na shuleni.

Yaani walimu kwa wazazi siku zote wanatakiwa kusaidiana katika malezi ya wanafunzi kwani wanategemeana kwa ajili ya kuwaendeleza wanafunzi katika suala zima la elimu na nidhamu.

Ushirikiano wa walimu na wazazi utasaidia pia kuepusha wanafunzi kujiingiza katika makundi mabaya yakiwamo ya kuvuta bhangi na dawa za kulevya.



**CHRISTINA GAMA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

VIBOKO shuleni vilikuwa na umuhimu wake, lakini kwa sasa ni kama vipo, havipo kutokana na matamko mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na viongozi wa serikali.

Hali hii kwa kiasi fulani imewafanya baadhi ya wanafunzi wasiwaogope wala kuheshimu walimu wao kwa kuwa wanajua hawawezi kuchapwa.


Yawezekana wapo wanaowatukana walimu na inawezekana wakapewa adhabu ya kusimamishwa masomo kwa siku kadhaa kisha wanarudi shuleni kuendelea na masomo.

Ninaamini kwamba adhabu kama hiyo ya kusimamishwa masomo kwa muda kwa mwanafunzi ambaye hana malengo ya kusoma, haiwezi kumbadilisha na inaweza kumfanya azidi kuwa mbaya zaidi.

Ili kuboresha nidhamu shuleni, sasa ni wakati wa kuwa na wataalam wa ushauri nasaha shuleni ambao jukumu lao litakuwa ni kuwajenga wanafunzi kimaadili.

Hilo likifanyika linaweza kuwaepusha na mambo ya utandawazi ambayo kwa kweli yamechangia kwa kiasi kikubwa kushusha nidhamu kwa baadhi ya wanafunzi kwa mfano kuiga mambo ambayo hayawafai na yanaendana na utamaduni wa kimagharibi.

Hivyo kwa hali kama hiyo wanafunzi hujifunza kuiga utamaduni huo na kusababisha kushuka kwa nidhamu na wakati mwingine kuleta msuguano kati yao na walimu.



**ELIAM MANUMBU (DIWANI MSTAAFU KATA YA MANZESE DAR)**

MOJA ya misingi ya ualimu ni mwalimu kutokuwa na mahusiano ya kimapenzi na mwanafunzi wake, hivyo kitendo cha mwalimu kukiuka msingi huo ni kujitoa katika ualimu moja kwa moja.

Lakini kwa upande mwingine, walimu nao wanachangia sana katika kushuka kwa nidhamu za wanafunzi, kwasababu baadhi ya walimu wanakiuka maadili ya kazi yao kwa kuwaingiza wanafunzi wao katika mambo ambayo ni kinyume na maadili. Kwa mfano mwalimu anafanya mapenzi na mwanafunzi, hivi hapo kutakuwa na nidhamu kweli?

Kama wamesahau, ngoja niwakumbushe kwamba mapenzi ni sumu ya maendeleo ya elimu kwa mwanafunzi, ndio maana kumekuwapo na taarifa kutoka maeneo mbalimbali nchini kwamba walimu wamefikishwa mahakamani kwa kuwapa mimba wanafunzi au kwa kufanya mapenzi na wanafunzi.

Inasikitisha kusikia au kuona mwalimu kama mzazi wa pili anampa mimba mwanafunzi.

Hebu walimu wazingatie maadili ya kazi yao na pia washirikiane na wazazi na walezi kuhakikisha wanafunzi wanakuwa salama shuleni na nyumbani.

Yaani kila mmoja atimize wajibu wake.



**ARAFA NJECHELE (KATIBU WA UWT WILAYA YA NZEGA, TABORA)**

KUSHUKA kwa nidhamu wakati mwingine kunasababishwa na wanafunzi hasa wanaotoka katika familia zenye ukwasi kwa kuwadharau walimu wao.

Wakiwaona kana kwamba si lolote si chochote. Simaanishi wote, lakini baadhi yao wana tabia za aina hiyo. Kitendo cha aina hiyo ni sawa na kushuka kwa nidhamu.

Unaweza kukuta baadhi ya wazazi wanawapa watoto wao kila kitu, hali inayowafanya wajione wameyapatia maisha hivyo hawawezi kuwa na heshima na wanawaona watu wengine wakiwamo walimu si lolote kwao. Wenye tabia hii wanatakiwa kuelimishwa.

Hapa ninamaana kuwa elimu ya malezi itolewe kwa wazazi na wanafunzi ili watambue madhara ya kushuka kwa nidhamu na pia watambue kwamba mwanafunzi bora anapaswa kuwa na nidhamu kwani ndio moja ya sifa inayoweza kumfanya apendwe na walimu wake na hivyo kufanikiwa zaidi kwenye masomo yake.

Kama mwanafunzi hana nidhamu shuleni, basi hata nyumbani kwao yuko hivyo na atakuwa kero kwa walimu na wazazi wasiopenda tabia hiyo.

Kwa mzazi au mlezi anayetambua kuwa elimu ni nyenzo muhimu katika maisha ya binadamu, atakuwa tayari kufanya kila njia kuhakikisha mtoto wake anakuwa na nidhamu kuanzia nyumbani, shuleni hadi kwa jamii inayomzunguka.



# Jamii yashauriwa ufugaji samaki

**Na Mwandishi Wetu,** RUNGWE

JAMII imeshauriwa kuchangamkia fursa ya ufugaji samaki kama jitihada za kuboresha upatikanaji wa lishe, maendeleo ya viwanda, pamoja na kujiongezea kipato.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Shamba Samaki, lililopo katika Kata ya Kiwira Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Kenny Nyambacha, ambapo alisema ufugaji wa samaki una faida kubwa ukilinganisha na ufugaji kuku pamoja na mazao mengine ya biashara.

Kenny alisema ametengeneza zaidi ya mabwawa 20 kwa ajili ya uzalishaji wa samaki na kwamba ndoto yake kubwa ni kuzalisha samaki wengi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi ili kuliingizia taifa fedha za kigeni.

"Ufugaji wa samaki kwa sasa ni dili kubwa kwa kuwa uhitaji ni mkubwa mbali na kutumia kama chakula, lakini kwa sasa tunaweza kusafirisha kupeleka mataifa mengine kuuza, nawashauri wananchi wenzangu kuchangamkia fursa hii, natamani kunufaika zaidi na mipango yangu ni kufungua kiwanda cha kuchakata samaki," alisema Kenny.

Kenny alisema kwa sasa amezalisha zaidi ya vifaranga 100,000 na kwamba wakazi wanaozunguka eneo hilo walijengewa uwezo wa namna ya ufugaji bora wa samaki.

Alisema kuwa mafunzo hayo yalikuwa ni chachu kwa jamii kwa kuwa yatawasaidia kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kuongeza kipato.

Aliongeza kuwa shamba hilo la mradi wa samaki limesaidia ajira kwa wanawake na vijana na pia eneo hilo linatumika kama sehemu ya kukuza shughuli za utalii wa ndani kwa wageni wanaofika kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania.

**Ufugaji wa samaki kwa sasa ni dili kubwa kwa kuwa uhitaji ni mkubwa mbali na kutumia kama chakula, lakini kwa sasa tunaweza kusafirisha kupeleka mataifa mengine kuuza, nawashauri wananchi wenzangu kuchangamkia fursa hii, natamani kunufaika zaidi na mipango yangu ni kufungua kiwanda cha kuchakata samaki.**

# CCM sasa yaelekeza kupalilia makaburi kuenzi marehemu

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mbeya Mjini kimeelekeza uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuweka utaratibu wa kufanya usafi maeneo ya makaburi kama njia ya kuwaenzi marehemu.

Agizo hilo lilitolewa na Katibu wa CCM Mbeya Mjini, Gervas Ndaki, wakati wa zoezi la kufanya usafi kwenye makaburi ya Sabasaba jijini Mbeya, ambapo alisema ni zaidi ya miaka mitano sasa eneo hilo halijafanyiwa usafi.

Kutokana na hali hiyo CCM katika kuadhimisha Wiki ya Wazazi waliamua kufanya usafi kwenye maeneo hayo ikiwa ni njia ya kuwaenzi marehemu na kuweka mji kuwa safi.

Alisema katika maadhimisho hayo jumla ya wanachama 200 walishiriki zoezi la kufanya usafi katika makaburi hayo.

**Jumuiya ya Chama Cha Mapinduzi kupitia Idara ya Mazingira inaelekeza kuwa kila mwanachama anatakiwa kulichukulia suala la usafi wa mazingira kama agenda namba moja.**

Ndaki alisema kitendo cha Halmashauri ya Jiji kushindwa kufanya usafi kwenye maeneo ya makaburi ikiwamo Sabasaba, Nzovwe na Loleza sio cha kiungwana na kwamba wameelekeza nguvu kwenye maeneo mengine na kusahau eneo muhimu kama makaburi.

"Tunaielekeza Halmashauri ya Jiji kufanya usafi katika maeneo haya kwa sababu ni miaka mingi usafi haujafanyika, lazima watambue kuwa moja ya kigezo kitakachowapa hati safi ya usafi ni kusafisha makaburi, chama kimeonyesha mfano kwa kufyeka mapori yote ndani ya makaburi haya sasa ni zamu yao kufanya usafi wa mara kwa mara," alisema Ndaki.

Kaimu Katibu wa Jumuiya ya Wazazi wa CCM, Mbeya Mjini, Islam Iddy, alisema wameamua kufanya usafi kwenye makaburi ya Sabasaba kwa sababu eneo hilo lilikuwa ni pori kubwa.

Alisema pori hilo lingeweza kuhifadhi wahalifu kama vile wabakaji, wezi na watumiaji wa dawa za kulevya pamoja na wadudu hatari ikiwamo nyoka.

"Jumuiya ya Chama Cha Mapinduzi kupitia Idara ya Mazingira inaelekeza kuwa kila mwanachama anatakiwa kulichukulia suala la usafi wa mazingira kama agenda namba moja," alisema Iddy.

Akizungumzia suala hilo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Gregory Emmanuel ambaye alishiriki katika zoezi la usafi katika makaburi ya Sabasaba, alikiri jiji kutofanya usafi katika eneo hilo.

Alikishukuru Chama Cha Mapinduzi kwa kufanya usafi katika makaburi hayo na kwamba Halmashauri ya Jiji itaandaa utaratibu wa kufanya usafi katika makaburi yote ya umma na kuwaomba wananchi nao kujenga utamaduni wa kufanya usafi kwenye makaburi ya ndugu zao.




Mkurugenzi Kitengo cha Mauzo ya Fedha za Kigeni wa Benki ya Barclays Tanzania, Esther Maruma (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa kituo cha kubadilishia fedha za kigeni cha benki hiyo. Kushoto ni Mkuu wa Masoko na Mawasiliano, Aron Luhanga na Mkuu wa Wateja Binafsi, Oscar Mwamfwagasi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Utafiti wagundua mbegu mpya za pareto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KITUO cha Utafiti wa Kilimo TARI - Uyole kimegundua mbegu mpya saba za zao la pareto ambazo mkulima akizitumia anaweza kuzalisha kati ya kilo 800 hadi 1,200 kwa hekta na hivyo kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Akizungumza na Nipashe juzi, mtafiti wa zao la pareto kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo TARI- Uyole kilichopo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Lucas Nzilamo, ambaye pia ni Mratibu wa Utafiti wa zao hilo nchini alisema mbegu hizo zitamsaidia mkulima kuongeza uzalishaji.

Nzilamo alisema mbegu hizo saba za zao la pareto zina viuatilifu kwa wingi, ambapo zimependekezwa na zinasubiri kupasishwa, huku akidai kuwa pareto ya Tanzania ina ubora kwa kuwa uchumaji wake unatumia mikono.

Alisema pareto ya Tanzania ni bora kwa sababu mkulima anachagua ua ambalo linafaa tofauti na mataifa mengine ambayo yanatumia mashine wakati wa uvunaji, hivyo kuvuna hata maua ambayo hayastahili kuvunwa.

"Lengo la utafiti wetu ni kuhakikisha mkulima anatumia mbegu bora ambazo zinakidhi mahitaji ya udongo katika maeneo husika, lakini pia kuongeza tija katika mazao, tumefanikiwa katika utafiti wetu kwani tumeshuhudia wakulima wanaofuata ushauri wetu kunufaika," alisema Nzilamo.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kituo hicho kimeendelea kufanya utafiti na kuzalisha mbegu mbalimbali za mazao ya nafaka ikiwamo jamii ya mikunde na mizizi.

Alisema mbegu zinazoendelea kubuniwa katika kituo hicho zinawanufaisha wakulima kwa sababu ni bora na zinaongeza uzalishaji.





# Uchaguzi mitaa kwa kanuni mpya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI uchaguzi wa serikali za mitaa 2019, ukitarajiwa kufanyika Novemba mwaka huu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) imewataka wadau wa vyama vya siasa kutoa maoni yenye tija kwa ajili ya rasimu za kanuni mpya za uchaguzi huo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tamisemi, Selemani Jafo, katika kikao kazi cha kupitia rasimu za kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019, jijini hapa.

Kikao hicho cha siku mbili kimekutanisha wadau wa vyama vya siasa, ikiwamo Baraza la Vyama vya Siasa, Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Uchaguzi na wizara mbalimbali.

Akifungua kikao hicho, Jafo alitaja rasimu tatu ambazo wadau hao watazijadili kuwa ni pamoja na rasimu ya kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji na mwenyekiti wa kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za mwaka 2019.

**Tuna imani nyie wadau wa vyama vya siasa mtatoa maoni yenye tija ili kutengeneza kanuni zilizo bora zitakazosimamia uchaguzi wa serikali za mitaa, uchaguzi huu unatarajia kufanyika muda wote Novemba mwaka huu.**

Ametaja rasimu zingine kuwa ni ya uchaguzi wa mwenyekiti wa mtaa na wajumbe wake, katika Mamlaka za Miji za mwaka 2019 na rasimu ya kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo za mwaka 2019.

"Tuna imani nyie wadau wa vyama vya siasa mtatoa maoni yenye tija ili kutengeneza kanuni zilizo bora zitakazosimamia uchaguzi wa serikali za mitaa, uchaguzi huu unatarajia kufanyika muda wote Novemba mwaka huu," alisema.

Alisema Tanzania inaongozwa kwa utaratibu wa demokrasia, hivyo serikali iliona ni vyema kutengeneza jukwaa la kuwakutanisha wadau mbalimbali wakiwamo vyama vya siasa ili kuwa na kanuni bora zitakazoendesha uchaguzi kwa amani na utulivu.

"Niliona siyo vyema kwa mujibu wa utaratibu wa uundwaji wa kanuni hizi lazima tuunde kanuni ambazo zinamchango mkubwa wa wadau mbalimbali ambao utasaidia sana katika mwenendo wa uchaguzi tunaoendana nao," alisema.

Jafo alisema wapo tayari kupokea maoni ya wadau hao kwa kuwa ni kundi muhimu kwenye uundwaji wa kanuni za uchaguzi.

Kadhalika, aliagiza ofisi yake kuhakikisha inawapatia mapema wadau kanuni hizo kwa kuwa wakati mwingine wamekuwa wakizitoa ukumbini.

"Inakuwa siyo jambo jema sana na inakuwa kama ni jambo la kuviziana, hili ni jambo letu sote kwa ajili ya nchi yetu, mapema kupata ushauri mzuri ulio bora na kanuni ziwe nzuri na imara ili kuweza kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa kwa uzuri," alisema.

Aliwataka kuhakikisha taifa linakuwa na kanuni za bora kwa kuwa maoni yao yatakayopendekezwa yatakuza demokrasia na utawala bora.

Aliahidi kuwa serikali itazingatia maoni yao ili kanuni hizo ziweze kuleta tija na ufanisi kwenye uchaguzi.

Jafo alisema utii wa sheria za nchi, kanuni na taratibu za uchaguzi ndiyo msingi wa uchaguzi ulio wa haki na wenye kuzingatia ushiriki wa makundi yote ya jamii.

"Vyama vya siasa vina wajibu wa kuwaelimisha na kuwaelekeza wagombea, wafuasi na wanachama wao kuzingatia matakwa ya sheria za nchi na kanuni hizi za uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, John Shibuda, alisema watahakikisha wanatengeneza kanuni zitakazojenga taswira nzuri ya nchi kitaifa na kimataifa.

Aliomba katika kikao hicho, Msajili wa Vyama vya Siasa kutoa uwianishaji wa kanuni hizo pamoja na sheria mpya ya vyama vya siasa ili isilete msuguano wakati wa uchaguzi huo.

"Ili kuondokana na dukuduku na sintofahamu kuwapo uwianishaji wa sheria ya vyama vya siasa na kanuni hizi za uchaguzi, tuongeze muda wa majadiliano uwe siku tatu ili tumsikie msajili anasemaje kwenye hili ili isitokee misuguano," alisema.



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, akitoa ufafanuzi kuhusu ukaguzi wa maduka ya ubadilishaji fedha za kigeni kwenye mkutano wa waandishi wa habari na Waziri wa Fedha uliofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wasiosikia watakiwa kubuni miradi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

UONGOZI wa Chama cha Viziwi Tanzania Mkoa wa Dodoma (CHAVITA), umewataka wanachama wake kubuni miradi itakayowawezesha kuondokana na utegemezi wa wahisani.

Wito huo ulitolewa jana na mwenyekiti wa chama hicho mkoani Dodoma, Yusufu Mloli, katika mkutano wa uchaguzi wa chama hicho, jijini hapa.

Alisema wanachama wanatakiwa kuunda vikundi vya ujasiriamali ili waweze kupatiwa mikopo itakayoweza kujikwamua kiuchumi.

Aidha, mwenyekiti huyo alisema kuwa kutokana na changamoto zilizopo kwa watu wenye ulemavu kwa upande wa viziwi mkoa wa Dodoma, utahakikisha unawahamasisha wanachama hao kufanya kazi kwa bidii.

Alisema miongoni mwa makundi ambayo yamekuwa na changamoto ya kujikwamua kiuchumi ni watu wenye ulemavu, hivyo chama hicho kitahakikisha wanachama wanajiunga na vikundi vya ujasiriamali kwa malengo ya kuwaletea maendeleo wao wenyewe na waondokane na tabia ya utegemezi.

Aidha, pamoja na changamoto hiyo ya watu wenye ulemavu uongozi huo utahakikisha unasimamia suala la upatikanaji wa ajira kwa kuishawishi serikali na halmashauri zake kutoa nafasi za ajira kwa wale walemavu wenye sifa.

"Tunapenda kuwahakikishia kuwa uongozi huu ambao mmeuchagua wenyewe tutafanya kazi kwa kushirikiana kwa pamoja kati yenu na sisi katika kuhakikisha upatikanaji wa ajira na mikopo inatolewa ili hizi changamoto tunazotukabili zinatatuliwa," alisema.

Awali, aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho, Mazengo Kusenha, aliwataka wanachama hao kutoa ushirikiano ili waweze kufikia malengo ya chama kwenye eneo la kielimu na kiafya.

# Halmashauri 12 kufikiwa mawasiliano vijijini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inatarajia kujenga mkongo wa taifa katika halmashauri 12 ili kufikisha huduma za mawasiliano vijijini kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Isack Kamwele, jijini hapa.

Alitaja halmashauri hizo kuwa ni Jiji la Dodoma, Mwanza, Manispaa ya Moshi, Tanga, Shinyanga, Mji wa Kibaha, Chamwino, Bahi, Geita, Chato, Kibaha na Ilemela.

Aidha, alisema serikali imetoa ruzuku kwa kampuni za simu ili ziendelee kufikisha huduma za mawasiliano vijijini na maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara.

Waziri huyo alisema mawasiliano yakisogezwa vijijini yatasaidia vijiji hivyo kuinuka kibiashara ikiwamo kufanya shughuli mbalimbali.

"Mpaka sasa kuna minara 530 imejengwa nchini na kiu yetu ni kuhakikisha kila sehemu mawasiliano yanapatikana," alisema.

Alibainisha serikali inaendelea kuhamasisha matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano ili kuona watu wanakwenda na wakati ili Tanzania ipige hatua kiuchumi.

Aliagiza kila mwananchi atumie mtandao kwa usahihi na si matumizi mengine ambayo hayatakuwa na faida.

Aliwataka wafanyakazi wa sekta hiyo kuzingatia utendaji kazi wao kutokana na kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa wananchi kwa ajili ya kupata mawasiliano.



# Waziri atoa neno migogoro ya waajiri, wafanyakazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Cyrus Castico, amewataka wafanyakazi na waajiri kuepukana na migogoro sehemu za kazi ili kuleta ufanisi na kukuza uchumi wa nchi.

Akifungua mkutano mkuu wa chama cha wafanyakazi wa viwanda, biashara, taasisi za fedha na huduma na ushauri, alisema ili kufikia maendeleo ni lazima kuwapo ushirikiano baina ya mwajiri na mwajiriwa.

**Lengo la kuwapo vyama vya wafanyakazi ni kupata umoja madhubuti utakaoweza kutetea maslahi yao.**

Aliwataka kutumia hekima na maarifa katika kuchagua viongozi wazalendo watakaosimamia vyema chama chao ili weweze kufikia malengo waliokusudia.

Aidha, aliwataka viongozi waliochaguliwa kufanya kazi kwa kujitolea, kuangalia maslahi ya wafanyakzi, kuacha ubaguzi na rushwa.

"Kama mtaendekeza ubaguzi, hamtoweza kufika mbele wala kupata maendeleo, hivyo ni vyema kila mmoja kwa nafasi yake kuwa balozi mzuri wa mweziwe," alisema Castico.

Alieleza kuwa rushwa ni adui mkubwa wa haki hivyo ni vyema kutoipa nafasi ili haki iweze kupatikana kwa kila mmoja.

Naye Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC), Khamisi Mwinyi Mohammed, alisema lengo la kuwapo vyama vya wafanyakazi ni kupata umoja madhubuti utakaoweza kutetea maslahi yao.

Aidha, alisema chama hicho kimejipanga kuhakikisha inapata viongozi madhubuti kwa vyama vichache vilivyopo kuliko kuwa na utitiri wa vyama usiokuwa na mpango wowote.



Wasamaria wema wakimsaidia mwendesha bodaboda kunyanyua gunia la mkaa na pikipiki baada ya kuanguka katika eneo la Mbezi Mwisho, kutokana na utelezi uliosababishwa na mvua iliyonyesha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wajasiriamali wawekewa mikakati kuwakomboa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Ajira Zanzibar, Ali Suleiman Ameir, amesema serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuwanyanyua kiuchumi wajasiriamali katika maeneo yao.

Aliyasema hayo katika uwanja wa Kisonge wakati akifunga maonyesho ya kwanza ya kazi za wajasiriamali yaliyoandaliwa na mtandao wa tamaduni za kijamii Zanzibar.

Alisema kuanzishwa kwa mfuko wa uwezeshaji, idara ya programu za uwezeshaji na vituo vya kuwaendeleza wajasiriamali kumesaidia baadhi ya wananchi hususani vijana kupata mbinu mbadala za kujiajiri.

Aidha, aliwataka wajasiriamali hao kutovunjika moyo kutokana na matatizo madogo madogo yanayojitokeza na badala yake wazidishe juhudi ili kuweza kufikia malengo waliojipangia ya kujikomboa na tatizo la umaskini linalowakabili wananchi.

Naye Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Omar Said Ameir, aliwashauri wamiliki wa vyombo vya habari Zanzibar kuwaunga mkono wajasiriamali kwa kuzitangaza bidhaa wanazozalisha ili ziweze kufahamika na kupata soko la uhakikia la ndani na nje ya nchi.

Aliitaka jamii kuwa na utamaduni wa kuthamini bidhaa zinazotengenezwa na wazawa kuliko kupenda bidhaa kutoka nje ya nchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mtandao wa Tamaduni za Kijamii Zanzibar, Ameir Abdallah Ameir, alisema wajasiriamali wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo uhaba wa fedha, vifungashio na uhaba wa masoko.

# Rc atangaza vita vitendo vya udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Ayoub Muhamed Mahmoud, ameitaka jamii kushirikiana na serikali katika kupambana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia na wizi wa watoto ambao umeanza kujitokeza visiwani Zanzibar.

Alisema jamii sasa inatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kuripoti matendo hayo ili serikali iweze kuchukua hatua za haraka.

Ayoub aliyasema katika kongamano la kupiga vita udhalilishaji na wizi wa watoto lililoandaliwa na Umoja wa Wanawake (UWT) Jimbo la Mwanakwerekwe.

Alisema ili kuondokana na matendo hayo ambayo kwa sasa yamekuwa yakijitokeza katika baadhi ya mitaa, ni vyema wananchi kuwa na mwamko wa kuripoti taarifa hizo ili serikali ichukue hatua kwa wakati.

Aliongeza kuwa huu si wakati wa kufumbia macho matendo hayo na kuwataka kuwafichua wale wote watakaobainika wanahusika na kufanya vitendo hivyo viovu.

"Mimi nataka niwaambie kuwa tusiwe nyuma katika kuripoti matukio haya katika sehemu zinazostahiki, tuseme hata kama wanaofanya ni viongozi maana tuna taarifa kuwa baadhi ya viongozi wakubwa wao ndio wafanyaji na wachochezi wa matendo haya," alisema Mkuu wa Mkoa huyo.

Aidha, alieleza kuwa kuna baadhi ya viongozi wengine wapo ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), lakini maneno yao na matendo yao hayafanani na dhamana walizonazo kwa kuwa baadhi yao ndiyo wachochezi wa vitendo vya udhalilishaji ndani ya mkoa huo.

Alisema kuwa kwa kiongozi yoyote atakae bainika kuhusika na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na wizi wa watoto hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

"Mimi huwa nasema kwa kinywa kipana, ndani ya mkoa huu hakuna aliyekuwa juu ya sheria kwa yeyote atakayefanya vitendo hivi awe kiongozi yupo ndani ya CCM au nje ya CCM hatutosita kumchukulia hatua dhidi yake," alisema.

Mkuu huyo alitoa wito kwa jumuiya hiyo ya wanawake kurudi katika malezi ya asili yenye silka na utamaduni wa Kizanzibar ili kuwa na jamii bora.

Alisema malezi ya pamoja ndio suluhisho la vitendo vya udhalilishaji, ambapo mzazi kuwa karibu na watoto kufuatilia nyendo zake na kumsimamia vyema katika suala zima la malezi.

Alieleza kufanya hivyo kutasaidia kupunguza uwezekano wa kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kuwalinda watoto dhidi ya vitendo hivyo.

Naye Katibu wa UWT Jimbo la Mwanakwerekwe, Rehema Kondo Kombo, alieleza lengo la kuandaa kongamano hilo ni kupaza sauti zao juu ya matendo hayo ya udhalilishaji ambayo kila siku yanaongezeka ndani ya visiwa vya Zanzibar.

"Tumeamua kupiga vita na kupaza sauti zetu ambapo kwa pamoja tunaweza kuondokana na janga hili ambalo linalitafuna taifa letu," alisema katibu huyo.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 01 April**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 02 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 203 April**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 04 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 05 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 06 April**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Dead silence
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 07 April**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 01 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
21:55 Kipindi Maalum: True Vision
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 02 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum: True Vision
21:05 Kipindi Maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 03 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Uongozi
21:40 Kipindi Maalum : Tanesco
22:05 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 04 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Kesho leo rpt
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi Maalum rpt: Uongozi
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 05 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 06 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 07 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters 2
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Magic house
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)

## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |


EATV
NIRVANA
LEO USIKU SAA 3:00



JUMANNE
11:00 DADAZ (live)
13:30 Kali Za Wana
14:00 Dakika10 Za Maangamizi
15:00 FUNGUKA
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Nirvana
21:30 Wakilisha
22:00 Grace Na Asili Yangu
22:30 Bongo Hits

NIRVANA ni kipindi cha kisasa kinachoongelea mitindo, sanaa, urembo na staili za maisha. NIRVANA inawalenga wale wanao ongoza kuonyesha mitindo mipya kwenye jamii na wale wanaofuatilia

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise
88.1FM DAR ES SALAAM


## CAPITAL RADIO

**CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM**
**FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE**

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

HABARI KIMATAIFA

# Rais wa Afrika Kusini ashutumu mashambulizi dhidi ya wageni

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

RAIS wa Afrika Kusini, Cryril Ramaphosa, ameshtumu ghasia zilizotokea hivi karibuni za mashambulizi dhidi ya wageni, na kutoa wito kwa taasisi za kiusalama kuwakamata wanaotekeleza vitendo hivyo.

Amesema kuwa ghasia hizo, ambazo zimekuwa zikiwalenga raia wa Malawi na raia wengine kutoka nchi za Afrika katika jimbo la Kwazulu Natal ni suala la kujutia hususan katika mkesha wa siku ya uhuru, ambapo taifa hilo linaadhimisha miaka 25 tangu uchaguzi wa kidemokrasia ufanyike nchini humo.

Wiki iliopita, idadi kubwa ya wananchi walilazimika kuzikimbia nyumba zao baada ya waandamanaji waliojawa na hasira kuwavamia na kuwaibia.

"Leo uchumi wetu na faida za jamii yetu zinatokana biashara na uwekezaji kutoka kwa washirika wetu katika bara Afrika na wengi wanaishi hapa Afrika Kusini, wanachangia sana maendeleo ya taifa hili. Maendeleo ya Afrika yanatokana na ongezeko la watu na ufanyaji wa biashara kutoka eneo moja hadi jingine kati ya mataifa tofauti ili sote tuweze kufaidika. Hatutakubali kuaawacha wahalifu kurudisha nyuma hatua zilizopigwa," alisema Ramaphosa.

Kutokana na hali hiyo, Waziri wa masuala ya kigeni nchini Afrika Kusini aliitisha mkutano wa dharura na mabalozi waliopo nchini humo, baada ya kutokea kwa mashambulizi dhidi ya wageni mjini Durban.

Jumatatu wiki iliyopita watu watatu walifariki kufuatia maandamano yanayolenga maduka ambayo yanamilikiwa na wageni.

Kutokana na maandamano hayo, Takriban watu 50 walitafuta hifadhi katika kituo kimoja cha polisi wakati kundi la vijana wa Afrika wasio na kazi walipowashinikiza kutoka katika majumba yao usiku.

**BBC**



Rais wa Rwanda, Paul Kagame, akiwasha Mwenge wa kumbukumbu ya mauaji ya Kigali, wakati wa maadhimisho ya mauaji ya halaiki yaliyotokea Rwanda mwaka 1994. **PICHA AFP**

## Rwanda yaanza maandalizi kukumbuka mauaji ya kimbari

**KIGALI,** Rwanda

RWANDA imeanza kuadhimisha wiki mahsusi ya maadhimisho ya kumbukumbu ya mauaji ya kimbari yaliyogharimu maisha ya watu 800,000 kutoka kabila la Watutsi na Wahutu mnamo mwaka 1994.

Ni miaka 25 imepita tangu kutokea kwa mauaji hayo mabaya yaliyobadilisha historia ya nchi hiyo tungu uhuru wake mnamo Julai 1962 ilipotawaliwa na watu kutoka kabila la Wahutu.

Kipindi hiki kinafanyika kama Umuganda, na ni juma linaloleta huzuni na matumaini kwa wakati mmoja kwa nchi ya Rwanda.

Mauaji hayo yalifanyika nchini humo isipokuwa wilaya moja tu ya Giti kaskazini magharibi mwa nchi hiyo.

Sababu ya wilaya hiyo kutoshuhudia mauaji ya kimbari ni mshikamano baina ya wananchi na uongozi uliosimama na kupinga kila aina ya uonevu uliokuwa unatokea nchini humo.

Watutsi kwa wahutu wanamsifu aliyekuwa kiongozi wao nyakati hizo, kutoruhusu propaganda za chuki na mauaji.

Aliyekuwa kiongozi wa wilaya hiyo ni Sebushumba Edouard, ambaye kwa sasa ni mzee aliyestaafu.

Mwaka 1996 kiongozi huyo mstaafu alikuwa miongoni mwa watu waliotunukiwa medali za heshima kutokana na juhudi zao za kulinda raia wakati wa mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi.

Katika siku 100 mnamo mwaka 1994, watu 800,000 waliuawa kikatili nchini Rwanda. Mauji hayo yalifanywa na wahutu wenye msimamo mkali.

**RFI**

## Rais Bouteflika wa Algeria kujiuzulu muda wowote

**ALGERS**, Algeria

TAARIFA kutoka nchini Algeria zimeeleza kuwa Rais wa nchi hiyo, Abdelaziz Bouteflika huenda akajiuzulu wiki hii.

Vituo viwili vya televisheni vinavyomilikiwa na watu binafsi Ennahar na El Bilad vilitangaza kuwa kuna uwezekano Rais Bouteflika akajiuzulu wiki hii kufuatia maandamano ya umma na shinikizo la jeshi kumtaka asitishe utawala wake wa miaka 20.

Taarifa hizo zimetangazwa baada ya Mkuu wa Vikosi vya Wanajenshi, Luteni Jenerali Ahmed Gaid Salah kulitaka kwa mara nyingine tena baraza la katiba limtangaze Rais Bouteflika mwenye umri wa miaka 82 kuwa hawezi kutawala.

Hata hivyo, Vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali havikutangaza ripoti kuhusu uwezekano wa kujiuzulu kwa rais huyo mkongwe kuliko wote Afrika, wala hakuna jibu lolote lililotolewa na ofisi ya rais.

Kituo cha Ennahar kilitangaza kuwa Rais Bouteflika anajiandaa kustaafu kuambatana na kifungu namba 102 cha katiba kinachomruhusu kuacha madaraka au kukabiliana na uamuzi wa baraza la katiba kama hana uwezo.

Taarifa hizo zimetangazwa saa chache baada ya Rais Bouteflika kuliteua baraza jipya la mawaziri. Duru za kisiasa zinasema huenda hiyo ni ishara kwamba pengine Bouteflika atang'atuka.

Waziri Mkuu wa Algeria, Noureddine Bedoui, ataliongoza baraza hilo la mawaziri 27. Mkuu wa vikosi vya wanajeshi Jenerali Ahmed Gaid Salah, amekabidhiwa wadhifa wa Naibu Waziri wa Ulinzi akiwa nafasi ya pili kiitifaki nyuma ya waziri mkuu Bedoui.

Wizara ya ulinzi anaiongoza mwenyewe Rais Bouteflika ambaye kikatiba ndiye kiongozi mkuu wa vikosi vya wanajeshi.

Hata hivyo, Ramtane Lamamra ambae marchi 11 aliteuliwa kuwa makamo waziri mkuu na waziri wa mambo ya nchi za nje hakutajwa katika baraza hilo jipya.

Licha ya mabadiliko hayo ya serikali maelfu ya wananchi wanaendelea kumiminika mjini Algiers na kupaza sauti kumtaka Rais Bouteflika ang'atuke.

Wanaharakati hao wameshangiliwa na watu waliokuwa ndani ya magari na kupiga honi njiani.

**DW**

## Viongozi nchi za Kiarabu waupinga uamuzi wa Trump

**TUNIS,** Tunisia

VIONGOZI wa jumuiya ya nchi za Kiarabu katika mkutano wao wa kilele uliofanyika mjini Tunis siku ya Jumapili, wameupinga kwa kauli moja uamuzi wa Marekani, Donald Trump wa kuitambua milima ya Golan kama sehemu ya Israeli.

Katika tamko la mwisho walilolitoa baada ya mkutano wao wa kilele kumalizika, viongozi hao wa Umoja wa Kiarabu walisisitiza kuwa milima ya Golan inayokaliwa na Israel ni eneo la Syria kulingana na sheria ya kimataifa, maamuzi ya Umoja wa Mataifa na ya Baraza la Usalama.

Katibu Mkuu wa jumuiya hiyo, Ahmed Aboul Gheit alisema hoja ya Rais Trump ni batili, sio halali kabisa.

Rais Trump alitia saini tamko la kuitambua milima ya Golan kuwa ni sehemu ya Israel wiki iliyopita.

Israel iliiteka milima ya Golan wakati wa vita vya mwaka 1967 vya mashariki ya kati baada ya Syria kuitumia sehemu hiyo yenye umuhimu wa kijeshi, kwa ajili ya kushambulia sehemu za kaskazini mwa Israel.

Israel ililiunganisha eneo hilo katika miliki yake mnamo mwaka 1981.

Kwa muda wa miaka mingi nchi za kiarabu zimekuwa zikitaka eneo hilo la milima lirudishwe na zimeulaani uamuzi wa Rais Trump wa kuitambua milima hiyo kuwa ni sehemu ya ardhi ya Israel.

Viongozi hao walisema kuwa watawasilisha azimio kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa dhidi ya uamuzi wa Marekani, pia wameahidi kuwaunga mkono Wapalestina katika jitihada zao za kutaka uhuru wao.

Syria haikuwakilishwa katika mkutano huo kutokana na kusimamishwa uanachama wake tangu mwaka 2011 na hadi mkutano huo wa kilele ulipomalizika viongozi wa jumuiya hiyo ya nchi za kiarabu hawakuwa wamefikia makubaliano juu ya kuiruhusu Syria kurejea kwenye jumuiya hiyo.

**DW**

# Maalim Seif ajiweka kando madeni CUF

**Na Romana Mallya**

ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), ambaye amehamia ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema hahusiki na madeni ya CUF kwa namna yoyote ile.

Maalim Seif aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akihojiwa kwenye kipindi cha asubuhi cha 360 Clouds FM, ambapo alisema hawezi kuwajibika kwa namna yoyote kwenye madeni ya CUF kwa sababu alishajivua kwa barua.

Alisema alimwandikia barua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kumjulisha kuwa hata wajibika kwa namna yoyote kwa sababu Msajili wa Vyama vya Siasa, alianza kutoa fedha za chama upande wa Prof. Ibrahim Lipumba.

"Nilimwandikia kumjulisha kuwa mimi ndiyo mhasibu wa mahesabu ya chama, lakini zipo fedha zinaingia sina habari nazo, nilimweleza kuanzia wakati huo najivua. Nilimjulisha kuwa fedha zinazoingia atajuana na wanaolipwa fedha hizo," alisema.

Maalim Seif alidai baada ya Msajili kuutambua upande wa Prof. Lipumba, ulivamia ofisi na hawajui walichukua nini.

"Hatujui wenzetu walichukua nini kwa sababu mahesabu tuliyokuwa nayo na mkurugenzi wa fedha, hatuna kwa sababu tuliyaacha ofisini," alisema.

**AMSHUTUMU MSAJILI**

Maalim Seif alidai kuwa baada ya kuondoka CUF kama wangeamua kuunda chama, Msajili asingetoa usajili wake.

"Namsema Msajili kwa sababu ya matendo aliyonifanyia, huyu ni kama vile ana majukumu kapewa kuhakikisha ananikata mbawa, angalia maamuzi yake aliyochukua kumrejesha Prof. Lipumba.

"Msajili alikata ruzuku za chama nikamwandikia barua, mbona umezuia ruzuku yetu, akanijibu kimaandishi kwamba amezuia kwa sababu tuna mgogoro, ukimalizika watatupa na kwamba fedha zetu wanaziweka," alisema.

Aliongeza kuwa, "Wakati Msajili akitujibu hivyo, papo hapo alikuwa akimpa fedha Prof. Lipumba ruzuku ile ile ya chama, tena kwa taratibu ambazo sizo ambazo zimewekwa kisheria na kikanuni," alisema.

Hivyo alisema waliona hakuna sababu ya kuanzisha chama kipya wakati upo uwezekano wa kujiunga vyama vingine.

Mtangazaji alipomuuliza Maalim Seif kama akipata fursa ya kukutana na Msajili angemuuliza swali gani, alijibu kwa kusema, "Ningemuuliza je, ulichokifanya ni haki?"

Kuhusu uamuzi wa kwenda ACT-Wazalendo, Maalim Seif alisema haukuwa wa ghafla bali wiki nne kabla ya uamuzi wa mahakama kutoka waliona maandishi ukutani ambayo yalionyesha hakuna uwezekano wa wao kupewa chama.

"Baada ya maandishi yale tukajitayarisha kwa kusema ikitokea hivyo tufanye nini, tulikuwa tumeshajua nini tutafanya, wiki mbili kabla ya uamuzi wa mahakama kutoka nilifanya ziara visiwani na Dar es Salaam kuwatahadharisha kuwa kuna dalili hizi kwamba wanataka kutunyang'anya chama, lakini niliwaambia wasijali," alisema.

Maalim Seif alisema aliwaeleza wanachama kuwa endapo watanyang'anywa chama, bado wao ni washindi na kwamba watachukua hatua ambazo upande wa pili watajuta.



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kampuni ya mafuta na gesi ya Equinor Tanzania, Genevieve Kasanga, akichangia mada inayohusu kitalu namba mbili cha mradi wa gesi Bahari Kuu, wakati wa warsha ya kuhusu rasilimali watu iliyoendeshwa na kampuni hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Ashauri Precision Air kuzitumia fursa Dodoma

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amelitaka Shirika la Ndege la Precision Air kutumia fursa ya kujengwa kwa uwanja wa ndege wa kisasa eneo la Msalato wenye ukubwa zaidi ya kilometa tatu, kupeleka ndege kubwa za kusafirisha abiria wanaoingia na kutoka.

Katambi alitoa wito huo jana, wakati akizindua safari ya kwanza ya ndege ya Precision Air kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma na Kilimanjaro kwenda Dodoma na kutoa huduma za usafiri kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi mara tatu kwa siku.

Katambi alisema uwanja wa ndege wa Msalato umetengewa Sh. bilioni 200 na tayari Sh. bilioni 3.5 zimetumika kulipa fidia kwa wakazi wa maeneo hayo na ujenzi utakapoanza na kukamilika ndege kubwa zitaanza kutua.

"Niwapongeze Precision Air kwa kuona fursa hii ya kusafirisha abiria wanaokuja katika jiji hili, mmefanya jambo kubwa na linalohamasisha maendeleo katika nchi yetu. Niwasihi tu mtuletee ndege kubwa zaidi ambazo zitasafirisha abiria wengi kwa sababu tumeshaanza mchakato wa ujenzi wa uwanja wa ndege mkubwa na kisasa," Katambi alisema.

Alisema pia wakazi wa Mkoa wa Dodoma ambao wanaelekea Mkoa wa Kilimanjaro, wataanza kunufaika na huduma za shirika hilo baada ya kufanya uzinduzi kwa sababu mkoa huo upo katikati ya nchi.

Mkuu huyo wa wilaya pia alisema kuwapo kwa usafiri wa ndege kutawezesha kukuza uchumi wa taifa na kupata unafuu wa nauli kutokana na kuwapo kwa ushindani wa kibiashara.

"Tunawapongeza kwa kuleta ushindani kwa sababu Shirika letu la Ndege la ATCL nalo lilishaanza kutoa huduma, ujio wenu kama washindani wa kibiashara utaleta manufaa kwa wananchi na serikali kwa ujumla," Katambi alisema.

Alisema kuna shughuli nyingi zinafanyika katika jiji hilo hivyo kuwapo kwa ndege zinazosafirisha abiria ni kukuza uchumi wa Watanzania.

Kaimu Mkurugenzi wa Precision Air, Patrick Mwanri, alisema kilichowashawishi kutoa huduma za usafiri za Dar es Salaam kuelekea Dodoma na Kilimanjaro kuelekea Dodoma ni kutokana uwekezaji mkubwa unaofanyika katika jiji baada ya serikali kuhamia Dodoma.

# DC apiga marufuku nyumba za ibada katikati ya makazi

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, amepiga marufuku nyumba za ibada zilizo kwenye maeneo yasiyo rasmi ikiwamo katikati ya makazi ya watu kuondoka na kwenda maeneo yaliyotegwa kwa ajili ya makanisa.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kupinga mimba na ndoa za utotoni pamoja na mauaji ya vikongwe, albino inayotekelezwa na Kanisa la Tanzania Assemblies of God, Mkoa wa Shinyanga.

Macha alisema serikali imetoa uhuru wa kuabudu na inaheshimu dini zote na madhehebu yote, lakini upo utaratibu wa kuzingatia.

Awali mchungaji wa kanisa hilo, Adrehem Mlelwa, alisema Mkoa wa Shinyanga ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa mimba na ndoa za utotoni , mauaji ya vikogwe, albino, imani za kishirikina, mambo ambayo ni chukizo kwa Mungu na kikwazo kwa maendeleo.

Katika kuunusuru Mkoa wa Shinyanga kuepukana na matendo maovu TAG ushirika wa Kahama limepanga kufanya mikutano 100 ya kupinga mimba na ndoa za utotoni, mauaji ya vikogwe, albino na ushirikina.

Mikutano hiyo itafanyika Halmashauri ya mji wa Kahama, Ushetu, Msalala, Kishapu, Wilaya ya Shinyanga Vijijini .

Mwangalizi wa kanisa hilo, Elias Gilbert, alisema kanisa linatambua juhudi zinazofanywa na serikali za kugharamia elimu bila malipo ili jamii iweze kuepukana na ujinga ambao ni kikwazo kwa taifa lolote linalopenda maendeleo .

Alisema ili kuunga mkono juhudi hizo, kanisa lilitoa mifuko ya saruji 50 kwa ajili ya shule za msingi za Nyandekwa iliyopo Halmashauri ya mji wa Kahama, Bulyanhulu, Ilogi Kabala, iliyopo katika Halmashauri ya Msalala na Iboja iliyopo Ushetu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**VIWANJA/MASHAMBA**

**NAFASI ZA KAZI UALIMU /** certificate au diploma /english/ mathematics /SST na science 0656490706/0655628640


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



Yunisi Ruben Mmari anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S3310-0034** kilichotolewa na Baraza la Taifa Mitihani mwaka 2012 katika shule ya Sekondari Lukani. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **BNG/RB/1391/2019**

215149702

## ANATAFUTWA NA POLISI



**Linda Dickson Nyange** Anatafutwa na Polisi kwa tuhuma za kutoroka na **Vyeti na fedha.** Donge nono litatolewa kwa yeyote atakaempata. Ripoti ya Polisi namba **MG/RB/1441/2019**

**Namba ya Simu: 0623 420410**

115150002

**RE; THE LAND ACT NO 4 OF 1999**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF REF NO; MG/LD/33230**

**REGISTERED OWNER; LAMIC SHARUA MASUDI.**

**LAND; PLOT NO. 1668(PN) BLOCK "Q"LUKOBE**

**MOROGORO MUNICIPALITY**

**APLICANT; LAMIC SHARUA MASUDI**

**TAKE NOTICE** that the ORIGINAL **LETTER OF OFFER** to the land described above is said to be lost and that I intend to issue a REPLACEMENT **OF THE ORIGINAL LETTER OF OFFER** in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within thirty days (30) from the date of this pubication.

**THE ORIGINAL LETTER OF OFFER** is found,should be delivered to the office of the ;Municipal Director,Morogoro Municipal Council,P.o box 166 Morogoro.

***Issued by:***

215150202

**Summons to appear (0.VR.20(1) of (CPC).**
**(Substituted Service)**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**

**AT DAR-ES-SALAAM**

**MISCELLANEOUS LAND APPLICATION NO, 11/2017**

**IDDI ATHUMAN NDAKI..................APPLICANT**

**VERSUS**

**SALUM SAID..............................RESPONDENT**

**TO**
**SALUM SAID**
**MINDU STREET**
**MOROGORO**

**WHEREAS:** The above named Applicant has instituted an application against you,you are here by summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorised on 26th day of APRILY 2019 at 09:00 hrs before Mgonya.J. (Chamber No.06) in the morning.

Taken notice that,in default of your appearence on that day the Application will be heard and determined in your absence.

Given under my hand and the seal of this Court,this **28th day of MARCH.**

DEPUTY REGISTRAR

215149902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHIWANDA FARM** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.999 ATL** AINA YA **ISUZU FOWARD** RANGI NYEUPE .CHASSIS NAMBA **NRR33C43001211** ENGINE NAMBA **6HH1257763** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. POLISI TAARIFA: **MB/RB/143/2019**

215149802

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
21/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 02/04/2019 kampuni ya **NKIRA TRADING AND INVESTMENT LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea **TUNDUMA kupitia VIGWAZA** gari hilo lenye namba za usajili:
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   1. **IT 4147**
   2. **IT 2923**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **10.70** |
| **Upana** | - | **mita** | **3:00** |
| **Kimo** | - | **mita** | **3.20** |

Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115151202

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
21/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 02-04-2019 kampuni ya **MASKI & SONS CONSTRUCTION LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea **LUGOBA (PWANI) kupitia VIGWAZA,** gari hilo lenye namba za usajili: **T 324 AAM / T 226 BSY**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **IT 0398 / IT 0309**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **22.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.20** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115151002

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
21/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe 02-04-2019 kampuni ya **GLOBAL LEADER ENTERPRISES (T) LIMITED** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA** kupitia VIGWAZA, gari hilo lenye namba za usajili: IT 0398 / IT 0309 na T 578 DHR/ T 956 DHT
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **IT 0398 / IT 0309**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **23.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.50** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

3. **T 578 DHR / T 956 DHT**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | **mita** | **20.00** |
| Upana | - | **mita** | **2.85** |
| Kimo | - | **mita** | **5.20** |

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115151302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MIKONGENI**

**Usimamizi wa mirathi No; 2/2019**

**Ombi la RAMADHANI RAJABU ATHUMANI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAJABU ATHUMANI KINUKE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 12/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 12/03/2019

215150102


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# EMERY aiona 4-bora Arsenal

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery (pichani chini), amesisitiza kwamba 'Washika Bunduki' hao wanastahili kumaliza nafasi nne za juu Ligi Kuu England msimu huu.

Baada ya kukumbana na vipigo kutoka kwa Chelsea na Manchester City, wengi waliamini kwamba Emery angeweza kumaliza kwenye nne bora na kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, raia huyo wa Hispania, anaamini kwamba Arsenal wana nafasi ya kumaliza kwenye nne bora msimu huu.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana Jumatatu dhidi ya Newcastle United, Emery amedai kwamba, kikosi chake kina nafasi kubwa ya kumaliza kwenye nne bora.

Alisema akiliambia Gazeti la Express: "Tunakwenda kumaliza kwenye nne bora na tupo kwenye ushindani wa ukweli.

"Najua wengi wanaweza kubeza hili, lakini ni wazi kwamba, tupo kwenye nafasi nzuri ya kumaliza katika nne bora."






# HAZARD amsikilizia Zidane

**MADRID,** Hispania

KUTUA kwa Eden Hazard pale Real Madrid ni suala linalosubiriwa uamuzi wa Zinedine Zidane ambaye bado hajawasha taa ya kijani kwa uhamisho huo, kwa mujibu wa Gazeti la Marca.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ameshabainisha hadharani kuhusu kuvutiwa na Zidane katika siku za hivi karibuni na akisema kwamba alikuwa shabiki mkubwa wa gwiji huyo wa Ufaransa wakati akikua.

Gazeti la Marca, limeripoti kwamba harakati za kumchukua nyota huyo wa Chelsea kutua hapo Santiago Bernabeu zipo vizuri, na ndio sababu kubwa kwa Blues hao kumsajili winga wa Borussia Dortmund, Christian Pulisic, wakati wa kipindi cha majira ya joto Januari.

Ripoti zimedai kwamba kitu pekee kinachokosekana kwa Hazard kuwa mchezaji wa Madrid kwa sasa ni kusubiri kuwashiwa taa ya kijani na Zidane, ambaye ndiye anasubiriwa kutoa maamuzi.

Uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kipindi cha majira ya joto kilichopita ulikwama baada ya Chelsea kutaka kiasi cha euro milioni 150.

Hazard kwa sasa huu ni msimu wake wa saba hapo Stamford Bridge, akiwa amefunga mabao 105 katika mechi 340 na alikuwa nguzo ya mafanikio ya Chelsea kutwaa ubingwa mwaka 2015 na 2017.

# Solskjaer amgeukia Pogba Man United

**MANCHSTER,** England

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer amesema kuwa kiungo wake, Paul Pogba ana furaha ndani ya klabu ya Manchester United licha ya ndoto za kijana huyo raia wa Ufaransa kutaka kutimkia Real Madrid.

Pogba, ambaye mara kadhaa amekuwa akihusishwa kutakiwa na klabu ya Madrid, amesikika akiizungumzia timu hiyo alipohojiwa wakati alipokuwa akiitumikia timu yake ya taifa.

"Real Madrid ni ndoto za kila mtu, ni moja kati ya klabu kubwa duniani, Zidane ndiye kocha pale kwa sasa, ni ndoto kwa kila mtoto na kila mchezaji," alisema Pogba.

"Kwa sasa ninayofuraha hapa Manchester, ninacheza nikiwa na kocha mpya. Kwa sasa nipo Manchester. Hatujui kitakachotokea baadaye."

Hata hivyo, kocha wa Real, Zinedine Zidane amewahi kusikika akisema anavutiwa na Mfaransa huyo mwenzake, Pogba.

"Navutiwa kweli na Pogba na mnafahamu hilo, namfahamu mno, yeye ni mchezaji wa aina ya kipekee na mwenye uwezo wa kufanya vitu vingi kwa sababu ya ujuzi na uwezo aliyo nao.

"Anafahamu namna ya kushambulia na kujilinda, siku zote husema anaipenda Real Madrid," amesema kocha huyo wa Real Madrid, Zinedine Zidane.




Lakini Solskjaer amesisitiza kuwa kijana huyo aliyeweka rekodi ya usajili ndani ya United kwa sasa ya pauni milioni 89 ataendelea kusalia Old Trafford kwa kuwa anahitaji kuijenga upya.

"Nisingependa kuzungumzia wachezaji wa timu nyingine bila shaka, lakini hii ni changamoto nyingine baada ya kutoka mapumziko. Wachezaji wamekuwa wakipatikana muda wote na mazingira tofauti," alisema Solskjaer.

"Paul ni mwelewa na mwenye heshima, ambaye alimjibu maswali yake, Zidane ambaye ni alama ya Ufaransa, kocha bora na amewahi kuwa mchezaji mwenye uwezo mkubwa," alisema Solskjaer.

Bosi huyo wa United pia amethibitisha kuwa Romelu Lukaku na Anthony Martial watakuwa tayari kurejea uwanjani baada ya kuuguza majeraha.



# DE LIGT tayari kujiunga Barcelona

**AMSTERDAM,** Uholanzi

'DOGO' wa maajabu wa Ajax, Matthijs de Ligt, anapanga kukamilisha uhamisho wa kwenda Barcelona baada ya 'Blaugrana' hao kupewa punguzo maalumu la kumsajili beki huyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 anachukuliwa kama mmoja wa nyota watakaotisha zaidi baadaye Ulaya, na wengi wamebainisha kwamba atafuata nyayo za mchezaji mwenzake wa Ajax, Frenkie de Jong na kukamilisha uhamisho wa kutua hapo Barcelona kipindi cha majira ya joto.

Akizungumza na Gazeti la De Telegraaf, Mkuu wa Kitengo cha Michezo wa Ajax, Valentijn Driessen, amedai kwamba dili la De Ligt kwenda Barcelona ni la uhakika.

Alinukuliwa tena na gazeti la The Sun akisema: "Ni wazi kwamba De Ligt ataondoka Ajax kwenda Barca.

"Ajax ilishaweka wazi kwamba Barcelona hawahitajiki kulipa zaidi kwa ajili ya Matthijs, tofauti na klabu nyingine."

Klabu kama Bayern Munich, Juventus na Manchester City zote zimekuwa zikimnyatia 'dogo' huyo, lakini inaonyesha wazi kwamba, Barcelona inaelekea kushinda kwenye mbio hizo, shukrani kwa mahusiano yao mazuri na Ajax.

Walipigana na klabu nyingine Ulaya kuweza kumsajili De Jong kwa pauni milioni 65 Januari mwaka huu, na kiungo huyo atatua pale Nou Camp majira ya kipindi cha joto.




# FEKIR afunguka uhamisho Liver

**LYON,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Lyon, Nabil Fekir, amefunguka kuhusu kutakiwa na Liverpool wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita, akibainisha kwamba anaweza kuangalia uwezekano wa kuondoka kwenye kikosi hcho cha Ligue 1 mwishoni mwa msimu huu.

Mfaransa huyo alikuwa akihusishwa na mpango wa kutua pale Anfield kipindi cha majira ya joto kilichopita na iliaminiwa kwamba uhamisho wake ulikaribia kukamilika kabla ya kushindikana dakika ya mwisho, baada ya uvumi kudai kwamba Liverpool walihofia hali yake ya majeraha ya goti.

Akizungumza na Telefoot, Fekir amesisitiza kwamba goti halikuwa tatizo kwake, lakini amebainisha kuwa kushindwa kuhamia Liverpool kumempa nguvu ya kujituma zaidi uwanjani.

Alisema: "Mengi yalizungumzwa kuhusu goti langu, kama ambavyo mara zote nimekuwa nikisema, hakuna tatizo katika goti langu. Ndio inatokea, na hiyo inanifanya mimi niendelee kujituma zaidi uwanjani."

Hata hivyo, alipoulizwa kama atashawishi kuondoka kupindi cha majira ya joto au kubakia Lyon, Fekir amekiri kwamba kwa sasa hajui nini kitatokea.

Aliongeza: "Kwa uhakika sijui, kwa sasa nipo Lyon, rais ananiamini, ni nzuri kwa sababu kila msimu unakuwa tofauti, lakini tumeanza majadiliano na rais na tutaona nini kitatokea."

Rais wa Lyon, Jeah-Michel Aulas, pia amebainisha kwamba kwa sasa klabu yake haijafanya mazungumzo ya kuhusu mkataba mpya na Fekir, huku akisema: "Tunazungumza kuhusu kila kitu, yeye ni nahodha wetu, tunazungumza na wakala wake pia, na ni kweli kwamba tunathamini mchango wa Nabil na kama kutakuwa na uwezekano wa kuongeza mkataba wake wa muda mrefu, litakuwa jambo la kuvutia zaidi."

# Spalletti ambwatukia Icardi kujiona 'Father'




**MILAN,** Italia

LUCIANO Spalletti amembwatukia Mauro Icardi (pichani), kwa kuwahujumu mashabiki wa Inter baada ya mshambuliaji huyo wa Argentina kuachwa kwenye kikosi hicho cha Nerazzurri wakati kikifungwa bao 1-0 na Lazio Jumapili.

Icardi hajaichezea klabu hiyo tangu Februari baada ya mazungumzo yake ya mkataba mpya kushindikana, lakini alirudi katika mazoezi na kikosi cha kwanza wakati wa mapumziko ya mechi za kimataifa na alikuwa katika uwezekano wa kuanza kwenye mchezo huo wa Jumapili, lakini baadaye akaondolewa kikosini.

Inter kwenye mchezo huo ilicheza kwa kiwango cha chini, lakini mashabiki wanaamini kwamba, kama Icardi angecheza wangeweza kupata matokeo tofauti.

Spalletti hakusita kulizungumza hilo waziwazi pale alimpomtupia lawama nyingi Icardi.

"Kwa leo, chaguo pekee kwa Icardi lilikuwa ni kukaa nje, ni sawa kwa wengine wamecheza kwa kiwango walichoweza," alisema akinukuliwa na Sky Sports Italia.

"Pamoja kwamba wengine walistahili kucheza, lakini yeye si kila kitu kwa klabu, yeye si mtu wa kubadilisha matokeo.

"Watu wanasema tunapoteza mechi nyingi tukiwa bila Icardi, lakini timu haikufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa miaka mingi wakati yeye akiwa kikosi cha kwanza.

"Wachezaji wachache ndio wanaweza kuleta tofauti, Messi anaweza kufanya hivyo, lakini sio Icardi."

## HABARI MICHEZO

### KWA UFUPI

**ZIDANE AMUWEKA BALE KIPORO**
KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema mustakabali wa baadaye wa nyota wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale, 29, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United na kurudi Tottenham, utaamuliwa mwishoni mwa msimu. **(Talksport)**

**GUARDIOLA ATAJA MAKOMBE MA4**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema timu yake inahitaji kucheza kama mashine endapo inahitaji kutwaa mataji manne msimu huu. **(Telegraph)**

**KROOS, BALE KUMPISHA POGBA**
MANCHESTER United itaulizia uwezekano wa kumpata Gareth Bale ama kiungo Mjerumani Toni Kroos, 29, kama sehemu ya dili lolote la Real Madrid kuipata huduma ya kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26. **(AS, via Express)**

**BARCA YAMUULIZIA MATA**
BARCELONA imewasiliana na baba na wakala wa Juan Mata, 30, kuhusu uwezekano wa kumpata kiungo huyo wa Man United ambaye mkataba wake unamalizika majira ya joto. **(Sun)**

**WELBECK 'KUFUNGWA' ARSENAL**
ARSENAL itampa mkataba mpya mshambuliaji wa England, Danny Welbeck, 28, wakati huu akianza mazoezi kabla ya msimu kumalizika. **(Independent)**

**ZIDANE KUAMUA KWA HAZARD**
MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Eden Hazard, 28, kuhamia Real Madrid kutategemeana na Zinedine Zidane kufanikisha uhamisho wa kiungo huyo wa kimataifa wa Ubelgiji. **(Marca)**

**SOLSKJAER AMKUBALI WAN-BISSAKA**
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, yupo tayari kutoa ofa ya pauni milioni 35 kwa beki wa kulia wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka, 21. **(Mail)**

**MARCELO SASA KUBAKI MADRID**
BEKI wa kushoto wa Brazil, Marcelo, 30, amebadili mawazo yake na sasa anataka kubaki Real Madrid kufuatia kurudi kwa Zinedine Zidane kuinoa miamba hiyo ya Hispania. **(AS)**

**HERRERA AGOMEWA UNITED**
MANCHESTER united imekataa kukubaliana na kiungo Mhispania Ander Herrera, 29, ambaye anataka kulipwa pauni 200,000 kwa wiki. Mhispania huyo atamaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu na amekuwa akitakiwa na miamba ya Ufaransa Paris St-Germain. **(Mirror)**


**EVERTON YAMTAKA JUMLA GOMES**
KOCHA wa Everton, Marco Silva, anatumai klabu hiyo inaweza "kuitumia fursa nzuri" waliyonayo na kumsajili jumla kiungo wa Barcelona na Ureno, Andre Gomes, anayeichezea kwa mkopo- ambaye pia anawindwa na Inter Milan. **(Liverpool Echo)**

**VERON ATABIRIA MASTAA SPURS**
KIUNGO wa zamani wa Inter na Manchester United, Juan Sebastian Veron, ambaye alicheza mechi ya manguli katika uwanja mpya wa Tottenham mwishoni mwa wiki, anaamini Spurs itawavutia wachezaji wengi wakubwa kutokana na uwanja wao mpya. **(Mirror)**

**BENITEZ AMTETEA ALMIRON KUTUPIA**
KOCHA wa Newcastle United, Rafael Benitez, amemtetea kiungo wa Paraguay, Miguel Almiron, 25, kwa kushindwa kufunga mechi sita za ugenini. **(Times)**

**REDKNAPP AMTAKA NOBLE UKOCHA**
KOCHA wa zamani wa West Ham, Harry Redknapp, angependa kumuona kiungo wa England na nahodha Mark Noble, 31, akifanya kazi ya ukocha na kuinoa klabu hiyo baada ya kutundika daluga. **(Star)**

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH: NAONEWA LIVERPOOL

### Sijafunga katika michezo michache, lakini kuna baadhi ya wachezaji ambao wana mabao sawa na mimi ila...

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool, Mohamed Salah, amejibu kukosolewa kwake baada ya ushindi muhimu wa mabao 2-1 walioupata Jumapili dhidi ya Tottenham, akisema maswali juu ya kiwango chake hivi karibuni si sahihi.

Salah alikuwa sehemu muhimu ya ushindi huo hapo Anfield, baada ya mpira wake wa kichwa alioуelekeza kwa kipa wa Spurs, Hugo Lloris, kusindikizwa kimyani na Toby Alderweireld aliyejifunga na hivyo kuipa Liverpool ushindi katika dakika ya 90.

Nyota huyo wa kimataifa wa Misri ambaye hadi sasa ana mabao 20 na pasi za mwisho ['assists'] nane msimu huu- amekuwa akiandamwa baada ya kucheka na nyavu mara moja tu katika mechi 11 zilizopita.

Lakini mshindi huyo wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa msimu uliopita, amepuuzia kukosolewa huko kwa kusema kuwa lengo lake ni katika kuisaidia Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu.

"Sijafunga katika michezo michache, lakini kuna baadhi ya wachezaji ambao wana mabao sawa na mimi, ila watu wanasema wachezaji hao wana msimu mzuri katika maisha yao," aliiambia Sky Sports.

"Kuna wachezaji watatu ama wanne na hakuna yeyote anayezungumza kuwahusu. Wanasema wanamsimu mzuri na ni mimi pekee ambaye ninamsimu mbaya.

"Ninataka kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu - hicho ndicho kitu muhimu zaidi kwangu."

Kipigo hicho kwa kikosi cha Mauricio Pochettino, kinaifanya Liverpool kukaa kileleni mwa ligi hiyo kwa pointi mbili zaidi, na bao hilo la kujifunga la Alderweireld lilikuja baada ya Lucas Moura kusawazisha la kwanza lililofungwa na Roberto Firmino.

Salah alikubali wanaume hao wa Jurgen Klopp kuwa chini ya ubora wao, lakini akasisitiza pointi ndiyo kitu cha muhimu zaidi kuliko kitu chochote kile.

"Huwezi mara zote kucheza vizuri, lakini kitu cha muhimu ni kupata pointi," alisema.

"Timu kubwa mara zote inatafuta namna ya kupata pointi na hicho ndicho tulichokifanya.

"Kila mechi sasa ni ngumu. Unatakiwa kujiweka mwenyewe katika mbio. Mechi yetu ijayo ni dhidi ya Southampton na wanapigania maisha yao.

"Unapaswa kuchukulia kila mechi kama changamoto. Tottenham ilicheza vizuri na walikaribia kupata pointi. Sasa tunachukulia hilo mechi baada ya mechi."

## HABARI MICHEZO

# YANGA NA SILAHA 20 NDANDA BILA AJIBU

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI jumla ya nyota 20 wa kikosi cha mabingwa wa kihistoria nchini, Yanga, leo alfajiri kilitarajiwa kuanza safari kueleka Mtwara tayari kwa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya wenyeji Ndanda FC, ambao umepangwa kupigwa Alhamisi katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona, kitaendelea kumkosa nahodha wake, Ibrahim Ajibu anayeendelea kuwa nje ya uwanja akiuguza majeraha ya mguu.

Ofisa Habari wa Yanga, Dismas Ten, alinukuliwa jana akisema Ajibu ataendelea kukosekana kikosini kupisha majeraha madogo aliyo nayo, huku Juma abdul akirejea kikosini baada ya kupona majeraha yake.

"Ibrahim Ajib bado tutaendelea kumkosa kikosini kutokana na majeraha ya mguu, lakini jambo jema ni kwamba Juma Abdul amerejea kikosini na atakuwa sehemu ya msafara wa kikosi chetu, mchezo utakuwa mgumu lakini maandalizi tuliyoyafanya yanatosha kutupa matokeo mazuri," alisema.

Yanga itashuka katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona, ikiwa na morali ya juu kutokana na kutinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA kufuatia kuitoa Alliance ya Mwanza kwa mikwaju ya penalti 4-3 baada ya dakika 90 za kawaida kumalizika zikiwa sare ya bao 1-1.

Kwa upande wake, kocha wa timu hiyo Mwinyi Zahera, amesema katika hatua hii ya mzunguko wa pili hakuna mchezo mwepesi, hivyo wanaenda Mtwara wakifahamu wanaenda kukutana na upinzani kutoka kwa wenyeji wao.

Yanga inaendelea kuongoza ligi ikiwa na pointi 67 huku wakicheza michezo 28 sawa na Azam yenye alama 59, wakati Simba ikiwa nafasi ya tatu na pointi zake 57 kutokana na kucheza mechi 22.



Nahodha wa Simba, John Bocco, akishangilia moja kati ya mabao mawili aliyoifungia Simba dhidi ya Mbao FC wakati wakishinda 3-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri juzi. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Bocco: Haikuwa rahisi 'kuchana' Mbao

**Na Somoe Ng'itu,** MOROGORO

BAADA ya timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mbao FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi mkoani hapa, nahodha wa Simba, John Bocco, amesema haikuwa "kazi rahisi" kuwafunga wapinzani hao kutoka jijini Mwanza.

Bocco alifunga mabao mawili katika mchezo huo, bao lingine lilifungwa na mshambuliaji Mnyarwanda, Meddie Kagere na kuwafanya mabingwa hao watetezi wafikishe pointi 57 wakicheza mechi 22.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bocco alisema Mbao FC waliingia huku wakijiamini na wakicheza "faulo za makusudi" ili kuwaondoa mchezoni, lakini hawakufanikiwa kutimiza malengo yao.

Mshambuliaji huyo alisema pia mbinu zao zilikuwa bora zaidi ukilinganisha na za Mbao FC, jambo ambalo liliwapa nafasi nzuri na hatimaye kupata ushindi katika mechi hiyo baada ya mchezo wa mzunguko wa kwanza kupoteza.

"Kwanza namshukuru Mungu tumemaliza salama, mechi haikuwa rahisi, ila mbinu zetu zilikuwa bora zaidi, sasa tunajipanga kwa mchezo unaofuata," alisema Bocco ambaye juzi alicheza kwa dakika 73 na nafasi yake kuchukuliwa na kiungo, Said Ndemla.

Naye nahodha wa Mbao FC, David Mwasa, alisema kilichowafanya wapoteze mechi hiyo ni kutotumia vema nafasi walizotengeza huku akikiri Simba ni timu kubwa.

"Tulishindwa kutumia vizuri nafasi tulizopata, wenzetu wamezitumia na wamefanikiwa, mechi ilikuwa ngumu, Simba ni timu kubwa, wao walicheza kwa presha na sisi tulicheza kwa presha, tunawapongeza kwa ushindi waliopata," alisema Mwasa.

Beki huyo aliongeza kuwa walilazimika kutumia nguvu kwa sababu ya kuwapunguza Simba kasi na waliamini wangeendelea kupata matokeo mazuri dhidi ya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya mzunguko wa kwanza kuwafunga kwa bao 1-0 katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.Simba | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4.Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.Mbao | 31 | 9 | 9 | 13 | 19 | 32 | 36 |
| 15.Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.Ruvu Shooting | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17.Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Shime aahidi ushindi mnono Twiga Stars

**Na Mwandishi Wetu**

ILI kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime, amesema anataka kupata ushindi mnono kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) utakaochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Twiga Stars inawakaribisha wadada wenzao wa Congo katika mechi ya kwanza ya kuwania tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki itakayofanyika mwakani jijini Tokyo, Japan.

Shime aliliambia gazeti hili kuwa amewaandaa wachezaji wake kupambana kuhakikisha wanamaliza "kazi" hapa nyumbani kwa kufunga mabao mengi.

**Alisema wachezaji aliowaita katika kikosi chake wanauzoefu na mashindano ya kimataifa na wamejipanga kuendelea kuwapa furaha mashabiki wa soka wa hapa nchini.**

"Kila siku ninawakumbusha kuhakikisha wanakuwa makini na watulivu, hii itatusaidia kupata ushindi mkubwa na mnono hapa nyumbani, sisi ndio tutaitangaza vema nchi kimataifa, wanaweza," alisema Shime.

Aliongeza kuwa kikosi chake kina mchezaji majeruhi mmoja tu ambaye ni Aisha Hamza, huku nyota wengine wakiwa katika hali nzuri na wanafanya mazoezi.

"Aisha tutamkosa katika mechi hizi mbili, atakaa nje kwa muda wa wiki sita," alisema Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Edna Lema.

Timu hizo zinatarajia kurudiana Aprili 9, mwaka huu jijini Kinshasa na mshindi wa jumla atakutana na Equatorial Guinea katika mechi za raundi ya pili zitakazochezwa kati ya Agosti 26 hadi Septemba 3, mwaka huu.

Michezo

Jumanne Aprili 2, 2019

Nipashe

## Hazard amsikilizia Zidane



HABARI UK. 28

MUNGU WANGU!...



Beki wa kushoto wa Tottenham, Danny Rose, akishindwa kuamini kilichotokea dakika ya 90 kufuatia beki wa kati, Toby Alderweireld, kujifunga wakati akitaka kuokoa mpira wa kichwa wa mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah (jezi 11), kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Anfield na wenyeji hao kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# AUSSEMS AKILI JESHINI, AIPOTEZEA MAZEMBE

## ●●● Apanga kushusha kikosi tofauti kesho, huku akieleza kila mechi ushindi lazima na kwamba...

**Somoe Ng'itu,** MOROGORO

KOCHA Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema kwa sasa akili na mawazo yake ipo 'jeshini' kwa 'wajeda' wa JKT Tanzania na si kuufikiria mchezo wa hatua ya robo fainali wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya TP Mazembe unaotarajiwa kuchezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Simba ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walitinga hatua hiyo baada ya kuifunga AS Vita ya Kongo mabao 2-1 na kumaliza katika nafasi ya pili ya hatua ya makundi wakiwa na pointi tisa nyuma ya vinara wa kundi lao, Al Ahly ya Misri waliomaliza na alama 10.

Aussems alitoa kauli hiyo juzi baada ya timu yake kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mbao FC na kueleza kwamba ameiweka TP Mazembe "kiporo" kwa sababu anajiandaa kwanza kuikaribisha JKT Tanzania hapo kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani hapa.

Mbelgiji huyo alisema anaendelea kukiandaa kikosi chake kucheza mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kutoa nafasi kwa kila mchezaji kuitumikia timu hiyo ili kufikia malengo waliyojipangia msimu huu.

"Akili yetu iko kwa ajili ya mechi ya Jumatano, ni lazima nifanye mabadiliko katika kikosi kitakachocheza, kila mchezaji atapata nafasi kulingana na mchezo uliopo na hii itatusaidia kuendelea kuimarika, JKT kwanza, TP Mazembe itafuata," alisema Aussems.

Aliongeza kuwa licha ya kuwa na siku chache za maandalizi ya mchezo huo wa kimataifa, benchi lake la ufundi linajipanga kuendelea kujiimarisha kwa sababu wanahitaji kushinda mechi zote zinazowakabili.

"Najua tutakuwa na siku mbili kabla ya kucheza na Mazembe, Alhamisi na Ijumaa, kitu muhimu ni kuhakikisha wachezaji wanakuwa na utimamu wa mwili, kila mchezaji atacheza na anatakiwa ajue majukumu yake," aliongeza kocha huyo ambaye anasaidiwa na Mtanzania, Dennis Kitambi.

Naye Kocha Msaidizi wa Mbao FC, Fulgence Novatus, alisema kuwa kikosi chake kilizidiwa uwezo na wapinzani wao Simba, ila bado wana nafasi ya kujirekebisha na kufanya vizuri katika mechi zinazofuata.

"Hatukufanya vizuri, tuliwaruhusu watawale mpira muda mrefu na kuwaacha huru, kuna makosa tulifanya na ndio yalitugharimu katika siku ya leo (juzi), kwa kifupi ligi hii ina ushindani na kila mechi ni sawa na fainali," alisema Novatus.

Kikosi cha Mbao kiliondoka mkoani hapa juzi usiku kurejea Mwanza ili kujiandaa na mechi yake nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho.

## Yanga warudishiwa Tiboroha, Igangula

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), imeyapitisha kwa mara nyingine majina ya waliomba kuwania nafasi ya uenyekiti katika Klabu ya Yanga, Dk. Jonas Tiboroha na Mbaraka Igangula, ambao sasa wanaruhusiwa kuendelea na mchakato huo.

Tiboroha na Igangula walisimamishwa kuendelea na kampeni zao za kugombea nafasi hiyo baada ya uchaguzi wa kwanza kusimamishwa na wanachama ambao walifungua kesi kupinga uchaguzi huo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Ally Mchungahela, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema wagombea wa nafasi ya uenyekiti wanaruhusiwa kuendelea kugombea katika uchaguzi mpya wa klabu hiyo ambao utafanyika Mei 5, mwaka huu.

"Mei 5, mwaka huu ndiyo siku ambayo uchaguzi mpya wa Yanga utafanyika na kutakuwa na siku za kuchukua fomu na usahili wa wagombea na mambo mengine.

"Wale wagombea walikuwapo katika mchakato wa awali kugombea nafasi mbalimbali wataendelea kama kawaida na wataungana na wapya ambao wataanza kuchukua fomu kuanzia Aprili 2, mwaka huu," alisema Mchungahela.

Wiki iliyopita serikali ililiagiza Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kwa kushirikiana na TFF, kuhakikisha uchaguzi wa Klabu ya Yanga unafanyika ndani ya siku 30.

Akitoa maagizo hayo wiki iliyopita jijini Dodoma, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuph Singo, alisema migogoro iliyokuwapo huko nyuma imeshafikia tamati, hivyo uchaguzi ndani ya Klabu ya Yanga ni lazima sasa ufanyike.

"Nailekeza BMT iwaelekeze TFF kuhakikisha taratibu zote za uchaguzi zinafuatwa na uchaguzi ndani ya Klabu ya Dar es Salaam Young Africans unafanyika ndani ya siku 30," alisema Singo huku akiwasihi viongozi, wanachama na wapenzi wa Yanga kutoanzisha migogoro wala vikwazo vingine bali kutumia hizo siku 30 kufanya uchaguzi ili kupata viongozi watakaoisimamia na kuiongoza ili kuendelea kufanya vizuri katika mpira wa miguu ndani na nje ya nchi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002